Alhamisi Septemba 5, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580015
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



## Kuachiwa ndege ya ATCL kwaibua furaha, gumzo

UKURASA 4




UKURASA 13

# Magufuli awasamehe Makamba na Ngeleja

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

**UPINZANI WALIA SHERIA MTANDAO NA TAKWIMU**

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni imetaka serikali kupeleka bungeni miswada ya marekebisho ya Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sheria ya Takwimu na Sheria ya Huduma za Vyombo...

UKURASA WA 7

**IDADI WAHANDISI WANAWAKE YAPAA**

BALOZI wa Norway nchini, Elizabeth Jacobsen, amesema ushirikiano wa nchi hiyo na Tanzania umewezesha...

UKURASA WA 7

**MCHINA, MAOFISA TBS KIZIMBANI**

RAIA wa China na maofisa wawili kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu...



Rais Dk. John Magufuli akizungumza jambo na Mbunge wa Misungwi, Charles Kitwanga, baada ya kufungua Mkutano wa Mashauriano wa Mwaka wa Bodi ya Usajili Wabunifu na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Bodi ya Usajili Makandarasi (CRB), Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), na wadau wa sekta ya ujenzi , jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Lissu aahirisha kurejea nchini

UKURASA 4

# Ubaguzi Afrika Kusini washutumiwa kila kona

**BUNGE**, serikali watoa tamko zito, raia wao nchini wahakikishiwa usalama... *Endelea ukurasa wa 2*

**MICHEZO** KIUNGO MTANZANIA ATAMANI KUTUA EPL UK.31

**MAONI, KATUNI** UK.6

# JPM awasamehe Makamba, Ngeleja

**Na Mary Geofrey**

SAKATA la sauti za vigogo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) zilizokuwa zinasambaa kwenye mitandao ya kijamii, limechukua sura mpya baada ya vigogo wawili kati ya waliokuwa wanasikika kuisema serikali kudaiwa kumwangukia Rais John Magufuli.

Vigogo wanaodaiwa kumwomba msamaha Rais ni aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) na Mbunge wa Bumbuli, January Makamba na Mbunge wa Sengerema, William Ngeleja.

Rais Magufuli aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano wa siku mbili wa pamoja wa wadau wa sekta ya ujenzi unaohusisha Bodi za Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Usajili wa Wahandisi (ERB) na Usajili wa Makandarasi (CRB), jijini Dar es Salaam.

Alisema vigogo hao na wengine walikuwa wakimtukana na sauti zao zilisambaa kwenye mitandao ya kijamii lakini wawili kati yao (bila kutaja idadi) walijitokeza kumwomba msamaha na kuamua kuwasamehe.

"Nakumbuka hivi karibuni kuna watu fulani fulani hivi walinitukana weee na nika 'prove'(nikathibitisha) sauti ni zao 'more than hundred percent' (zaidi ya asilimia 100). Nikawafikiria nikaona hata nikiwaacha wapelekwe kwenye Kamati ya Maadili (ya Chama Cha Mapinduzi- CCM) adhabu itakuwa kubwa, nikaona ninyamaze.

"Lakini wakajitokeza wawili kati yao wakaniomba msamaha, nami nikajiuliza na mimi kila siku naomba msamaha kwa Mungu na nasali ile sala ya baba yetu utusamehe makosa yetu kama tunavyowasemehe wengine.

Nikaona hawa waliokuja kuniomba msamaha na kweli ya dhamira yao nisipowasamehe ni bataki na maumivu makubwa ndani ya moyo wangu," alisema Rais Magufuli.

"Niliamua nikawasamehe, waliniomba msamaha wakanigusa, nikaona hawa ni vijana bado wanatafuta maisha na mimi nikaamua kuwasamehe nikasahau kabisa."

Mbali na Ngeleja na Makamba, sauti zingine zilizosambaa ni za makatibu wakuu wastaafu wa CCM, Yusuph Makamba na Abdulrahman Kinana na Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Benard Membe.

Aliwasihi Watanzania kuwa na desturi ya kusameheana kwa sababu wote ni watoto wa Mungu, hivyo wanatakiwa kusameheana na kuwa huru.

Rais Magufuli alisisitiza kuwa wadau hao wa ujenzi nchini wanatakiwa kufanya kazi kwa ushirikiano na kusameheana ili kutimiza wajibu wao kikamilifu.

"Mtu akikuudhi na kukutukana kiasi gani ni muhimu kusamehe na kuuishi upendo wa kweli wa kusamehe. Hata ninyi (wataalamu wa ujenzi) sameheaneni na mimi nimewasamehe," alisema.

Nipashe iliwatafuta Ngeleja na Makamba ili kuzungumzia msamaha huo wa Rais, lakini Makamba aliomba apigiwe baadaye lakini hakujibu na Ngeleja simu yake ya kiganjani iliita bila majibu.

Alipotafutwa na Nipashe bungeni jijini Dodoma jana, January Makamba alikataa kulizungumzia suala hilo akisema: "Mkubwa akishasema, sisi wadogo hatuwezi kusema tena."




Spika wa Bunge, Job Ndugai (wa pili kushoto), Spika wa Kenya, Justin Muturi (kushoto), Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid (wa tatu kushoto) na Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai, wakimsikiliza Mbunge kutoka Bunge la Kenya anayewakilisha watu wenye ulemavu, Dennitah Ghati, wakati wa Mkutano wa 50 wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika unaoendelea mjini Zanzibar jana. PICHA: BUNGE

# Ubaguzi Afrika Kusini washutumiwa kila kona

**Romana Mallya na Enock Charles**

YAMEIBUKA malalamiko kadhaa kuhusu Watanzania waishio Afrika Kusini kuwa waathirika wa vurugu zinazoendelea nchini humo.

Hata hivyo, pamoja na Watanzania hao kuiomba Tanzania iseme lolote, yenyewe imesema inaunga mkono na imeridhishwa na hatua ambazo tayari Rais Cyril Ramaphosa, amekwisha zichukua.

Katika video fupi iliyosambaa mtandaoni jana, mama mmoja aliyejitambulisha kama Mtanzania anayeishi nchini humo, alidai vurugu hizo zimemrudisha nyuma kiuchumi kwa kuwa vitu vyake vyote katika eneo lake la biashara vimechomwa moto.

Alisema licha ya kuwa na vibali vyote vinavyohitajika vya kuishi na kufanya biashara nchini humo, lakini amepoteza kila kitu.

"Unaona duka jinsi lilivyo wamemaliza kila kitu, friji zote zimeungua yaani wametuacha kama vile tunatakiwa tuanze moja hakuna unachoweza kufanya na mpaka sasa hivi hatujui serikali yao inaongea kitu gani yaani," alilalamika mzungumzaji huyo.

Bungeni jijini Dodoma, sakata hilo liliwainua vitini wabunge wa pande zote mbili waliouomba uongozi kuahirisha shughuli za Bunge za jana ili kujadili jambo hilo la dharura.

Elibariki Kingu, Mbunge wa Sindiga Magharibi (CCM), alisema amepata taarifa kupitia vyombo vya habari juu ya mauaji ya Waafrika Afrika Kusini.

"Mheshimiwa Naibu Spika, nimetumiwa taarifa na Mtanzania mwenzangu kwamba maduka yake yamechomwa moto, lakini pia tumeshuhudia kwenye taarifa mbalimbali raia wenzetu weusi kutoka Zimbabwe na Nigeria wakichomwa moto wakiwa hai.

"Kwa sababu Tanzania imekuwa taifa ambalo limesimamia ukombozi wa mataifa mengi ya Bara la Afrika na katika kipindi hicho, taifa letu halijawahi kukaa kimya dhidi ya uzalilishaji.

"Tanzania ilipaza sauti dhidi ya unyanyasaji wa watu weusi uliokuwa ukifanywa na serikali ya makaburu. Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba mwongozo wa kiti chako, ipi kauli ya Bunge lako na serikali dhidi ya mauaji ya watu weusi yanayoendelea Afrika Kusini?" Kingu alihoji.

Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche (Chadema), alisimama na kutoa hoja ya Bunge kuahirisha shughuli zake za jana ili kujadili jambo hilo la dharura.

"Watu wetu, Waafrika wenzetu, hakuna Mchina wala mzungu, ni Waafrika kwa Waafrika wanauawa. Nchi yetu ilikuwa kiongozi katika kupigania uhuru wa Afrika na Waafrika Kusini waliishi hapa kwetu.

"Vilevile, Rais wa nchi (Dk. John Magufuli) ni Mwenyekiti wa SADC, ni jambo la dharura. Tunahitaji kauli ya dharura na nchi nyingi

INAENDELEA UK 8

## ... Awataka wahandisi kupunguza gharama

**Na Mary Geofrey**

RAIS John Magufuli amewataka wabunifu na wakadiriaji majenzi, kushusha gharama za uchoraji ramani ili Watanzania waweze kumudu kutumia huduma hizo nchini.

Rais Magufuli alitoa wito huyo jana jijini Dar es Salaam, alipokuwa akifungua mkutano wa pamoja wa bodi za Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Usajili wa Wahandisi (ERB) na Usajili Makandarasi (CRB).

Alisema wataalam hao wamekuwa wakitoza gharama kubwa za ramani hadi Sh. milioni mbili wakati ramani zenyewe wanazichukua kwenye mitandao ya intaneti.

"Nawasihi mpunguze gharama za kuuza ramani za nyumba ili mpate wateja wengi kwa sababu ramani mnauza kuanzia Sh. milioni mbili, wakati mwingine mnazi'google' kwenye mitandaoni alafu mnamtumia mtu hadi tatu achague lakini mnauza gharama kubwa," alisema Rais.

Alisema gharama ya Sh. milioni mbili ni kubwa hivyo Watanzania wengi hawawezi kumudu hivyo ni muhimu kuzishusha.

Aidha, Rais Magufuli alizitaka bodi hizo kuendelea kuongeza ukali na kuchukua hatua kwa watendaji ambao hawatimizi wajibu wao kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuwafutia leseni zao.

Alisema licha ya watalaam wanaokiuka taratibu kuchukuliwa hatua changamoto iliyopo ni makandarasi wanaofukuzwa kusajiliwa kwa majina mengine.

"Kama ni kufukuzwa kazi afukuzwe kabisa, akafuge samaki, msiwa 'entertain' (msiwaendekeze'), kuwe na kampuni chache zinazofanya kazi vizuri kuliko kuwa na nyingi zisizo na tija," Rais Magufuli alisema.

Kadhalika Rais Magufuli aliagiza watendaji wa bodi hiyo kwa kushirikiana na Wizara ya Katiba na Sheria kubadili sheria ambazo zinawabana makandarasi na wataalam hao wa ndani kufanya kazi za miradi mikubwa.

Alisema mbali na upungufu ya kisheria makandarasi wengi hawana udhubutu wa kuomba tenda na wengine huingia mitini kabla hawajamaliza kazi.

Awali Mwenyekiti wa Bodi ya CRB, Consolata Ngimbwa, aliiomba serikali kuweka mazingira wezeshi ya kisheria ya utekelezaji wa miradi ya serikali ili makandarasi wa nje kushirikisha makandarasi wa ndani katika kazi zao.

"Tumejitahidi sana kuwaunganisha makandarasi wetu kwenye miradi mbalimbali mikubwa inayojengwa na wageni lakini kwa sababu hakuna sheria inayowalazimu kutoa kazi kwa wazawa ni kuomba na wanaoombwa wanatoa wanavyojisikia na hata malipo wanayotoa si mazuri sana,

INAENDELEA UK 8

## TANGAZO


Ya kwanza Tanzania!
Tigo Mobile Shop
Top Up
Buy Bundle
Home Internet by tigo
Value Added Service
FREE 100GB
Home Internet kutoka Tigo
Sasa unaweza kumudu matumizi ya router au modem yako kupitia simu ya mkononi na ufurahie huduma ya Tigo Home Internet yenye kasi ya 4G+
Tembelea duka lolote la Tigo uunganishwe.
Home Internet by tigo
Pakua App ya Tigo Pesa kutoka
Google Play
App Store
tigo

## Mapya safari ya Lissu kurejea nchini Jumamosi

**Na Enock Charles**

ALIYEKUWA Mbunge wa Shingida Mashariki na Mwanasheria Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, ameahirisha mpango wa kurejea nchini keshokutwa kutoka Ubelgiji kama alivyoahidi.

Lissu amesema kuwa ameahirisha safari ya kurejea nchini kutokana na kutopata kibali cha madaktari wake.

Akizungumza na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC), mwanasheria huyo amesema kuwa hataweza kurejea nchini Jumamosi kama alivyosema awali kwa kuwa ana ratiba ya kumuona daktari wake Oktoba mosi mwaka huu na Oktoba 8, mwaka huu.

"Nilisema mwanzoni kuwa nitarudi tarehe 7 Septemba ya mwaka huu ambayo ni Jumamosi hii ya keshokutwa… lakini mpaka sasa sijapata ruhusa ya daktari wangu, daktari wangu ameniambia ataniona tarehe 1 Oktoba na kwa mara ya mwisho tarehe nane Oktoba," alisema Lissu alisema

Kuhusu kuapishwa kwa aliyekuwa mbunge mteule wa Jimbo la Singida Mashariki, Miraji Mtaturu, ambaye ndie aliyechukua nafasi yake, Lissu amesema hiyo haimpi shida kwa vile suala hilo bado lipo mahakamani na endapo atashinda kesi mbunge huyo mpya atatenguliwa na yeye kurejeshewa kiti chake.

"Hiyo haina athari yoyote kwa shauri lililopo mahakamani… wabunge huwa wanachaguliwa, wanaapishwa, wanatumikia ubunge halafu mahakama ikipata ushahidi kwa aliyetenguliwa alitenguliwa kinyume cha sheria, anafutiwa ubunge," alisema.

Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam Jumatatu ilishindwa kutoa zuio la muda la kuapishwa Mtaturu baada ya kuahirisha kutoa uamuzi wa kusikiliza kesi ya msingi hadi Septemba 9, mwaka huu, hivyo juzi mbunge huyo mpya aliapishwa ikuwa siku ya kwanza ya Mkutano wa Bunge wa 14.

Katika taarifa aliyoitoa kwa vyombo mbalimbali awali, Lissu alisema kuwa angerejea nchini Septemba 7, mwaka huu akitokea Ubelgiji alipo kwa ajili ya matibabu tangu mwaka jana.

Mwanasheria huyo ambaye amehudumu kama mbunge kwa takribani mihula miwili, alivuliwa ubunge baada ya taarifa iliyotolewa na Spika wa Bunge, Job Ndugai, kwa maelezo kuwa amekuwa mtoro wa mikutano ya Bunge pamoja na kutokujaza fomu za maadili ya watumishi wa umma.

Septemba 7, juzi Lissu alishambuliwa kwa kupigwa risasi zaidi ya 30 na watu wasiojulikana karibu na nyumbani kwake Area 'D' jijini Dodoma majira ya mchana akiwa katika gari lake wakati akitoka kwenye kikao cha bunge.



Mwenyekiti wa chama cha wachapishaji Tanzania (PATA), Gabriel Kitua, akifungua maonyesho ya vitabu 2019, yaliyofanyika katika Maktaba Kuu ya Tanzania, Barabara ya Bibi Titi Mohamed, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kuachiwa ndege ATCL kwaibua furaha, gumzo

**Na Waandishi Wetu**

MUDA mfupi baada ya ndege aina ya Airbus A220-300 ya Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), Afrika Kusini kuachiwa, imeibuka furaha na gumzo kutoka kwa viongozi mbalimbali wa serikali.

Kaimu Balozi wa Tanzania nchini humo, alisema mlalamikaji hakutarajia kuwa Tanzania itashinda kwenye kesi ya kuzuiwa kwa ndege hiyo.

Kesi hiyo ilifunguliwa na mkulima Hermanus Steyne katika Mahakama Kuu ya Gauteng, nchini humo, kwa alichodai anaidai serikali ya Tanzania Sh. milioni 373 baada ya mali zake kutaifishwa na serikali ya awamu ya kwanza Januari 1982.

Ndege hiyo ilishikiliwa Agosti 23, mwaka huu, baada ya kwenda nchini humo kwa safari za kawaida, kutokana na kuanzishwa kwa njia mpya ya safari za ndege za ATCL nchini humo.

Akizungumza na televisheni ya taifa jana kwa njia ya simu, Kaimu Balozi wa Tanzania nchini humo, Richard Lupembe, alisema ndani ya mahakama hiyo ilikuwa ni furaha kubwa kwa kuwa awali hawakuwa na matarajio ya kushinda kwa kuwa waliofungua kesi walikuwa na matarajio ya ushindi na ndiyo maana wamekata rufani.

"Lakini baada ya Jaji kusema tumeshinda sisi na wao wameshindwa, kila mtu akaingia mlango wake anaoujua yeye, sisi tukabaki na furaha yetu na kuanza kujipanga kuelekea uwanja wa ndege," alisema.

Kuhusu kukata rufani, alisema walioshindwa wanajitahidi kukata rufani, lakini hakuzuii ndege hiyo kuondoka nchini humo na kufanyakazi kama kawaida.

"Wamekata rufani kwenye Mahakama ambayo imesikiliza shauri la awali," alisema Balozi Lupembe.

"Baada ya hukumu ya Jaji hawakutakiwa kujibu lolote zaidi ya kusikia hukumu...alitushtaki anatudai, lakini baada ya kujitetea imeonekana hatudai chochote na tumeruhusiwa ndege yetu kuondoka."

**WAZIRI WA UJENZI**

Jijini Dar es Salaam Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alithibitisha kuachiwa kwa ndege hiyo na kueleza kuwa itarudi katika safari zake za kawaida kwa sababu Watanzania wanapenda kupanda ndege za kwao.

Waziri huyo alisema hayo jana wakati akitoa shukrani kwa Rais John Magufuli kwa kufungua mkutano wa pamoja wa wadau wa siku mbili wa wajenzi wanaohusisha Bodi za Usajili wa Wabunifu Majengo na Makadiriaji Majenzi (AQRB), Usajili wa Wahandisi (ERB) na Usajili Makandarasi (CRB).

Alisema ndege hiyo imeshaachiliwa, tayari kwa kuanza kufanya safari zake, na kwamba serikali inaendelea na ratiba ya kununua ndege nyingine mbili kama walivyokuwa wamepanga.

"Mheshimiwa Rais, ndege yetu imeachiliwa rasmi, najua mtakuwa mnapokea taarifa kutoka kwenye mitandao ya kijamii, lakini kwa mfumo wa kiserikali hii ndio taarifa rasmi," alisema Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI**

Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Damas Ndumbaro, aliyekuwapo mahakamani, alisema:

"Tanzania imeridhishwa na uamuzi wa mahakama na Rais Magufuli ameshapewa taarifa ya hukumu ya ndege yetu."

Aidha, katika hukumu hiyo mahakama imemtaka mlalamikaji Steyne aliyepeleka kibali cha kushikiliwa ndege hiyo alipe gharama za kesi hiyo kwa walalamikiwa.

Mlalamikaji huyo ambaye alipata kibali cha kuishikilia ndege hiyo, alisema hajaridhishwa na hukumu na kwamba amekata rufani.

Taarifa zilizoripotiwa na vyombo mbalimbali vya kimataifa imeeleza kuwa rufani hiyo inatarajiwa kusikilizwa.

Wakili wa Steyn, alisema: "Tumearifiwa kuwa ACSA (kampuni inayoendesha viwanja vya ndege Afrika Kusini (ACSA) ipo katika harakati za kuiachia ndege. Kama ndege itaondoka Afrika Kusini, mteja wangu atapoteza bima yake, na jambo hili (rufani) linahitaji kusikilizwa kwa haraka."

Aidha, iliripotiwa kuwa rufani ilianza kusikilizwa jana katika Mahakama hiyo.

**MCHUANO MAHAKAMANI**

Wakati wa usikilizaji wa kesi hiyo mahakamani, jopo la wanasheria wa Tanzania waliopelekwa nchini humo walieleza kuwa amri hiyo ilitolewa kimakosa na kutaka iondolewe.

Wakili wa mlalamikaji, Wakefied, alisisitiza kuwa kuna kesi ya msingi ya kujibu na kuitaka mahakama kuangalia vigezo vya madai hayo na kuvitendea haki.

**WAZIRI KABUDI**

Naye Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema jijini Dar es Salaam kuwa wanasheria wa Tanzania wakiongozwa na Dk. Ndumbaro wakishirikiana na timu ya wenzao nchini humo wamewezesha ndege hiyo kuachiwa.

"Dk. Ndumbaro alipelekwa Afrika Kusini tangu Jumamosi iliyopita kwa ajili ya kusimamia shughuli hiyo, uamuzi wa mahakama wa kuiachia ndege yetu umetolewa leo (jana) saa nne asubuhi ambapo ni saa tano kwa mujibu wa saa za Afrika Mashariki," alisema wakati akitoa tiketi za ndege kwa wanafunzi 100 wanaokwenda masomoni Israel.

Alisema ndege hiyo imeachiwa kwa sababu za serikali ya Tanzania na wanasheria wake walizitoa mahakamani.

"Taarifa zaidi zitatolewa baadaye, mahakama leo imesoma hukumu yake baada ya sisi kuwasilisha hoja zetu Jumanne (juzi) kuomba mahakama itengue uamuzi uliotolewa na Jaji aliyesikiliza kesi hiyo bila ya sisi kuwapo mahakamani.

Hayo ni maamuzi ya mahakama yaliyotolewa, lakini utekelezaji wake tutazidi kufahamishana hapo baadaye," alisema.

Prof. Kabudi alisema serikali inaendelea kufuatilia baada ya uamuzi huo ni nini kitaendelea.

"Ninawashukuru wanasheria wetu waliotuwakilisha kwenye kesi hii wakiongozwa na Naibu Waziri Dk. Ndumbaro na timu ya mawakili Afrika Kusini," alisema.

**BOSI ATCL**

Mtendaji Mkuu wa ATCL, Ladislaus Matindi, alisema: "Tutaendelea na safari zetu kwa kuwa kesi iliyokuwa mahakamani haituhusu sisi wala hawakulishtaki shirika."

***Imeandikwa na Romana Mallya, Mary Geofrey, Mariam Magili na Rahma Kisilwa (Tudarco)***



Mfanyakazi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Amani Mollel, akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana na wenzake wawili na kusomewa mashtaka matano ikiwamo matumizi mabaya ya madaraka na kusaidia kuingizwa nchini kwa marobota ya mifuko ya plastiki isiyokuwa na viwango yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 73. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Upinzani wataka Sheria Makosa Kimtandao, Takwimu zifumuliwe

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni imetaka serikali kupeleka bungeni miswada ya marekebisho ya Sheria ya Makosa ya Kimtandao, Sheria ya Takwimu na Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari kwa kuwa inaamini sheria hizo zimesababishwa kuminywa kwa uhuru wa mawasiliano.

Akiwasilisha bungeni maoni ya kambi hiyo kuhusu Muswada wa Sheria ya Serikali Mtandao ya Mwaka 2019, Mbunge wa Viti Maalum, Catherine Ruge, alisema pamoja na malengo mazuri ya uanzishwaji wa Mamlaka ya Serikali Mtandao, kambi hiyo inaona yatakwama ikiwa serikali haitafanya marekebisho ya sheria hizo.

Ruge ambaye aliwasilisha maoni hayo kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa kambi hiyo katika Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ruth Mollel, alisema sheria hizo zinadhibiti mawasiliano ya kimtandao na upatikanaji wa taarifa.

"Ili sheria inayopendekezwa iweze kufanya kazi na kufikia malengo yaliyokusudiwa, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza serikali ilete miswada ya marekebisho ya sheria nilizozitaja hivi punde ili vipengele pingamizi vinavyozuia uhuru wa mawasiliano ya kimtandao na upatikanaji wa taarifa na takwimu za serikali vifutwe.

"Kwa kufanya hivyo, kutatoa mwaya kwa sheria inayopendekezwa kufanya kazi. Ikiwa jambo hili halitafanyika, basi sheria hii inayopendekezwa itakuwa imetungwa tu kuweka kumbukumbu kwamba kuna Sheria ya Serikali Mtandao lakini kimsingi utekelezaji wake utakuwa ni changamoto kubwa.

"Pia, serikali itambue kwamba wajibu wake mkubwa ni kutoa huduma kwa wananchi ambao wengi wao takribani asilimia 70 wanaishi vijijini ambako kuna changamoto za mawasiliano ya kimtandao.

"Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaikumbusha serikali kushirikiana na sekta binafsi hususan kampuni binafsi za simu, kujenga miundombinu ya mawasiliano katika maeneo ya vijijini ili wananchi waishio vijijini waweze kunufaika na mfumo huu wa Serikali Mtandao," alisema.

Awali, akiwasilisha muswada huo bungeni jana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki, alisema kutungwa kwa sheria hiyo kutaisaidia serikali kuongeza udhibiti wa kuboresha utekelezaji wa Serikali Mtandao nchini.

Alisema sheria hiyo pia itasaidia kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya serikali, usimamizi wa matumizi ya rasilimali Tehama katika taasisi za umma, kuboresha mazingira ya biashara (mifumo ya leseni, kodi, benki, usimamizi wa ardhi na utoaji wa hati za kusafiria) na kuimarisha utendaji kazi serikalini.

# Mbivu mbichi kesi vigogo wa Simba Sept. 17

**Na Hellen Mwango**

HATIMA ya kesi ya kughushi na kutakatisha Dola za Marekani 300,000 inayowakabili vigogo wa Klabu ya Simba, akiwamo Rais Evance Aveva na wenzake kama wana kesi ya kujibu au la kujulikana Septemba 17, mwaka huu baada ya upande wa Jamhuri kufunga ushahidi wake jana.

Jana upande wa Jamhuri ulifunga ushahidi wake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Mbali na Aveva, washtakiwa wengine ni Mwenyekiti wa zamani wa Kamati ya usajili wa klabu hiyo, Zackaria Hanspoppe na Makamu wa Rais Godfrey Nyange, maarufu kama Kaburu.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Leonard Swai, alidai kuwa baada ya kuita mashahidi 10 na kuwasilisha vielelezo mbalimbali umefunga ushahidi wake.

Awali mahakamani hapo, Mtaalamu wa Maabara ya Sayansi Jinai, kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, jijini Dar es Salaam, Faustine Mashauri, alidai Septemba 4, 2017 akiwa katika ofisi za maabara hiyo, alipokea bahasha kutoka kwa Mkurugenzi wa Takukuru iliyokuwa na vielelezo pamoja na barua ya maombi ya uchunguzi wa vielelezo hivyo.

Alidai, vielelezo hivyo ni vile vinavyobishaniwa na visivyobishaniwa na kwamba vinavyobishaniwa ni hundi kutoka benki ya CRDB na fomu ya maombi ya kuhamisha fedha kutoka benki hiyo kwenda benki nyingine.

Alidai baada ya kufanya uchunguzi alibaini sahihi zilizokuwa katika hundi zinafanana na sahihi zisizobishaniwa za Nyange na Aveva wanazotumia katika shuguli zao za kila siku.

"Mheshimiwa hakimu uchunguzi ulibaini kitaalamu kwamba nyaraka zilisainiwa na Aveva na Nyange," alidai Mashauri.

Alidai kuwa baada ya kukamilisha uchunguzi, aliandaa ripoti na kuiwasilisha Ofisi ya Takukuru.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka 10 ikiwamo kula njama, kughushi, kuwasilisha nyaraka za kughushi, kutoa maelezo ya uongo na utakatishaji wa fedha.

Katika shtaka la kughushi linalowakabili washtakiwa wote, inadaiwa katika tarehe hizo hizo kwa pamoja walighushi hati ya malipo ya kibiashara ya Mei 28, 2016 wakionyesha kwamba nyasi bandia zilizonunuliwa na Simba zinathamani ya dola 40,577 sawa na zaidi ya Sh. milioni 90 huku wakijua si kweli.

Pia katika mashtaka mengine inadaiwa Aveva, Godfrey Nyange na Hans Poppe kati ya Machi 10 na Septemba 30, 2016, waliwasilisha nyaraka za uongo kuonyesha Simba imenunua nyasi bandia zenye thamani ya Dola za Kimarekani 40,577.



## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Tamasha la Jinsia lije na suluhu changamoto zaidi*

**HARAKATI** za kupigania haki za wanawake na watoto na makundi mengine kama watu wanye ulemavu ni endelevu nchini na duaniani kwa ujumla.

Ni makundi yanayohitaji utetezi kutokana kuathiriwa na mambo mbalimbali katika jamii, kubwa kuwanyima haki zao za msingi kama elimu, umiliki wa rasilimali, ikiwamo ardhi na ushiriki katika maamuzi, kwa kutaja baadhi.

Kwa miaka kadhaa wanawake wamekuwa nyuma kutokana na mila na utamaduni katika jamii zetu kuwabagua kwa kuwanyima elimu katika umri wa kusoma, hivyo kuwakosesha fursa ya maendeleo maishani.

Wanawake leo hii wanaendelea kukwama kupata maendeleo kutokana na mila na utamaduni kuwanyima haki ya kumiliki ardhi ambayo ndio msingi wa maendeleo pamoja na kurithi mali.

Kikwazo hiki kinawanyima fursa wanawake wengi kujiendeleza kwa kufanya shughuli za kujiongezea kipato hususan za ujasiriamali, ambazo zinampasa kuwa na dhamana ya kupata mkopo kutoka taasisi za fedha na benki.

Kundi hilo kukosa uwakilishi katika vyombo vya maamuzi kimekuwa kilio kwa kuda mrefu kutokana na uamuzi wa sera, mipango na sheria kutungwa bila kushurutishwa, hivyo kutowatatulia changamoto zinazowahusu.

Vile vile, wanawake, watoto na watu wenye ulemavu wamekuwa waathirika wakuu wa matukio ya ukatili kama kuuawa, kubakwa, kulawitiwa, kutelekezwa, kuteketwa na mengine mengi ambayo kimsingi yanakiuka utu wa binadamu.

Hata hivyo jitihada kadhaa zimekuwa zikifanyika kukabiliana na changamoto zote tulizozitaja dhidi ya makundi haya kupitia utungaji wa sheria, sera na kutekeleza mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo nchi yetu imeiridhia.

Kwa kuwa jitihada hizo ni endelevu, tunatarajia kuwa Tamasha la Jinsia linalotarajiwa kufanyika nchini mwezi huu, litakuwa sehemu sahihi ya kuzipitia, kuzijadili na kufanya tathmini kuhusiana na changamoto hizo kwa lengo la kuhakikisha kuwa zinaendelea kutatuliwa na kuyapunguzia mzigo wa kunyanyaswa, kufanyiwa ukatili na kuyanyima fursa makundi hayo.

Tamasha hilo ambalo huratibiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na kufanyika nchini kila baada ya miaka miwili linalotarajia kufanyika kuanzia Septemba 24 hadi 27, mwaka huu, tunatarajia kuwa limefanyika miaka 25 tangu kuanzishwa kwa mtandao huo, hivyo litakuwa na masuala mengi ya kujadili kwa lengo la kumkomboa mwanamke.

Tunasema hivyo kwa kuwa matamasha haya yamekuwa yakiwakutanisha wanawake kutoka kila pande za dunia wakiwamo waliopata mafanikio makubwa kujadili masuala ya kuwakomboa pamoja na mtoto wa kike, hivyo kuna umuhimu wa kufanya maandalizi mazuri ikiwamo kuandaa vizuri ajenda za kujadili.

Ajenda hizo zijikite zaidi katika hali halisi ya changamoto zinazowakabili wanawake na mtoto wa kike nchini na kuja na maazimio ambayo yatakabidhiwa kwa serikali ili yatekeleze katika kutunga sera, sheria na uaandaaji wa mipango na mikakati ya maendeleo.

Tunatarajia kuona Tamasha hilo likileta matokeo chanya katika ukombozi wa mwanamke kutokana na mabadiliko katika maendeleo ya wanawake yaliyoletwa na Mkutano wa Nne wa Wanawake Duniani uliofanyika Beijing nchini China mapema miaka ya tisini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# *Masanduku huduma ya kwanza kwenye mabasi, malori ni aibu*

Na Augusta Njoji, DODOMA

**HUDUMA** ya kwanza huwa ni ya haraka anayopewa mwathirika wa ajali au ugonjwa wa ghafla.

Katika mazingira ndani ya mabasi, imeonekana kuwa ni ya hatari, kutokana na masanduku kubeba dawa zilizopitwa na wakati, pia kuwa na nyembe zenye kutu.

Madhumuni ya huduma hiyo ni kulinda maisha, kusaidia kufufua na kuzuia madhara ya namna hiyo, mpaka huduma ya kamili ya kidaktari itakapopatikana kwa kwenda hospitali au nyumbani kwa majeruhi.

Lakini ushuhuda wa kilichopo kwenye mabasi ni hatari, kwa kuwa hizo dawa au huduma atakayotakiwa kupewa mtu, inakuwa ngumu kuipata, kutokana na hali mbaya ya masanduku na vilivyomo ndani yake.

Masanduku ya huduma ya kwanza kwenye mabasi ya abiria na malori yana dawa zilizopitwa na wakati, nyembe zenye kutu na dawa zimemwagika ovyo.

Pia kuna kashfa wamekutwa nayo baadhi ya waendesha malori, kwamba masanduku yao yamejazwa kondomu.

Katika uhalisia unaotakiwa, sanduku la huduma ya kwanza linapaswa kuwa na 'plaster' au bandeji zinazonata, zikiwa salama kwa ajili ya kufunga vidonda na 'gauze' safi na salama ya kufunga majeraha makubwa, majisafi na salama, kripu bandeji, mkasi na dawa za kuzuia maumivu.

Sanduku hilo linapaswa kuwa na bandeji za pembe tatu, mipira ya mkononi (gloves) na 'tweezer' kwa ajili ya kuondolea vipande vya vitu kwenye ngozi.

Hiyo inaambatana na kuwapo daftari dogo la kuandikia huduma iliyofanyika, tarehe na saa husika, pia spiriti, pamba, sindano au pini. Nasema katka magari yetu, hali ni tofauti sana. Katika ukaguzi mdogo uliofanywa kwenye kituo cha mabasi yaendayo mikoani, kilichoko Igambilo mkoani Iringa, ilibainika masanduku hayakuwa na uwezo wa kumsaidia abiria anapopatwa na dharura ya ugonjwa, kwani vyote ndani yake vilikuwa vimepitwa na wakati.

Koplo Faustina Nduguru kutoka Kitengo cha Elimu kwa Umma, Makao Makuu ya Kikosi cha Usalama Barabarani, anasema amekumbana na dawa kuhifadhiwa kwenye mabakuli ya vyakula na zimepitwa na wakati, huku magari hayana kabisa masanduku aina hiyo.

Mwelimishaji huyo, anatumia fursa kusema madereva wanatakiwa kukagua masanduku yao kila wanapoanza safari na kujali uhifadhi wake, ili kuondokana na dhana ya kuweka kitu asikamatwe na wasimamizi wa sheria za usalama barabarani, wakati ndani hakuna vinavyotakiwa.

Koplo Faustina anasema, katika masanduku aliyoyakagua kwa mshtukizo, alikuta baadhi ya dawa zimemwagika na kuwapo chupa tupu.

Anawakumbusha madereva kutambua wajibu wao katika utunzaji masanduku hayo, kwa kuwa 'kila mtu ni abiria wa kesho' na atahitaji huduma itokanayo na masanduku hayo, akiwa safarini.

Pia anawakumbusha madereva walichojifunza kuhusu umuhimu wa matumizi ya sanduku la huduma ya kwanza na wajibu wa kukikagua kabla ya kuanza safari, lakini wanafanya kinyume, ambao ni uzembe.

Rai yake kwa wamiliki wa mabasi, watambue umuhimu wa masanduku hayo wanayoyatelekeza na mengine yaliwekwa tangu siku gari lilipoanza safari, dawa zake hazijawahi kubadilishwa.

Nitoe rai, hebu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsi, Wazeee na Watoto, kwa kushirikana na Jeshi la Polisi na wadau wengine, waongeze juhudi ya kutopa elimu kwa umma, hususan kwa madereva, kuhusu umuhimu wa masanduku yanayotakiwa kuwekwa na aina ya dawa zake.

Najua ndugu zetu wa polisi wa usalama barabarani ambao ndio wadau wakuu walishaanza, nihimize juhudi kuendelezwa zaidi.

# Wahandisi wanawake waongezeka hadi 500

**Na Juster Prudence, TUDARCo**

BALOZI wa Norway nchini, Elizabeth Jacobsen, amesema ushirikiano wa nchi hiyo na Tanzania umewezesha kuongezeka kwa wahandisi wanawake kutoka 96 mpaka 500 kwa sasa.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam katika mkutano wa wadau wa sekta ya ujenzi uliohusisha Bodi za Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), wahandishi na makandarasi, alisema mabadiliko hayo ni mafanikio makubwa ya kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye sekta hiyo.

Alisema tangu mwaka 2010 Norway imekuwa ikishirikiana na Tanzania kutoa mafunzo kwa wahandisi wanawake na hadi wako takriban 500 waliopata mafunzo na kupewa leseni kama waajiriwa na wataalamu wahandisi wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads).

Kwa mujibu wa balozi huyo, serikali hiyo imeshiriki kwenye miradi ya gesi wawekezaji ambapo faida yake inaweza kuchukua muda mrefu kupatikana.

"Kwa baadhi ya mazingira kama miradi ya gesi wawekezaji wamejitolea sana kufanya uwekezaji wa awali na ambapo faida yake inaweza ikachukua muda mrefu kupatikana," alisema Balozi Jacobsen.

Aidha, alisema Norway inasaidia nia ya Tanzania ya kufikia malengo ya uchumi wa kati kupitia sekta ya viwanda kwa kuongeza mapato ya makusanyo ya ndani. Kutokana na hali hiyo, alisema wanasubiri kwa hamu mfumo wa kuboresha mazingira ya kufanyia biashara nchini Tanzania, ili kuhakikisha sekta ya umma inakuwa na ufanisi na inasaidia uwekezaji katika sekta binafsi ili kuongeza mapato na kutengeneza ajira nchini.



Wafanyabiashara wadogo wakiendelea na shughuli zao katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana, licha ya Manispaa ya Ubungo kuwatangazia kuhama kwenda eneo la Kwa Beda, ili kupisha upanuzi wa barabara ya Morogoro na nyingine za eneo hilo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mchina, maofisa TBS kizimbani

**Na Mwandishi Wetu**

RAIA wa China na maofisa wawili kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS), wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana wakikabiliwa na mashtaka matano yanayohusiana na uingizaji wa mifuko isiyokuwa ya viwango.

Washtakiwa hao ni Zuopo Wang, anayefahamika kama Michael, ambaye ni Mkurugenzi kutoka Waadilifu Co Ltd na mkazi wa Mbezi Beach, Wasalim

Msilamgunda na Aman Mollel, ambao wote ni maofisa kutoka TBS, ambao wanaishi Baruti na Namanga jijini.

Mashtaka dhidi yao ni pamoja na kula njama ya kutenda kosa, kuongoza uhalifu ulioandaliwa, kupakua bidhaa kwa ajili ya soko la Tanzania bila kufuata mahitaji ya viwango vya Tanzania na matumizi mabaya ya madaraka.

Mbele ya Hakimu Mkazi Victoria Mwaikambo, washtakiwa hawakuruhusiwa kujibu mashtaka hayo kwa sababu yanaangukia chini ya Sheria ya Uhujumu Uchumi. Hakimu aliwataarifu washtakiwa kuwa mahakama hiyo haina

mamlaka ya kufanya chochote katika kesi hiyo.

Kwa kuwa hakukuwa na kizuizi cha dhamana, hakimu aliagiza washtakiwa kwenda Mahakama Kuu ambayo imepewa mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo, kwa ajili ya kuomba dhamana ikiwa wanahitaji, kesi hiyo iliahirishwa hadi Septemba 17, 2019, kwa ajili ya kutajwa kwa vile uchunguzi haujakamilika.

Wakili wa Serikali, Janeth Magoho, alidai kwamba katika muda na mahali kusipojulikana katika Jiji la Dar es Salaam, washtakiwa walikula njama kutenda kosa la kuidhinisha uingizaji ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mifuko isiyo ya viwango.

Inadaiwa kati ya Agosti 2 na 8, 2019 wilayani Ilala, wakiwa maofisa wa umma na kukiuka kazi zao, Msilamgunda na Mollel walitimiza lengo la kijinai kwa kuruhusu uingizaji nchini marobota 255 ya mifuko isiyokidhi viwango yenye thamani ya Sh. 73,885,531.97.

Mifuko kama hiyo, kwa mujibu wa upande wa mashtaka, haikukidhi viwango vilivyowekwa na TBS.

Ilidaiwa kipindi hicho hicho, akiwa sio ofisa wa umma, lakini akishirikiana na wafanyakazi hao wawili wa TBS, Wang alitimiza lengo la kijinai kwa kuruhusu uingizaji nchini marobota hayo.

Agosti 17, 2019 katika eneo la Mbezi Beach Makonde wilayani Kinondoni , raia huyo wa China alidaiwa kukutwa na wakaguzi kutoka Baraza la Mazingira Tanzania (NEMC) na TBS akiingiza marobota 255 ya mifuko hiyo kutoka China.

Upande wa mashitaka ulidai pia kuwa kati ya Agosti 2 na 8, 2019 wilayani Kinondoni, wakiwa wafanyakazi wa TBS na wakaguzi, kwa pamoja

Msilamgunda na Mollel watumia madaraka yao vibaya kwa kushindwa kutekeleza majukumu yao na majukumu yao na matokeo yake waliidhinisha uingizaji wa mifuko hiyo.

## Wakulima walia usitishwaji ununuzi mazao 5

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

WAKATI Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akiagiza viongozi wa mikoa kuhamasisha kusimamia matumizi ya mfumo wa stakabadhi ghalani kwenye ununuzi wa mazao ya wakulima kupitia vyama vya ushirika, Mrajisi Mkuu wa Ushirika nchini, ametoa waraka wa kusitisha ununuzi huo.

Kusitishwa kwa ununuzi huo kunafuatia barua ya Septemba 3, mwaka huu inayoeleza kuwa dhana na matumizi ya mfumo wa ushirika kwa ununuzi wa mazao matano umesitishwa.

Waraka huo uliosainiwa na Mrajisi Mkuu wa Ushirika, Tito Haule na kupelekwa kwa wakuu wa mikoa nchini, unaeleza kusitisha matumizi ya mfumo huo kwa mazao ya ufuta, choroko, dengu, mbaazi na soya.

Haule alidai katika waraka huo kwamba uamuzi wa sasa unasitisha pia kwa muda usiojulikana waraka namba moja wa mwaka 2019 uliotolewa mwezi Mei mwaka huu, kuhusu ruhusa ya ununuzi wa mazao yakiwamo choroko na dengu kwa mikoa ya Shinyanga na Mwanza.

Hata hivyo, waraka huo unaeleza jinsi ya utekelezaji wa hatua nyingine kwa vyama ambavyo tayari vilikuwa vimeshaanza kukusanya mazao ya wakulima na kusubiri minada ili kuondoa migongano.

Alipoulizwa kuhusu msimamo huo, Mrajisi Haule alisema, Tume ya Ushirika nchini haina malumbano na wakulima badala yake inafanyakazi nao kwa karibu hasa kwenye suala la kutafuta bei nzuri na kuweka rekodi za mazao na pato linalotokana na fedha za kigeni.

Hata hivyo, uamuzi huo wa kusitisha ununuzi umepokewa kwa hisia tofauti na baadhi ya wawakilishi wa wakulima, wakidai hatua hiyo ya Wizara ya Kilimo itawasaidia walanguzi wa mazao.

Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Wakulima Mkoa wa Ruvuma (SONAMCU), Salum Juma Brash, alisema wameipokea taarifa hiyo kwa masikitiko na kuziomba mamlaka kuingilia kati.

Alisema mfumo wa stakabadhi ghalani ni bora na umewasaidia wakulima kuwa na sauti na nguvu ya kupanga bei ya mazao yao mnadani, badala ya kuwatumia walanguzi wanaokwenda kwa wakulima vijijini na kununua kwa bei waitakayo wao.

Alidai kuwa uamuzi huo umewasukuma kumwandikia barua Rais Dk. John Magufuli ya kumuomba wizara itafakari uamuzi huo.

Pia wawakilishi wa Muungano wa Vyama vya Wakulima nchini (MVIWATA) kutoka katika mikoa saba, wamelaani hatua hiyo wakidai inawakumbusha uchungu ya nyuma.

Walisema chini ya mpango huo, MVIWATA na NFRA iliwasaidia wakulima kuwa na dhamana benki, kukopesha fedha za kupanua mashamba na kupata uhakika wa pembejeo.

# Ubaguzi Afrika Kusini washutumiwa kila kona

INATOKA UK 2

zimeshatoa kauli, sisi bado hatujazungumza.

"Watanzania walioko kule wanaishi kwa hofu. Kwa hiyo, ningependa uturuhusu Bunge lijadili jambo hili kwa dharura," Heche aliwasilisha.

Naye Mbunge wa Biharamulo, Oscar Mukusa (CCM), pia aliomba Bunge kuahirisha shughuli zake za jana ili kujadili jambo hilo la dharura kwa kuzingatia Tanzania sasa ni Mwenyekiti wa SADC na iliongoza kupambana na makaburu Afrika Kusini.

"Sasa naomba mwongozo wako Bunge liahirishe shughuli zake ili tujadili jambo hili tuweze kuishauri serikali namna ya kupambana na makaburu wenye rangi nyeusi ambao wanaelekea kuisambaratisha Afrika," alisema.

Hata hivyo, katika mwongozo wake, Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliyekuwa anaongoza kikao, alisema hana taarifa ya idadi ya Watanzania waliouawa, lakini akakiri kuna Waafrika waliouawa katika vurugu hizo.

Dk. Tulia pia alisema kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 47 na 48 za Bunge, chombo hicho hakiwezi kutoa kauli kwa maana ya miongozo ya wabunge hao ilivyoombwa.

"Lakini, serikali inao utaratibu wa mambo gani ya kuyatolea kauli na yapi si yakuyatolea kauli. Serikali inalifahamu jambo hili na kwa mujibu wa Kanuni ya 48K, serikali itakapoona inafaa, itatolea kauli jambo hili.

Baadhi ya wananchi wa nchi hiyo wameingia mtaani kufanya vurugu kwa kuwachoma na kuwajeruhi na kuharibu mali za raia wa nchi nyingine waliowekeza humo, kwa madai kuwa wamechukua ajira zao.

Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi, alipoulizwa kuhusiana tukio hilo lililotokea nchini humo na hatua gani ambazo imeshazichukua dhidi ya Watanzania waishio huko, alisema wameridhishwa na hatua ambazo tayari Rais Ramaphosa alizochukua.

Katika ukurasa wake wa Twitter, Rais Ramaphosa, ameeleza kulaani tukio hilo lililoendelea katika maeneo mbalimbali nchini humo na kumwagiza Waziri wake wa Ulinzi kuchukua hatua za haraka dhidi ya uhalifu.

Akizungumzia vurugu hizo na kama kuna Watanzania walioathiriwa nazo wakati akikabidhi tiketi za ndege kwa vijana 100 ambao leo wanakwenda Israel kufanya mafunzo ya mwaka mmoja ya ujuzi wa kilimo, Waziri Kabudi alisema Tanzania inampa moyo Rais Ramaphosa kuhusiana na kauli zake na hatua anazozichukua kukabiliana na hali hiyo.

"Kama yeye alivyosema, matukio hayo yametia doa nchi hiyo. Rais Ramaphosa ana kazi kubwa ya kuwarejeshea matumaini ya kuishi katika nchi zao Waafrika Kusini hasa waafrika walio wengi wasio na ardhi na ajira," alisema.

Alisema kwa taarifa walizonazo hadi wakati huo (jana mchana) hakuna Mtanzania yeyote aliyeuawa.



Vijana wakitoka kukata majani kwa ajili ya kulisha ng'ombe, katika eneo la Mbagala, Manispaa ya Temeke, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## ... Awataka wahandisi kupunguza gharama

INATOKA UK 2

kwa hiyo tunaomba utusaidie hili ili miradi ijayo tushiriki vizuri," alisema Ngimbwa.

Alisema pia watendaji wengi wa serikali kutoa uhuru kwa makandarasi kutumia benki na bima badala ya wao kulazimishwa kutumia benki tu na kwamba wanaomba miradi iongezeke ili lengo la kukuza makandarasi litimie kwa sababu miradi wanayopewa ni michache.

**MGOGO AIBUA SHANGWE**

Katika hatua nyingine Mchungaji Mashuhuri nchini, Daniel Mgogo, jana alizua taharuki na shangwe katika mkutano huo.

Mchungaji Mgogo alizua taharuki hiyo kwa kushangiliwa na washiriki katika mkutano huo zaidi ya 4,000, baada ya kuitwa na mshehereshaji kwa ajili ya kufanya maombi kabla ya kuanza mkutano huo.

Mchungaji Mgogo alitanguliwa na viongozi wengine watatu wa dini akiwamo Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhadi Mussa Salum na makasisi wawili wa Kanisa Katoliki na Anglikana.

Alipoitwa m Mchungaji Mgogo, watu walilipuka kwa shangwe na kuanza kumfurahia wakati akielekea mbele kwa ajili ya kusoma dua hiyo. Kutokana na shangwe hizo, Mchungaji Mgogo alianza kwa kumwomba msamaha Rais Magufuli kwa kile kinachotokea huku akimweleza kuwa ni udhihirisho kuwa ana wafuasi wengi wanaofuatilia kupitia mitandao ya kijamii.

Mchungaji Mgogo alianza kwa kumsifia Rais John Magufuli kwa kazi nzuri anazofanya na kusema kuwa Watanzania wapo nyuma yake na wanazikubali. "Rais Magufuli acha niseme tu hii fursa niliitafuta muda mrefu, acha nikueleze tu kuwa tumekuelewa, hata kama wahawajasema lakini wanakuelewa," Mchungaji Mgogo alisema.

## Adaiwa kumuua mtoto wa miaka 7 akimtuhumu kuiba Sh. 2000

**Na Renatus Masuguliko, GEITA**

JESHI la Polisi mkoani Geita linamshikilia Tabitha Marcko (38), mkazi wa kitongoji cha Kilimahewa, Kijiji cha Lulembela wilayani Mbogwe, kwa tuhuma za kumuua kwa kipigo mtoto wa dada yake, mwanafunzi wa darasa la kwanza Charles Deogratias (7), kwa madai ya kumuibia Sh. 2,000.

Akithibisha jana kutokea kwa mauaji hayo, Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Geita, Dismas Kisusi, alikiri kuwapo kwa tukio hilo akisema kuwa chanzo cha tukio hilo ni mtuhumiwa kumtuhumu mtoto huyo kuiba Sh. 2,000.

''Tayari tunamshikilia mtuhumiwa na upelelezi utakapokamilika tutamfikisha mahakamani kwa ajili ya hatua za kisheria,'' alisema Afande Kisusi.

Mwenyekiti wa kitongonji cha Kilimahewa lilipotokea tukio hilo, Hamis Budaga, alidai mtuhumiwa alianza kumpiga mtoto huyo toka saa tatu usiku na kisha kumfungia ndani ya nyumba na kwenda matembezini.

Alisema alipopata taarifa za tukio hilo alifuatilia na kumkuta mtoto akiwa katika hatua ya kukata roho.

## Tigo sasa yaja na 'Home Internet'

**Na Mwandishi Wetu**

WATEJA wa Kampuni ya mawasiliano ya Tigo, kwa mara ya kwanza watapata fursa ya kufurahia huduma ya 'Home Internet' yenye kasi ya 4G+ kwenye maeneo wanayoishi.

Huduma hiyo ni ya kwanza na ya kipekee Tanzania yenye ubunifu wa hali ya juu itakayowafanya wateja wafurahie intaneti ya 4G+ kwa kutumia vifaa vya 'router' au 'moderm'.

Kampuni hiyo ilizindua rasmi juzi huduma hiyo ambayo itatatua changamoto ambazo watumiaji wa mitandao ya simu hususan wale wa nyumbani wamekuwa wakikabiliana nazo.

Kupitia huduma hiyo, wateja wa Tigo sasa watapata fursa ya kupanga na kuchagua ni jinsi gani watatumia huduma ya intaneti, ikiwamo kununua vifurushi, kuongeza na kuangalia salio kupitia simu zao za mkononi.

"Mrejesho kutoka kwa wateja wetu umeonyesha kwamba kuna umuhimu wa uwepo wa huduma rahisi na ya uhakika ya mtandao wa intaneti majumbani. Hata hivyo, uzoefu katika matumizi ya huduma ya mtandao wa intaneti majumbani kwa wateja ni jambo lenye umuhimu mkubwa sana kwetu," ameeleza Mkuu wa kitengo cha Biashara wa Tigo, Tarik Boudiaf.

"Zama zile za mteja kusumbuka kutumia simu yake ya mkononi kama modem au kuhamisha line inayotumika kwenye modem au router ili kupata huduma ya intanet zimekwisha pita kitambo. Zama za kununua kifurushi ama kuongeza au kuangalia salio la laini inayotumika kwenye modem au router kwa kutumia kifaa kingine, ni jambo ambalo humpa mteja usumbufu, nazo zimekwisha pita kitambo," aliongeza Boudiaf. Kupitia huduma hiyo, alisema wateja sasa wanaweza kupangilia matumizi yao ya huduma ya intaneti kwa kuunganisha vifaa vya modem na router kutumia Tigo Pesa App.

"Lengo letu ni kuhakikisha kuwa kila mteja wa Tigo nchini ambaye atahitaji kutumia huduma yetu ya Home Internet anaunganishwa muda wote bila vikwazo vyovyote," ameongeza Boudiaf.

Kwa mujibu wa Boudiaf, huduma hii mpya iliyozinduliwa kwa mara ya kwanza nchini ni sehemu tu ya jitihada za kampuni ya Tigo ya kutoa huduma zinazojali maslahi ya wateja katika kuwapa uzoefu endelevu wa kijiditali kupitia mtandao wenye kasi zaidi wa 4G+.

Ili kujiunga na kufurahia huduma hiyo ya Home Internet, wateja wa Tigo wanaweza kununua modem au router katika maduka ya Tigo yaliyopo nchi nzima. Wateja wa Home internet wanaweza kuwasiliana na kitengo cha huduma kwa wateja wakati wowote, yani masaa 24 kwa siku.

HABARI MIKOANI

# Majeruhi sita wa ajali ya lori la mafuta Moro waruhusiwa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

HALI ya majeruhi waliolazwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro baada ya kuungua kwa moto uliosababishwa na lori la mafuta lililopinduka na kuwaka moto, zinaendelea vizuri, huku sita wakiruhusiwa.

Hata hivyo, majeruhi 10 wa ajali hiyo iliyotokea Agosti 10, mwaka huu eneo la Msamvu Itigi, Manispaa ya Morogoro, wanaendelea na matibabu.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Dk. Kusirye Ukio, akizungumza na Nipashe, alisema kuwa majeruhi hao 10 waliobaki wanaendelea vyema na matibabu na wameshaanza kufanya mazoezi mara mbili hadi zaidi kwa kutwa.

Alisema wengi wa majeruhi waliolazwa hospitalini hapo waliungua chini ya asilimia hamsini na jitihada za madaktari na wauguzi zimeendelea kuhakikisha zinafanikisha matibabu yao.

Hata hivyo, alisema changamoto kubwa kwa majeruhi hao ni utunzaji wa ngozi zao ili waepukane na wadudu jamii ya bakteria, ili wasiweze kupata magonjwa mengine kwa urahisi.

Kuhusu huduma za kitabibu, Dk. Ukio alisema zinajitosheleza kutokana na kuwa na vifaa tiba vya kutosha na dawa, isipokuwa kwa suala la chakula na lishe kutoka kwa ndugu wanaowauguza majeruhi hao.




Machinga wakiwa wameyashika mashuka kwa staili, wakati wasisubiri wateja kando ya Barabara ya Msimbazi, eneo la Kariakoo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Wizara ya Madini sasa yaja kivingine uchambuzi wa sera

**Na Idda Mushi, MOROGORO**

WIZARA ya Madini imeanza kuangalia mahitaji mapya ya kiujuzi katika wizara hiyo kutokana na mabadiliko yanayoendelea, kwa kuwawezesha watendaji wake kuchambua sera na nyaraka za serikali.

Eneo lingine linalotarajiwa kujengewa uwezo ni kwa wataalamu wa kukagua na kushauri uanzishwaji wa migodi na uthaminishaji wa madini ambako bado ni changamoto.

Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Prof. Amos Msanjila, alisema hayo mjini Morogoro wakati akizungumza na Nipashe, baada ya kukutana na watendaji wa wizara hiyo waliokuwa wakijadili namna ya kuchambua sera na nyaraka za serikali.

Prof. Msanjila alisema kukosekana kwa ujuzi unaoendana na hali halisi ya mabadiliko yaliyopo, kumeathiri kufikia malengo wanayojiweka, hivyo kuyafikia kwa ugumu.

"Ieleweke tu kwamba, kusoma digrii ya kwanza, ya pili na ya tatu ni mfumo ambao unamwandaa mtu ili aweze kujifunza akiwa maeneo yake ya kazi na kufanya kazi anazozifanya kwa wakati huo," alisema na kuongeza:

"Kwa hiyo hizi changamoto zilizopo za uchambuzi wa sera, uandishi, ni vitu ambavyo vinatakiwa kujifunza ukiwa kazini, ndio maana tumeliona hili na kuamua kutoa kozi fupi fupi kusaidia wafanyakazi wetu kuziba mapungufu haya, sio ya kielimu bali ya kiujuzi."

Alisema walishafanya mafunzo ya kufanya kazi za kiungozi, kuandika kiuongozi kwa watumishi wake na sasa wamelenga kuwaongezea ujuzi watumishi wa wizara hiyo namna ya kuchambua na kuandika sera, mikakati na maandiko yanayohitajika katika utekelezaji wa shughuli za wizara hiyo.

"Haya sio mapungufu, kwa jinsi maisha yanavyobadilika utahitaji ujuzi fulani, sio mapungufu, ni mahitaji mapya ya ujuzi, kama sasa nchi imebadilika uelekeo, tunataka kujenga uchumi wa viwanda, ni tofauti na tulivyokuwa tukichambua nyaraka tunasema hizi ni kwa ajili ya siasa ni kilimo, au kilimo kwanza."

"Ili wafanyakazi wetu waweze kuendana ni lazima tuwatafutie kozi fupi fupi kuendana na mazingira ya sasa...hata mimi nilipoteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu (wakati huo) nilikuwa ni profesa tayari, lakini nilikwenda kujifunza kuandika documents (maandiko) ya serikali," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti, Sera na Uchumi (REPOA), Dk. Donald Mmari, alisema kwa ufadhili wa ubalozi wa Norway, wameamua kusaidia wachambuzi wa sera wa wizara mbalimbali serikalini, ili wafikie matarajio ya maendeleo ya nchi kama ilivyo katika dira ya maendeleo ya nchi ya mwaka 2025.

Alisema nia ni kuhakikisha matokeo ya utafiti wa ndani na nje ya nchi yanafanikiwa kuwa na sera nzuri zinazokidhi maendeleo ya nchi na ushindani wa masoko ya kidunia kwa kuwa teknolojia imebadilika, kuna mabadiliko ya sheria ambayo yanahimiza madini na rasilimali nyingine zinawafaidisha Watanzania.

## Mkurugenzi apewa siku saba za majiko

**Na Halima Ikunji, TABORA**

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Manispaa Tabora, Bosco Ndunguru, amepewa siku saba kuhakikisha anagawa majiko banifu 100 yaliobakia kwa walengwa bila kubagua kwa kufuata taratibu zilizopo.

Agizo hilo lilitolewa na Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka huu, Mzee Mkonge Ali, alipokuwa akikagua mradi wa kutengeneza mkaa unaotokana na mabaki ya mazao na taka ngumu za mimea katika kiwanda cha Kuja na Kushoka kilichopo mjini hapa.

Mkongea alitoa agizo hilo kufuatia kubaini kuwapo kwa idadi ya majiko hayo ambayo yalipaswa kuwa yamekwishatolewa kwa walengwa ambao ni vikundi mbalimbali vya vijana, kinamama na makundi mengine yenye uhitaji.

Alieleza kuwa anashangazwa hadi sasa majiko hayo bado yapo kiwandani ambapo yalitengenezwa tangu Juni mwaka huu na kutakiwa kugawiwa kwa walengwa ili yawanufaishe katika shughuli zao.

## Wanufaika wa Tasaf wapewa mbinu miradi

**Na Elizabeth Zaya, SINGIDA**

MKURUGENZI wa Manispaa ya Singida, Bravo Lyapembile, amewashauri wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), kuanzisha miradi endelevu ambayo itawasaidia kuwa na uhakika wa maisha.

Lyapembile alitoa wito huo alipokuwa akizungumza na maofisa wa Tasaf kutoka makao makuu ambao wanafanya ziara za kukagua utekelezaji wa mpango huo mkoani Singida.

Alisema ipo miradi mbalimbali ambayo wameanzishiwa na mfuko huo, hivyo kazi yao ni kuhakikisha wanaisimamia na kuiendeleza kwa nguvu zote pamoja na kuendelea kujipanua kimawazo kwa kuanzisha miradi mingine ambayo itakuwa endelevu. "Hii miradi endelevu itasaidia kuwaweka katika hali ya juu zaidi, tunaamini wanufaika walio wengi wamewezeshwa na Tasaf, wanafuga, wanalima na wako kwenye vikundi ambavyo kwa kweli vimewasaidia kwa kiwango kikubwa," alisema na kuendelea:

Alisema pamoja na kupunguza umaskini kwa idadi kubwa ya watu katika Manispaa hiyo, pia imesaidia kuinua kiwango cha elimu na uboreshaji katika sekta ya afya.

"Mfano katika baadhi ya vijiji, Tasaf wamejenga zahanati na hata pia wamesaidia kutoa fedha za kununulia taulo za kujisitiri kwa wanafunzi wa kike, kwa hiyo kazi wanayofanya ni kubwa na wanahitaji kuungwa mkono," alisema.

# Mikoa mitano kinara kwa ukatili wa watoto yaanikwa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SERIKALI imetaja mikoa mitano kinara wa vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto nchini, huku takwimu zikionesha vitendo hivyo vimeongezeka.

Mikoa hiyo ni Tanga, Mbeya, Mwanza, Arusha na Tabora.

Hayo yalielezwa na Naibu Waziri Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Fautine Ndugulile, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Ulanga (CCM), Goodluck Mlinga.

Katika swali lake, Mlinga alisema kumekuwa na tatizo kubwa katika jamii la ubakaji wa watoto wadogo chini ya miaka mitano na vikongwe na kuhoji kama serikali imewahi kufanya utafiti wa kujua chanzo cha tatizo hili.

Akijibu, Dk.Ndugulile alikiri kuwapo ongezeko la vitendo vya ukatili hasa ubakaji wa watoto wadogo na vikongwe.

Alisema kwa mujibu wa taarifa za jeshi la polisi za mwaka 2018 za makosa ya ukatili wa kijinsia kwa watoto, hali ya vitendo vya ukatili kwa watoto nchini imeongezeka kutoka matukio 13,457 ya mwaka 2017, hadi matukio 14,419 ya mwaka 2018.

"Ongezeko la makosa ni 1,034 sawa na asilimia 7.7 na mikoa inayoongoza ni Tanga(1,039), Mbeya (1,001), Mwanza(809), Arusha (792) na Tabora (618)," alisema.

Alitaja makosa yanayoongoza ni ubakaji (5,557), mimba (2,692), kulawiti (1,159), shambulio (965) na kujeruhi (705).

Aidha, alisema mwaka 2009 serikali kwa kushirikiana na UNICEF ilifanya utafiti kuhusu hali ya ukatili dhidi ya watoto, utafiti huo unaonyesha kuwa asilimia 60 ya vitendo vya ukatili dhidi ya watoto hufanyika nyumbani na vinafanywa na watu wa karibu wa familia.

Pia alisema asilimia 40 ya vitendo hivyo hufanyika shuleni.

Alibainisha kuwa sababu kubwa ya vyanzo vikubwa vya ukatili ni imani potofu, elimu au hali duni ya umaskini, kutetereka kwa misingi ya malezi ndani ya familia, mila na desturi potofu utandawazi.

"Aidha, hakuna utafiti uliofanyika kuhusu ubakaji wa vikongwe ingawaje vyanzo vya ukatili vinashabihiana na ule wa watoto," alisema.

Alisema serikali itaendelea kutoa elimu na kuhamasisha jamii kutambua jukumu lao la malezi na matunzo ya watoto na wazee.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Boniphace Simbachawene (aliyesimama), akiteta jambo na Mbunge wa Jimbo la Bumbuli ambaye ni waziri wa zamani wa ofisi hiyo, Januari Makamba (wa pili kushoto), walipokutana katika kikao cha kwanza cha Mkutano wa 16 wa Bunge, jijini Dodoma juzi. Kulia ni Mbunge wa Kibaha Vijijini, Hamoud Jumaa. **PICHA: MAELEZO**

# Siku saba kufutiwa kesi kampuni za tumbaku

WIZARA ya Kilimo na Wizara ya Viwanda na Biashara zimetoa siku saba kuondolewa mahakamani kesi zote ambazo zinazikabili kampuni nne za ununuzi wa tumbaku zilizopigwa faini ya zaidi ya Sh. bilioni 11 ili ziendelee na biashara ya kununua zao hilo.

Kutokana na kesi hizo, zimesababisha tumbaku kiasi cha kilo milioni 12 kuwa mikononi mwa wakulima hadi sasa bila kununuliwa

Hayo yalibainishwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Urambo (CCM), Margaret Sitta.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema hadi jana kuna tani 12,000 za tumbaku ambazo hazijanunuliwa, wakati msimu wa kilimo umeshafika na baadhi ya kampuni hazijatoa makisio.

"Je, serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kwamba tumbaku yote inanunuliwa na makisio yanapatikana? Kuna taarifa kwamba kampuni ya Tanzania Leaf Tobacco Company Limited(TLTC), ambayo ilinunua tumbaku tani kilogramu milioni 16 ilikuwa na viwanda vya tumbaku na maghala na wakati huo ilikuwa na wafanyakazi 300 ambao sasa kampuni hii ikijitoa wafanyakazi wanapoteza kazi?" alihoji.

Alihoji serikali inachukua hatua gani kuhakikisha hiyo kampuni pamoja na kuondoka itakuwaje maana ilikuwa mnunuzi mkubwa.

Akijibu, Bashe alisema kesi hizo ziondoke mahakamani ndani ya siku saba ili wafanyabiashara hao kuendelea kufanya biashara kwa kuwa ni azma ya serikali kuhakikisha biashara inafanyika katika mazingira sahihi. Alikiri kuna tumbaku mikononi mwa wakulima kiasi cha kilo milioni 12, lakini serikali ilichukua hatua mbalimbali.

"Kampuni ambazo zilikuwa zikinunua tumbaku zimekuwa zikipitia changamoto mbalimbali, changamoto nyingine zinasababishwa na uzembe wa baadhi ya watumishi wa serikali, na sisi wizara tumechukua hatua, jana tumekutana na kampuni nne zote za tumbaku ambazo zinanunua tumbaku nchini ambazo zimeonyesha nia kutonunua tumbaku ambazo zipo kwa wakulima," alisema.

Alisema Septemba 12 baraza la Tumbaku litakutana na kampuni hizo ili tumbaku hizo ziweze kuondoka mikononi mwa wakulima.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alisema serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuwasaidia wakulima nchini hususan wakulima wa tumbaku ili zao hilo la biashara liwe kuwasaidia wakulima na Taifa kwa ujumla kwa kuingiza fedha za kigeni.

Alihoji wanunuzi wangapi wamepatikana hadi sasa ili wakulima walime tumbaku nyingi kwa bei ya ushindani ili kumnufaisha mkulima na Taifa kwa ujumla. Bashe alisema makisio ya mahitaji ya mbolea kwa Mkoa wa Tabora ni jumla ya tani 9,092 sawa na asilimia 42.13 ya mahitaji ya mbolea za zao hilo nchini ya tani 21,582, huku Halmashauri ya Urambo ikihitaji jumla ya tani 2,468.96.

Alisema hadi kufikia Agosti 15, 2019 upatikanaji wa mbolea katika Halmashauri ya Urambo kwa ajili ya vitalu ni mifuko 1014.64 sawa na upatikanaji wa asilimia 100 na usambazaji unatarajiwa kukamilika Septemba 10,2019.

"Wanunuzi wakubwa wa tumbaku hapa nchini ni Alliance One Tobacco Tanzania Limited (AOTTL), Premium Active Tanzania Limited (PATL), Japanese Tobacco International Leaf Services (JTILS) na TLTC, Magefa Growers Limited na Grand Tobacco Limited," alisema.

Aidha alisema serikali inaendelea kufanya majadiliano ya mwisho na kampuni kubwa ya British American Tobacco (BAT) ili kampuni hiyo ianze kununua tumbaku kwa wakulima katika msimu wa kilimo 2019/20.

"Vilevile, serikali imefanya mazungumzi na nchi ya China ili iweze kununua tumbaku kutoka Tanzania ambapo nchi hiyo imeanisha aina za mbegu za tumbaku ambazo wanataka zizalishwe nchini ili kukidhi ladha ya tumbaku wanayohitaji," alisema.

## Sababu wamiliki wa meli kutokata leseni

BUNGE limeelezwa kuwa kufuatia marekebisho ya Kanuni za Uvuvi wa Bahari Kuu za mwaka 2009, wamiliki wa meli zinazofanya uvuvi huo wamesita kukata leseni kutokana na kutokukubaliana na masharti mapya.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Dimani, Juma Ali Juma (CCM), ambaye alisema serikali imezuia kutoa leseni kutokana na ubadhirifu uliokuwa ukifanywa na taasisi za utoaji leseni.

Alisema uzuiaji huo umepoteza mapato mengi ya serikali na kuifanya taasisi ya uvuvi wa Bahari Kuu kushindwa kufanya kazi zake inavyotakiwa.

"Je, ni lini serikali itamaliza mchakato wa kujipanga ili kuanza kutoa leseni?" Je, taasisi ya uvuvi wa bahari kuu imesaidiwa kwa kiasi gani ili iweze kujiendesha kwa kipindi hicho ambacho haikupata mgawo unaotokana na leseni?" alihoji.

Akijibu, Ulega alisema serikali ilisimamisha utoaji wa leseni za uvuvi wa Bahari kuu kuanzia Agosti 8, 2016 mpaka desemba mwaka 2016 ili kuruhusu marekebisho ya kanuni za uvuvi wa Bahari kuu za mwaka 2009.

"Marekebisho haya ni pamoja na maboresha ya masharti ya leseni yaliyopo katika kifungu cha 10 ya Kanuni za mwaka 2009 za kanuni za kusimamia uvuvi wa Bahari Kuu kwa lengo la kuongeza mapato ya serikali," alisema.

Alisema kufuatia marekebisho hayo wamiliki wa meli zinazovua katika Bahari kuu wamesita kukata leseni kutokana na kutokukubaliana na masharti mapya yaliyoongezwa katika kanuni mpya za mwaka 2016.

"Kulingana na Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu ya mwaka 1998 na marekebisho yake ya mwaka 2017, Mamlaka hupatiwa asilimia 50 ya mapato yote yanayokusanywa kwa mwaka," alisema.

Alifafanua hatua hiyo ni kutokana na bakaa ya mgawo huo mamlaka imeendelea kujiendesha na kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa sheria.

"Aidha, serikali ya SMT na SMZ zipo kwenye hatua za mwisho kutatua changamoto ya meli za uvuvi kutokukata leseni na kuiwezesha Mamlaka kujiendesha," alisema.



# Serikali yashauriwa mikataba kimataifa

**Na Zanura Mollel, LONGIDO**

SERIKALI imeshauriwa kulinda, kutunza na kuheshimu haki za binadamu kama ilivyoridhia na kutia saini mikataba ya kimataifa na ya kikanda na kuridhiwa kwenye katiba ya nchi.

Rai hiyo ilitolewa na Mkufunzi wa Taifa wa Dhana ya Uwajibikaji kwa Jamii (SAM), Nemence Iriya, wakati wa mafunzo kwa wadau na wakuu wa idara wilayani Longido.

Alisema kwa mujibu wa Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, imeainisha haki hizo na wajibu wa serikali kwa wananchi na mikataba, matamko, maazimio mbalimbali ya kikanda na kimataifa waliyotia saini. Iriya alisema mafunzo hayo yalitolewa na shirika lisilo la kiserikali la Ansaf kwa lengo la kuikumbusha serikali wajibu wake kwa wananchi kwa mujibu wa mikataba, maazimio na makubaliano ya kikanda na kimataifa.

Hata hivyo, alisema wananchi si wanufaika wa huduma za umma na pia hawana kauli ya umiliki halali wa haki za binadamu kutokana na kutokuwa na uwezo wa kusimamia haki hizo kwa mujibu wa sheria.

Alisema wananchi wana haki ya kunufaika na rasilimali zilizopo nchini kwa kuwa ndio waliyoiweka serikali madarakani, hivyo rasilimali hizo zitumike vizuri kuwahudumia wananchi.

Aliongeza kuwa Tanzania ni moja ya nchi 150, duniani zilizotia saini mikataba ya haki za binadamu, ya haki za kiuchumi, kijamii na kiutamaduni (ICESCR).

Kwa mujibu wa mkufunzi huyo, mkataba wa Afrika (Banjul) uliotiwa saini mwaka 1981, unazungumzia utu na haki za binadamu, huku ukizitaka nchi wanachama zilizotoa saini mkataba huo kuhakikisha taarifa zinazozalishwa na kutunzwa ziwekwe wazi kwa mtu yeyote anayezihitaji na sio kwa matumizi ya taasisi hizo peke yake.

Aidha, alisema ibara ya 16 ya mkataba huo, inaelezea haki ya upatikanaji wa huduma ya afya wakati ibara ya 17 inazungumzia haki ya kupata elimu na ibara ya 22 inasisitiza haki ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni kwa kulinda dola za mataifa yote yenye kutekeleza maendeleo ndani ya jamii.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema suala la jamii kupata taarifa ni haki yao na hata makubaliano ya tume ya haki za binadamu kupitia azimio la misingi ya uhuru wa kujieleza wa Afrika wa mwaka 2002, inazungumzia upatikanaji wa haki ya kupata taarifa kwa mtu yeyote.

"Hata Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, ibara ya 18, inaelezea uhuru wa mawazo na upatikanaji wa taarifa na ibara ya 14 inazungumzia haki ya kuishi," alisema Iriya.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya ufundi stadi ya Healsun katika kijiji cha Muriet, jijini Arusha, wakionyesha elimu ya ufundi kwa vitendo kwa wazazi (hawapo pichani), waliohudhuria katika mahafali ya nne ya darasa la saba ya shule hiyo, juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Hospitali yanunua CT-Scan ya kisasa

**Na Cynthia Mwilolezi, MBULU**

HOSPITALI ya Rufani ya Kilutheri ya Haydom wilayani Mbulu mkoani Manyara, inayohudumia zaidi ya wagonjwa 120,000 kwa mwaka, imenunua mashine mpya ya kisasa ya uchunguzi ya mionzi (CT-Scan) ambayo kwa miaka miwili hakukuwa na huduma hiyo baada ya iliyokuwapo kuharibika.

Hospitali hiyo kwa mwaka huhudumia wastani wa wagonjwa 105,296 wa nje na 14,020 wa ndani wa mikoa ya Manyara, Arusha, Tabora, Singida, Dodoma na Simiyu.

Mkurugenzi wa Tiba wa Hospitali hiyo, Dk. Emmanuel Nuwass, akizungumza na waandishi wa habari juzi, alisema Sh. milioni 800 zimetumika kuinunua mashine hiyo nchini Ujerumani na kuisafirisha hadi hospitalini hapo.

Dk. Nuwass alisema awali mashine iliyokuwapo iliharibika miaka miwili iliyopita, hivyo kusababisha wagonjwa wengi kukosa huduma ya vipimo hivyo.

Alisema kutokana na ukosefu wa mashine hiyo, iliwabidi watu wa eneo hilo kufuata vipimo takribani kilomita 400 hadi 600 kwenye hospitali za kanda za KCMC Kilimanjaro na Bugando Mwanza.

Alisema mashine hiyo ya kisasa itasaidia wagonjwa wengi hasa wasio na kipato kupata vipimo kwenye eneo la karibu na wanatarajia itazinduliwa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, hivi karibuni.

Catherine Faustine, mkazi wa eneo hilo, alisema wananchi wengi wameshindwa kupata huduma hiyo kutokana na umbali mrefu wa kufuata katika hospitali zingine kubwa.

"Kuna baadhi ya watu walifariki (dunia) kwa sababu hawana fedha za kwenda kupimwa katika hospitali za mbali kama KCMC Moshi au Muhimbili, Dar es Salaam. Tunashukuru kwa kupata mashine hii," alisema.

Mtaalamu wa Mionzi wa Hospitali hiyo, Paulo Fissoo, alisema mashine hiyo ina uwezo mkubwa zaidi tofauti na ile ya awali iliyoharibika. Hospitali ya Haydom inayomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mbulu, ilianzishwa na wamisionari wa Norway mwaka 1955 ikiwa na vitanda 50 na sasa ina vitanda 420.

Wagonjwa wanaopata huduma hospitali hiyo wanatoka wilaya za Mbulu, Hanang na Babati mkoani Manyara, Karatu mkoani Arusha, Igunga mkoani Tabora, Iramba na Mkalama mkoani Singida, Kondoa mkoani Dodoma na Meatu mkoani Simiyu.

# Bil. 4.1/- kutumika kujenga barabara

**Na Allan Isack, ARUASHA**

HALMASHAURI ya Jiji la Arusha imekabidhi mradi wa Sh. bilioni 4.1 wa ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 4.3 kwa kampuni ya ujenzi ya Sinohydro Corporation Ltd , unaotarajiwa kuanza Septemba 11, mwaka huu.

Barabara hiyo ni nyongeza ya mkataba na itajengwa kutoka Kisongo hadi Bypass na itakuwa na urefu wa kilometa 3.44 kupitia fedha za mradi wa Miji Mkakati ya Tanzania (TSCP ), inayoratibiwa na Benki ya Dunia chini ya Ofisi ya Rais (Tamisemi).

Akizungumza baada ya kuukabidhi mradi kwa kampuni hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Sifael Kulanga ambaye ni mwanasheria wa jiji hilo, alisema mradi huo ni wa nyongeza na utatekelewa ndani ya miezi minne hadi Januari 11, mwakani.

Alisema mradi huo utasaida kuondoa msongamano wa magari katikati ya Jiji la Arusha na una manufaa ya moja kwa moja kwa wananchi na utasaidia usalama kwenye uwanja mdogo wa ndege badala ya kukata katikati ya uwanja na barabara hiyo itasaidia kuchepuka pembezoni mwa uwanja.

"Barabara hii ina umuhimu mkubwa sana katika uwanja wetu wa ndege na maeneo ya shule ya sekondari na itafungua fursa kwa wanaowahi katikati ya jiji kutoka stendi kubwa ya mabasi ya mkoani inayotarajiwa kujengwa Olasit."

Mhandisi wa Barabara wa Kampuni ya Snohydro, Lang Yang Shang, alisema wataifanya kazi hiyo ndani ya muda uliopangwa mkataba na kwa viwango vilivyowekwa na kwa ubora.

Awali akitoa taarifa ya mradi huo, Mhandisi Augusti Mbuya, alisema barabara hiyo, ni muunganiko wa bypass na itarahisisha mchepuko na kusaidia usalama, na aliishukuru serikali ya awamu ya tano kwa kutenga fedha hizo.

Alisema mradi huo utaanza Septemba 11, mwaka huu na jana ilikuwa kuweka makabidhiano kwa Jiji kumkabidhi rasmi mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo.

Mstahiki Meya wa Jiji la Arusha, Kalist Lazaro, alisema barabara hiyo ni sehemu ya mkataba uliotiwa saini wiki iliyopita na utakuwa kielelezo cha kueleza jinsi utekelezaji wa ilani ya uchaguzi kwa wananchi mwaka ujao jinsi serikali ilivyotekeleza miradi yake.

**"Barabara hii ina umuhimu mkubwa sana katika uwanja wetu wa ndege na maeneo ya shule ya sekondari na itafungua fursa kwa wanaowahi katikati ya jiji kutoka stendi kubwa ya mabasi ya mkoani inayotarajiwa kujengwa Olasit."**

# Adaiwa kumchoma kisu mzazi mwenziwe

**Na Mwandishi Wetu, ROMBO**

UKATILI ni uhalifu kama uhalifu mwingine. Ndivyo unavyoweza kusema baada ya mkazi wa Kijiji cha Mrere, Rombo mkoani Kilimanjaro, Innocent Kimario, kudaiwa kujeruhiwa kwa kuchomwa na kitu chenye ncha kali mbavuni na mwanamke aliyezaa naye mtoto mmoja.

Kimario ambaye anajishughulisha na kazi za upasuaji wa mbao, anadaiwa kujeruhiwa na mwanamke aitwaye Gloria Joseph.

Habari zilizopatikana jana na baadaye kuthibitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Hamisi Issah, zilieleza kuwa chanzo cha ugomvi huo uliosababisha Kimario kuchomwa na kitu chenye ncha kali mbavuni ni kucheleweesha kutoa fedha za matunzo ya mtoto.

"Inasemekana kwamba chanzo cha tukio hilo ni mwanamke huyo kuhitaji matunzo ya mtoto, lakini alipomwomba na kuchelewa kumpatia mahitaji hayo, alimvizia na kumchoma na kitu chenye ncha kali," alisema Kamanda Issah.

Kwa sasa mwanamume huyo anapatiwa matibabu katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Rombo (Huruma) ambayo inamilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo la Moshi.

Pamoja na taarifa hiyo ya polisi, mmoja wa wasaidizi wa kisheria katika Wilaya ya Rombo, aliyeomba jina lake lisitajwe, alisema wanawake wengi hujikuta wanakabiliwa na majukumu mengi ya kifamilia, pasipo usaidizi kutoka kwa waume zao.

Alisema mwanamke asipopata ushirikiano wa mmewe katika majukumu ya nyumbani, huchoka, huwa na hasira, husongwa na mawazo na hukosa nafasi ya kushiriki katika masuala ya kijamii na kwamba ni wajibu kwa kila mwanaume kumsaidia mke wake majukumu ya nyumbani.

## Wachanga mil. 267/ - ujenzi kituo cha afya

**Na Godfrey Mushi, HAI**

WADAU wa maendeleo wa Wilaya ya Hai, ambao ni vyama vya ushirika, wamejitutumua kuchangia Sh. milioni 267.9 za ujenzi wa kituo cha afya cha heshima kinachotarajiwa kujengwa eneo la Weruweru.

Kituo hicho cha afya ni miongoni mwa miradi miwili ya kipaumbele itakayojengwa ikiwamo pia mradi mkubwa wa kimkakati wa ujenzi wa soko la kimataifa la nafaka ambalo uwekezaji wake utagharimu kiasi cha Sh. bilioni 11 katika eneo la Kwa Sadala.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa mradi huo wa kituo cha afya cha heshima cha Rais John Magufuli, mbele ya Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kilimanjaro, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo, alisema wadau hao wameamua kwa hiari yao kuiunga mkono serikali.

"Kama ilivyo desturi ya waungwana wengine ambao ni wadau wa maendeleo katika nyanja mbalimbali, vyama vya ushirika hapa kwetu viliamua kuunga mkono juhudi za serikali katika uboreshaji wa huduma za afya kwa kuchangia Sh. 267,952,415 ili kuwezesha utekelezaji wa mradi huu," alisema.

Kituo hicho cha kisasa kitakachojengwa Weruweru, kitakuwa na watoa huduma ya dharura na upasuaji, maabara, wodi ya wazazi, mochwari, jengo la kufulia nguo, nyumba ya mtumishi na miundombinu mingine.

Kwa kawaida kituo cha afya hujengwa kwa gharama ya Sh. milioni 600 kutokana na kuongeza kwa gharama ya majengo mengine ikiwamo jengo la wagonjwa wa nje (OPD).

Pamoja na mambo mengine, Sintoo alisema serikali kuu imeipelekea zaidi ya Sh. 1,729,894,651 kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika Wilaya ya Hai, hivyo kumaliza tatizo la upungufu wa upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.

Akipokea taarifa hiyo Katibu wa CCM, mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, aliipongeza halmashauri hiyo kwa kusimamia vyema matumizi ya fedha za serikali na kuhakikisha miradi inayojengwa inakuwa na ubora unaotakiwa na kutekelezwa kwa muda mwafaka.



Mwenyekiti wa chama cha wachimbaji madini Mkoa wa Manyara (Marema), Justin Nyari (katikati), akizungumza na wadau wa madini wa wilayani Simanjiro juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Wasusia miradi kudai malipo yao

**Na Mwandishi Wetu, SAME**

WAZABUNI wanaotoa huduma ya vifaa vya ujenzi na mafundi jamii wanaofanya kazi za ujenzi katika Shule ya Sekondari Makanya, Same mkoani Kilimanjaro, wanadaiwa 'kususa' wakati mwingine kuendelea na kazi hiyo wakishinikiza kwanza malipo yao.

Mkuu wa Shule hiyo, Damas Hosteri, alitoa taarifa hiyo kwa Mjumbe wa Halmashauri ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (NEC) Mkoa wa Kilimanjaro, Joseph Thadayo, aliyetembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa mabweni mawili ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Akitoa taarifa hiyo, Hosteri alisema changamoto kubwa inayosababisha malalamiko hayo ni mfumo wa malipo FFARS.

Kitaalamu mfumo huo wa malipo unaitwa "Facility Financial Accounting Reporting System (FFARS) ambao unatumika katika vituo vya kutolea huduma kwenye zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya na shule.

"Huo mfumo wa malipo wa FFARS, ulitupa changamoto sana kwa sababu kwa muda mrefu, wazabuni na hata mafundi hawa (force account) walishindwa kuendelea na kazi kwa kudai malipo yao kwa muda mrefu na baadhi ya wazabuni wa vifaa vya ujenzi, walikataa kuwapatia vifaa kwa madai ya kucheleweshewa malipo," alisema.

Kwa mujibu wa Hosteri, serikali ilitoa Sh. milioni 190 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili ya kulaza wanafunzi wa kidato cha tano na sita katika shule hiyo ya kitaifa.

Pia fedha hizo zitatumika kujenga vyumba viwili vya madarasa katika shule hiyo ambayo yatagharimu Sh. milioni 40 kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Akikagua mradi huo, Tadayo alisema CCM imeridhishwa na utekelezaji wa ujenzi wa madarasa hayo na mabweni hayo, kwani yamejengwa kwa ubora unaotakiwa na matumizi sahihi ya fedha za serikali.

Alisema hatua hiyo ni utekelezaji mzuri wa ilani ya uchaguzi, miradi imetekelezwa vizuri na kazi inaridhisha ujenzi umefanywa kwa kiwango cha juu ili kuwawezesha watoto wote kupata elimu.

Alisema ujenzi wa bweni utapunguza tatizo la mimba kwa wanafunzi wa kike na litaongeza fursa kwa wanafunzi kupata muda mrefu wa kujisomea na kutoa wito kwa wananchi kuchangia mchango wao wa nguvu kazi ili kuweza kukamilisha ujenzi wa mabweni hayo.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alisema serikali italifanyia kazi tatizo la vyoo vya shule hiyo kujaa maji machafu na kwamba hatua hiyo itakwenda sambamba na ujenzi wa choo kipya katika shule hiyo.

# ama

ALHAMISI SEPTEMBA 5, 2019

AFYA NA MAZINGIRA



**Kashfa ngono watoto ilivyomtupia mzigo wa kuhamia jela miaka sita**

Ukurasa 18



Ukurasa 17

Sakata nyama choma latinga Mahakama Kuu



Ukurasa 14

**Bosi Mkuu UN: Ahadi za Ebola 'kiduchu'**



# Kinamama wa kisasa na shida wanazowapa watoto kunyonya

Ukurasa 14

# Bosi Mkuu UN: Ahadi za Ebola 'kiduchu'

**KINSHASA,** DRC

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Mataifa, António Guterres, amelalamika kwamba kucheleweshwa zaidi katika kupokea fedha za wafadhili, kunamaanisha watashindwa katika vita dhidi ya Ebola.

Akizumguza mjini Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia Congo (DRC) Guetress anasema Umoja wa Mataifa umepokea asilimia 15 pekee ya kile kinachohitajika katika mapambano ya kukabili mlipuko wa Ebola mwaka huu.

Ni kauli aliyotoa kwa wanahabari, kabla ya kukutana na Rais, Felix Tshisekedi. Baadaye alipata fursa ya kutembelea katika eneo la Beni, ambako kunatajwa kuwa kiini cha mlipuko, alikokagua zahanati zinazowatibu walioambukizwa ugonjwa huo

Katibu Mkuu kupitia fursa hiyo, aliwahimiza wafadhili kuheshimu ahadi walizotoa.

Pia Jumatatu wiki hii, waziri wa zamani wa afya nchini hapa, Oly Ilunga, alihojiwa na polisi kuhusu namna alivyosimamia fedha za kupambana na mlipuko wa Ebola.

Ilunga alijiuzulu wadhifa huo, mwezi Julai baada ya kusimamia mapambano ya Ebola kwa takribani mwaka mmoja. Inadaiwa, kuwapo ufujaji wa fedha hizo katika kijiji cha kimoja.



Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, António Guterres **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

# Kinamama wa kisasa na shida wanazowapa watoto kunyonya

## • Vita kusaka urembo 'ni shida'



Watoto wakinyonya maziwa. **PICHA: MTANDAO**

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

***MWEZI uliopita kulikuwapo mfululizo wa makala zinazohusiana na Siku ya Unyoyeshaji Duniani. Katika makala ifuatayo, endelea kupata undani wa tabia ya kinamama kukwepa kunyoyesha na namna inavyoathiri afya ya watoto, pia msimamo wa serikali ulipo. Endelea.***

KUANZIA tarehe Mosi ya mwezi Agosti katika mfululizo wa siku saba, ni maadhimisho ya Siku ya Unyonyeshaji Maziwa ya Mama, ambayo katika sayansi ya afya yanajulikana kuwa muhimu zaidi.

Pamoja na nafasi ya lishe hiyo, bado katika sura ya pili kuna changamoto lukuki inayoekezwa kutokana na kushuka kwa hali ya unyonyeshaji duniani, ikiwamo nchini Tanzania.

> **"Mimi niliacha. Niliona naharibu matiti yatalala wakati nina uwezo wa kumpa mwanangu maziwa mbadala na akakua.**

Takwimu za mwaka 2015/2016 na mwaka jana zinazoonyesha asilimia 43 tu ya watoto wanyonyeshwa hadi kufikia umri wa miaka miwili nchini.

Shirika la Watoto Duniani(UNICEF), zinaonyesha kwamba takribani watoto milioni 7.6 duniani hawanyonyeshwi kila mwaka.

Matokeo ya utafiti huo yanaonyesha idadi ya watoto wasionyonyeshwa na mama zao ni kubwa zaidi katika mataifa yaliyoendelea, ikilinganishwa na yale maskini.

Inaelezwa kwamba, asilimia nne ya watoto kwenye nchi maskini hawanyonyeshwi kabisa maziwa ya mama, wakati katika nchi zilizoendelea kundi hilo linafikisha asilimia 22.

Miongoni mwa sababu zinazotajwa, ni hofu ya baadhi ya wanawake kuharibu maumbile ya matiti yao kupitia dhana 'kuacha matiti yasimame' na wapo wengine wanashindwa kufanya, hivyo kutokana na kuelemewa na majukumu ya kimaisha

### KAULI YA WAZIRI

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, anazungumzia hilo akiunga mkono hoja ya watafiti, kwamba kuna kundi la wanawake hawakunyonyesha watoto kwa madai ya matiti yao kuharibika na wanaishia kuwapa watoto vyakula mbadala.

Ummy analalamika kwamba, ni jambo linaloathiri makuzi ya watoto na ulinzi wa maumbile ya watoto unakaribisha hatari ya saratani.

"Kuna watu wanaogopa wanadai kuwa wanachakaa hasa visichana vya siku hizi, dhana hii si sahihi, matiti yakiharibika kuna 'blazia' sasa kipi bora kuharibika au kupata saratani, kuna watu wananyonyesha watoto 10 lakini matiti ni saa sita,"analalamika, huku akikumbusha hatari mtu anapoyonyesha anajiepusha na saratani, pia mimba za muda mfupi baada ya kujifungua.

Anaongeza: "Hali ya unyonyeshaji wa maziwa ya mama nchini kwetu imepungua kwa asilimia moja. 'Visichana' vya sasa hivi asilimia moja havitaki kunyonyesha, kwa maana hiyo watoto 20,000 wanaozaliwa hawanyonyeshwi."

Pia, anasistiza umuhimu wa watoto kunyonyeshwa kwa kipindi cha miezi sita ya kwanza bila ya kupewa kingine cha ziada, kwani wapo wazazi wanaokiuka kwa kuwapa maji na uji.

"Watoto wanaonyonyeshwa bila kupewa chochote ni asilimia 58. Jitihada hazijafanikiwa, lazima tuwasaidie. Watalaamu wanasema miezi sita apewe maziwa ya mama tu. Sasa hawa wamama wanatingwa na majukumu wakiwaachia kina bibi majumbani, unakuta amepewa maji, uji kitu ambacho hakitakiwi," anasema.

Waziri Ummy anasema, idadi ya wanawake wanaonyonyesha watoto ipasavyo imepungua, hivyo kuna haja kutolewa elimu ya jamii kuwawezesha watoto kupata maziwa ya mama.

### ATOA AGIZO

Kupitia tamko hilo, waziri anaziagiza ofisi binafsi na za umma nchini, zitenge vyumba maalum vya kunyonyeshea watoto ana anawataka watumishi wanaonyimwa na waajiri muda huo wa kisheria saa mbili kunyonyesha, watoe taarifa ili hatua zichukuliwe, kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini ya mwaka 2004.

"Chumba hicho kitasaidia. Kuna saa maziwa yanatoka mengi, anaweza kwenda kwenye kile chumba akakamua maziwa akaweka katika friji na wataalamu wanasema yanakaa saa sita hadi nane," anaeleza.

Ummya anasisitiza: "Hii itasaidia kinamama makazini kupata saa mbili kutoka kwa mwajiri kwa ajili ya kunyonyesha."

### MWAKILISHI UNICEF

Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Watoto nchini (Unicef), James Gitau, anasema Shirika la Afya

AFYA

# Kinamama wa kisasa na shida wanazowapa watoto kunyonya

Duniani(WHO), linasisitiza mtoto anapaswa kunyonyeshwa hasa miezi sita ya mwanzo kabla ya kupatiwa vyakula vingine na itasaidia kuepuka magonjwa.

Anataja changamoto iliyopo ni kwamba, katika uwiano wa kasi ya unyonyeshaji, kwamba kuna mtoto mmoja kati ya wawili hawanyonyeshwi ndani ya saa moja baada ya kuzaliwa.

"Watoto wanne kati ya 10 hawanyonyeshwi miezi yao sita baada ya kuzaliwa. Pia, watoto sita kati ya 10 hawanyonyeshwi hadi miaka miwili au zaidi,"anasema

Gitau, kwamba ili kuboresha unyonyeshaji, kunahitajika jitihada zinazoshirikisha wanaume, familia na maeneo ya kazi.

### WANYONYESHAJI

Regina William, anaeleza uzoefu wake kwamba hakupenda kumnyonyesha mwanawe na alitekeleza hilo kipindi cha baada ya mtoto kutimiza umri miezi mitatu, akahamia katika kumpatia vyakula mbadala kama maziwa ya kopo na uji mwepesi.

"Mimi niliacha. Niliona naharibu matiti yatalala wakati nina uwezo wa kumpa mwanangu maziwa mbadala na akakua," anasema.

Mzazi mwingine, Jamila Omari, ana simulizi kwamba alikuwa anabanwa sana na kazi zake hata akalazimika kumuanzishia mtoto maziwa ya kopo na alipofikisha miezi minne alimuachisha kunyonya.

Anasema alipoifikia hatua hiyo ya kumuachisha mwanawe katika umri huo alihakikisha anampatia maziwa hayo na mpaka sasa mtoto huyo amefikisha umri wa miaka mitatu.

Sakina Abdula ni mkazi wa jijini Dodoma, mwenye mtazamo tofauti na kinamama watangulizi wake, akisema binfasi amewanyonyesha ipasavyo kwa kipindi cha zaidi ya miaka miwili na hakuwahi kufikiria kutowanyonyesha kwa hofu ya kuharibu maumbile.

"Mimi nashangaa wanaacha kunyonyesha eti wanaharibu matiti... wanawanyima watoto haki ya msingi ya kupata maziwa ya mama. Wengine tu ni wavivu kunyonyesha kwa uhalisia wanaleta visingizio ambavyo havina mashiko," anasema.

### VIFO TISHIO

Ofisa Lishe Mwandamizi kutoka Taasisi ya Chakula na Lishe(TFNC), Neema Joshua, anasema tafiti zinaonyesha taratibu zisizofaa za unyonyeshaji zinaathiri maendeleo ya uhai wa watoto na inachangia kwa kiasi kikubwa.

Anasema vifo vya watoto vichanga vipo juu sana nchini ambapo vifo 25 hutokea kwa kila vichanga 1000 waliozaliwa hai , huku vifo vya watoto chini ya mwaka mmoja vikiwa ni vifo 43 kwa kila watoto 1000 waliozaliwa hai.

Vilevile, anasema katika kundi la watoto wenye umri chini ya miaka mitano, kuna vifo 67 kwa kila watoto 1000 wanaozaliwa hai.

Anataja njia mojawapo ya kuepuka kasoro hiyo ni kuboresha huduma za afya, kwa kuwasaidia kinamama wawanyonyeshe ipasavyo watoto wao.

"Kama tukiweza kufanya uboreshaji huo tunaweza kuzuia vifo zaidi ya 820,000 kwa mwaka vya watoto, takriban nusu ya magonjwa ya kuhara na theluthi moja ya magonjwa ya njia ya hewa yanaweza kuzuilika kwa kunyonyesha watoto maziwa ya mama," anasema.

Anaeleza kuwa unyonyeshaji wa muda mrefu (miaka miwili au zaidi) unasaidia kupunguza unene uliozidi na magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari kwa watoto.



Watoto wakinyonya maziwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



> "Sababu kubwa ikiwa ni ulishaji usiokuwa sahihi ambapo sababu zinazochangia hilo tatizo ni mama kuwa na majukumu mengi yanayosababisha kukosa muda wa kumtunza mtoto.

### UNYONYESHAJI ULIVYO

Mratibu wa Lishe ya Mama na Mtoto kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Sikitu Simon, anasema takwimu za utafiti wa hali ya lishe nchini mwaka jana, 2018 inaonyesha watoto wanaoanzishwa maziwa ya mama kwa wakati sahihi ndani ya saa moja mara tu baada ya kuzaliwa ni asilimia 53, ikilinganisha na asilimia 51 wa mwaka 2015/2016.

"Watoto walionyonyeshwa maziwa pekee bila kupewa maji au vyakula vingine kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo baada ya kuzaliwa ni asilimia 58 ukilinganisha na asilimia 59 ya mwaka 2015/2016,"anasema.

Hata hivyo, anasema takwimu hizo zinaonyesha asilimia 31 ya watoto chini ya miaka mitano wamedumaa ukilinganisha na asilimia 34 ya mwaka 2015/2016.

"Sababu kubwa ikiwa ni ulishaji usiokuwa sahihi ambapo sababu zinazochangia hilo tatizo ni mama kuwa na majukumu mengi yanayosababisha kukosa muda wa kumtunza mtoto,"anasema

Anabainisha watoto walionyonyeshwa maziwa ya mama pekee kwa miezi sita ya mwanzo, hupata Madini Chuma ya kutosha na hukingwa na upungufu wa wekundu wa damu kwa kipindi chote cha miezi sita.

### UMUHIMU WAKE

Maziwa ya mwanzo baada ya mama kujifungua huwa ni mazito na yana rangi ya njano, yanayotoka siku chache baada ya mama kujifungua.

Maziwa hayo ni muhimu sana kwa lishe ya mtoto na yana kinga nyingi za mwili kumlinda mtoto na maradhi mbalimbali ya kibinadamu.

Hayo ni maziwa ya mwanzo yenye chembe nyeupe za damu ya mama, zinazotengeneza kinga mwili kwa ajili ya kumlinda mtoto dhidi ya maradhi.

Anafafanua kuwa, kiafya mtoto mchanga anatajwa kuwa na tumbo dogo mithili ya ngumi yake, hivyo matone machache ya maziwa ya mwanzo ya njano humshibisha.

Katika hilo, haishauriwi kumpa chakula kingine wala maji kwa kuwa anakuwa ameshiba, hivyo ziada ya lishe au maji inamkwamisha kunyonya maziwa ya mwanzo.

Pia, inaelezwa ni hali inayomzuia mama kutengeneza maziwa ya kutosha kwani kadiri mtoto anavyonyonya ndipo mama anazidi kutengeneza maziwa, jambo linalozaa umuhimu wa mama kumnyonyesha mtoto titi moja kwa muda wastani wa dakika takribani 20 hadi 30 mpaka amalize maziwa yote, kabla ya kumpa titi lingine kumwezesha kushiba kikamilifu.

MAZINGIRA

# Simulizi ya makubwa yaliyojificha kuhusu moto na darasa toka Moro

Na Sabato Kasika

## • Kwanini ulipuke, mtaji wake nini? • Moto wa gesi 'janga' la majumbani • Haya ndiyo makundi yake matano



Haya ndiyo mazingira ya moto uliotokea mjini Morogoro. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

VIUMBE hai vyote vinaufahamu. Binadamu, wanyama na wadudu wanaijua kwa kina na tabia zake.

Mimea, kupitia tabia ya kimaumbile yake, zaidi inauhisi na kupata athari zake. Lakini, licha ya kuwapo yote hayo, bado inarudi mtihani pale mtu anapohoji tafsiri ya moto ni kitu gani? Ni swali gumu kulidadavua.

Wanasanyansi kitaaluma wamelitolea tafsiri. Kwa mujibu wa mtandao mojwapo wa unaokusanya kazi za wanasanyansi (sciencelearn.org.nz/resources/7) wanautafsiri moto kuwa ni matokeo ya hali dhahiri ya kuungua kwa aina fulani ya kemikali.

Hiyo wanaieleza msingi wake unajumuisha hewa ya oksijeni na aina nyingine ya mafuta, ambazo zinapokutana katika msuguano mkali, zao la mwisho baada ya moto, huwa ni kitu kipya, mathalani majivu.

Watalaam hao wanafafanua zaidi wakisema, ili utokee moto, ni sharti patokee joto kali inayokuwa chanzo cha moto kuwaka. Ni kwa kiasi gani moto huo utadumu? Inategemea kiwango cha hewa ya oksijeni iliyopo, joto kali na mafuta ndani yake.

Vilevile, anataja kasi ya moto kutokea inategemea nguvu ya msuguano, huku wataalamu wakienda mbali zaidi kwamba, kuna aina ya msuguano huanzisha cheche na kuzaa mlipuko.

Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Nchini, ambalo kimsingi ndilo lenye jukumu la kuzima moto na kuokoa maisha na mali katika majanga yatokanayo na moto, mafuriko, tetemeko la ardhi, ajali za barabarani na majanga mengine yanayofanana, nalo lina tafsiri rasmi ya moto.

Inspekta Joseph Mwasabeja, ni Msemaji wa jeshi la Zimamoto na Uokoaji nchini, ambaye katika mazungmzo na Nipashe hivi karibuni, naye kama walivyo wataalamu watafiti, ana ufafanuzi na undani wa dhana 'moto.'

Anachambua: "Kwanza tufahamu maana ya moto, je moto ni nini? Moto ni muwako unaotokana na mngongano endelevu wa kikemikali na baadaye huzalisha joto na mwanga.

'Mgongano huu endelevu, ni lazima kuwe na vitu vitatu muhimu ambavyo ni hewa ya oksijeni, joto la kutosha na 'fuel' (mafuta), yaani chakula cha moto, ambacho ni kitu chochote kinachoweza kuwaka."

### MADARAJA YAKE

Inspekta Mwasabeja anaufafanua moto, kwamba umegawanyika katika madaraja makuu matano, akisisitiza ni muhimu Watanzania kuyafahamu, kwa vile dhana moto ni kitu hatari kwa mali, afya, pia maisha ya watu na viumbe.

Anataja kuwapo Daraja A kuwa ni moto unaotokana na vitu vya asili ya mimea, kama vile karatasi, mbao, nguo na vingine vya aina hiyo.

> **Wataalmu wa elimu ya matumizi ya gesi wanadokeza kuwapo kasoro katika biashara ya gesi zikiwa na upungufu, unaopaswa kufanyiwa kazi na mteja.**



Msemaji wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Nchini, Inspekta Joseph Mwakabeja.

Pia, anataja Daraja B, kuwa ni moto utokanao na vimiminika vinavyowaka, au ilivyozoeleka na wengi; moto wa mafuta.

"Daraja C, ni moto wa gesi inayowaka na milipuko yote itokanayo na gesi. Moto huo tunauweka katika daraja C na daraja D. Kwenye moto huu, viunguavyo ni vitu vyenye asili ya madini kama vile chuma," anasema.

Msemaji huyo anataja daraja la tano la moto ambalo ni F au K, kuwa unaosababishwa na mafuta ya kupikia yanapochemka sana na endapo yatapata chanzo kidogo cha kisababishi cha moto, huweza kuwaka.

"Hapa ni muhimu nitoe ufafanuzi. Kwanza katika miaka ya '80' kulikuwapo Daraja E la moto ambalo ni umeme, lakini baadaye ikabainika hakuna moto wa umeme, bali umeme ni chanzo kikubwa cha moto," anasema.

Inspekta Mwasabeja anaeleza kwamba, baadaye katika miaka ya 2000, Waingereza waligundua moto Daraja F, ni mafuta ya kupikia na anafanua kuwa nchini Marekani linaitwa daraja K.

### KUEPUKA AJALI

Inspekta Mwasabeja, anasema gari lolote lenye shehena ya mafuta linapoanguka, busara ni kwamba halipaswi kukaribiwa na mtu asiye mtaalamu vita dhidi ya moto.

Anafafanua tahadhari haiishi katika mafuta pekee, bali bidhaa nyinginezo zinazosafirishwa katika mfumo wa sumu na kemikali hatari.

Mtaalamu huyo anataja mbinu hiyo ndio sahihi zaidi, inayosaidia usalama wa watu dhidi ya kusogelea eneo lenye ajali, kwa lengo la kuiba au kushuhudia, badala yake wakae mbali kutoa taarifa kwa mamlaka husika.

Kwa mujibu wa jeshi hilo, mara inapotokea ajali, watu wanatakiwa kuwa umbali wa mita 500 (nusu kilomita ) kutoka eneo la tukio na kupiga simu namba 114, ili mamlaka ziweze kuchukua hatua haraka.

"Zimamoto inapofika kwenye eneo la tukio, huweka alama za onyo kuanzia umbali wa mita 25 kutoka ilipo ajali ili kwamba hata ukitokea mlipuko, basi iwe rahisi watu kusalimika," anasema Inspekta Mwasabeja.

Anafafanua kuwa, hayo yanafanyika ili kutenganisha eneo salama na hatari, lakini anaeleza masikitisho yake watu badala ya kuzingatia maelekezo hayo, baadhi wanakimbilia ajali ama kwa kujineemesha au kushuhudia tukio.

Ushauri wake, ni vyema jamii ikazingatia elimu inayotolewa, kuhakikisha wanakuwa salama na mali zao badala ya kujiingiza kwenye majanga, ambayo mwisho wake si mzuri.

"Vilevile, mbali na kuchota mafuta baada ya lori kuanguka, pia wanatakiwa kujua matumizi sahihi ya majiko ya gesi badala ya kufanya kienyeji, kwani nayo ni hatari iwapo mtumiaji hatazingatia maelekezo," anasema.

### MITIHANI GESI

Inspekta Mwasameja anafafanua kuwa, gesi lenye mtungi, ni muhimu mtungi uwe nje huku nyaya zake ndizo zinazoingia ndani ya nyumba.

Ushauri mwingine wa kitaalamu, ni kwamba kwenye majiko nyaya zake zinapaswa kutumika kwa muda si zaidi miaka miwili kisha zinunuliwa mpya.

Majiko yasiyo na mitungi je? Ushauri wake, wapikaji watumie nje, kwani ni hatari gesi kujaa ndani ya nyumba.

Pia, ndio maoni ya Inspekta Mwasabeja, kwa wanaotumia majiko ya mkaa wapikie nje kwa ajili ya usalama wao, akiongeza hata hewa itokayo si salama.

Wataalmu wa elimu ya matumizi ya gesi wanadokeza kuwapo kasoro katika biashara ya gesi zikiwa na upungufu, unaopaswa kufanyiwa kazi na mteja.

Nao wakufunzi kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, wanashauri mtu anaponunua gesi na kuifikisha nyumbani asubiri kwa wastani dakika 30 hadi 45, ili gesi itulie kwanza kutokana na misukosuko ya ubebaji kabla matumizi.

Watumiaji majiko hayo, pia wanapewa mbinu za kubaini wizi unaofanywa na wajanja wachache wauza gesi kwamba ni kuweka mtungi kwenye dyaba lenye maji au jiko dogo la gesi kwenye ndoo ya maji.

"Kama mtungi utakuwa haijajaa gesi, utaelea kwenye maji na kama jiko nalo litakuwa halijajaa, litaendelea, pia kama mtungi utakuwa umetoboka itakuwa ni rahisi kubaini," anasema.

### AJALI NCHINI

Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, linasema kumekuwapo na ajali za moto katika maeneo mbalimbali na hasa ule wa Daraja B, unaotokana na vimiminika vinavyowaka.

Inspekta Mwasabeja, anatoa mfano mwaka 2002 ilitokea ajali ya moto wa mafuta katika eneo la Ideweli mkoani Mbeya na kusababisha vifo vya watu zaidi ya 30 na wengine 100 walijeruhiwa, baada ya gari kupata ajali na wao kuchota mafuta.

Anataja nyingine ilitokea mwanzoni mwa mwezi uliopita mjini Morogoro na kusababisha watu zaidi ya 100 kupoteza maisha na kadhaa bado wanaendelea kupatiwa matibabu hospitalini.

> **Wataalmu wa elimu ya matumizi ya gesi wanadokeza kuwapo kasoro katika biashara ya gesi zikiwa na upungufu, unaopaswa kufanyiwa kazi na mteja.**

Msemaji huyo wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, anasema Watanzania wanapaswa kujifunza kutokana na historia kwa kuwa tukio la moto si mara ya kwanza.

"Matukio kama hayo yanapotokea hasa ya magari yanayobeba mafuta na kemikali ni hatari, hatutakiwi kuyasogelea isipokuwa wataalamu kwa ajili ya kuondoa hatari iliyo mbele," anasema.

Wakati vifo vya Morogoro vinaendelea kuombolezwa na majeruhi wanauguzwa, Agosti 25 mwaka huu kuna ajali nyingine ya lori la mafuta ilitokea eneo la Benako, Ngara mkoani Kagera na watu wakakimbilia kwenda kuchota mafuta.

Inaelezwa, kwa bahati Polisi mkoani humo waliwahi kuwadhibiti.

Kwa sasa Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Elisha Gaguti, ameliagiza Jeshi la Polisi mkoani kuwasaka wote waliohusika kuchota mafuta kwenye lori hilo.

## Sakata nyama choma latinga Mahakama Kuu



Kitongoji ambako kuna malalamiko. Picha ndogo ni jiko kunakoandaliwa mishikaki. **PICHA: MTANDAO**

**Perth,** Australia

MWANAMKE nchini Australia, amewafikisha mahakamani majirani zake akidai kukerwa na uchomaji nyama katika eneo la nyumba yake.

Cilla Carden, kutoka jiji la Perth, Magharibi mwa Australia, amedai kuwa shughuli zao za uchomaji nyama, uvutaji wa sigara na kelele za watoto unavunja sheria za makazi ya watu.

Amefuata njia hiyo ya kisheria, ili shughuli hizo ziache kufanywa na majirani.

Hata hivyo, ni shauri lililochukua mkondo mrefu kisheria, sasa ikitinga katika Mahakama Kuu, baada ya mchuano na maamuzi ya awali kutofikia maafikiano sahihi.

Mahakama ya Jimbo, imetupa mbali madai yake kwa kusema kuwa hayana maana na ushahidi wa kutosha.

Mjadala wa hoja hiyo kizimbani, yalihusisha maelezo kama familia zinazoishi jirani yake kupunguza mwanga wa taa zao, kuwanyamazisha wanyama wanaofuga, pamoja na kuweka miti kwenye bustani zao za mapumziko.



Anasema kuwa, harufu ya moshi wa sigara na nyama choma, zimemsababishia ashindwe kuishi vizuri.

"Siwezi kufurahia sehemu yangu ya kupumzika. Wameweka jiko la nyama choma ili nifikiwe na harufu ya samaki - harufu pekee ninayopata ni ya samaki tu," anasema Cilla Carden, Jumatatu wiki hii.

Mahakamani alijibiwa kuwa familia hizo zinajaribu kuishi kama pamoja, Hata hivyo familia waliyokua wakilalamikiwa, wameshahamisha jiko lao la kuchomea nyama, kama sehemu ya kumsaidia mlalamikaji.

Mahakama iliongeza pia, familia hiyo wamekua hawawashi taa usiku na kuwazuia watoto kucheza kutokana na hofu walioipata kwa kushitakiwa.

Mama Carden alikata rufani kuhusu uamuzi huo katika Mahakama Kuu ya Australia Magharibi, alikabidhi kurasa zaidi ya 400 zenye malalamiko ya kukata rufani mwezi Machi.

Mwanasheria Mkuu wa Mahakama hiyo, anadai kuwa kurasa 400 zilikabidhiwa kwa mahakama zinashangaza an anongeza:

"Hawaruhusu watoto wao kutoka nje usiku. Hawajawasha taa kwa siku kadhaa wakiogopa hatua atakazozichua mlalamikaji na jirani yao. Hili halikubaliki."

Mwezi Julai mahakama iliamua dhidi ya mlalamikaji wakisema malalamishi yake yamekuwa mzigo mzito kwa majirani, huku mlalamikaji Carden akiwajibu kuwa atachukua hatua zaidi katika mahakama nyingine.

AFYA

KARDINALI PELL

# Kashfa ngono watoto ilivyor mzigo wa kuhamia jela miak

• Wapo walioibua madai zama;1961 na 1969 • Alipohojiwa alizibeba lawa
• Mdau vita ya vijana, Ukimwi, ndoa, mimba • Alisakata kabumbu hadi si

**Na Mwandishi Wetu**




George Pell, chini ya ulinzi baada ya kuhukumiwa. **PICHA: MTANDAO.**

NI wiki mbili au nusu mwezi uliopita kamili, kwa maana ya siku 15 sasa zimepita tangu msumari wa kisheria kuendelea kupigilia hukumu ya jela miaka sita, kwa Kardinali George Pell wa nchini Australia, akihusishwa na udhalilishaji watoto.

Hiyo ni baada ya kutupwa kwa rufani yake kutokana na hukumu aliyopewa wastani wa nusu mwaka uliopita.

Ni hali inayotafsiriwa kuingia katika rekodi kuwa kiongozi wa juu zaidi wa kanisa hilo duniani kukumbwa na kashfa nzito ya namna hiyo, hadi hatua ya hukumu kisheria, huku ikibeba sura ya pigo kwao.

Akiwa ametumikia nafasi ya Askofu wa Jimbo la Sydney tangu mwaka 1996 na kupandishwa cheo kuwa Kardinali mwaka 2003, Pell, mwenye umri wa miaka 78, shitaka na hukumu yake inaangukia katika kuwajibika wa udhallishaji watoto kingono.

Mnamo Juni mwaka 2017, ndipo alipoanza kusomewa mashitaka mahakamani na baada ya kesi kuendeshwa, Desemba mwaka jana, alitiwa hatiani kwa mashitaka matano yanayohusu udhalilishaji wavulana, matendo yanayoelezwa kutokea katika miaka ya 1990.

Hatimaye, Machi13 mwaka huu, Jaji Peter Kidd wa Mahakama ya Victoria, nchini Australia, alimhukumu kifungo jela miaka sita, ambayo haina fursa ya kisheria kupatiwa kifungo cha nje kupitia msamaha wa parole.

Kardinali hakuridhika, aliwasilisha rufani kupinga hukumu hiyo na ilisikilizwa kwa siku mbili, mwezi Juni mwaka huu na uamuzi wake wa tarehe 21mwezi uliopita, uliridhia hukumu ya awali kwamba aendelee kutumikia kifungo kwa adhabu ileile

**MAMBO YALIVYOMGEUKA**

Tangu mwanzoni mwa miaka ya 2000, kulianza kuwapo vuguvugu la kashfa kwa kanisa, jamii kupitia vyombo vya habari na mitandao ya jamii ilichachamaa, hata kanisa kuanza kulifanyia kazi.

Wakati sakata lilipoanza kuibuka mwaka 2002, aliyekuwa kijana wa miaka 12 mwaka 1961 (wakati analalamika alikuwa na miaka 41), alidai kudhalilishwa katika kambi ya vijana jijini Melbourne. Hata hivyo, aliondoa dai lake, kwamba lishughulikiwe na kanisa.

Baadaye ilishika sura pana, wanaharakati wakija juu na wanasiasa kama kawaida yao nao wakadakia hoja, moto ukawa mkubwa pale ilipokuwa hoja bungeni.

> **Kama dereva wa gari akampakia mwanamke na akamdhalilisha, sidhani kama ni sahihi kuuwajibisha uongozi wa kampuni.**

Ni jambo lililotokea, huku Kardinali Pell akizidi kukwea vyeo vya kanisa, hata akafikia kukasimiwa baadhi ya madaraka muhimu katika makao makuu ya Kanisa, ikiwamo kuingoza Sekretarieti ya Uchumi.

Mwishoni mwa 2012, serikali ya Australia iliunda tume kufuatilia kashfa hiyo na Kardinali Pell, akalipokea kwa tamko: "Nadhani ni fursa kuwasaidia wahanga, pia nafasi ya kusafisha hali ya hewa, kutofautisha kashfa na uzushi na kampeni ya vyombo vya habari dhidi ya Kanisa Katoliki."

Akizumgumza katika hotuba yake ya Krismasi mwaka huo, Kardinali alirudia kuwaomba radhi waathirika na akwaambia Wakristo wawasaidie walioumizwa na jinai hiyo kubwa ya udhalilishaji.

Tume iliendesha vikao vyake kati ya mwaka 2013 na 2017 na Kardinali Pell alitoa ushahidi mara kadhaa.

Mnamo Mei 27, 2013 Kardinali Pell, alitoa ushahidi mbele ya Kamati ya Bunge iliyofuatilia kashfa hiyo ya kuwadhalilisha watoto kutoka katika mhimili wa kanisa na mashirika mengineyo.

Katika majibu na ufafanuzi wake, kiongozi huyo alitamka: "samahani na samahani sana." Alikiri kashfa hiyo inamuangukia katika nafasi yake ya kulea kanisa.

Ushahidi aliutoa Machi 2014, akiwa jijini Sydney na kupitia mazungumzo ya video kutoka jijini Vatican, Agosti ya mwaka huo; pia kati ya Machi na Februari mwaka 2016.

Mmoja wa walalamikaji anayedai kudhalilishwa mwaka 1969, katika shule moja ya msingi chini ya usimamizi wa pell, alidai kiongozi huyo alimsikia akilalamika kuomba msaada, lakini hakufanya hivyo.

Hata hivyo, dai hilo lilitupwa baada ya Pell kujitetea kwa kutoa ushahidi wa pasi ya kusafiri, unaothibitisha kipindi cha dai la kashfa hakuwapo nchini Australia. Tume ililitupa dai hilo.

Kiongozi huyo aliangukiwa na kashfa nyingine ikimhusu alipokuwa Askofu wa Sydney, iliyohusishwa na udhalilishaji watoto 55, mzizi wa kashfa ukiangukia wakati hajapewa uaskofu.

Mwishoni mwa mwaka 2012, serikali ya Australia iliunda tume kufuatilia kashfa hiyo, ambayo Kardinali Pell kwa upande wake alipokea kwa tamko: "Nadhani ni fursa kuwasaidia wahanga; nafasi ya kusafisha hali ya hewa na kutofautisha kashfa na uzushi na kampeni ya vyombo vya habari dhidi ya Kanisa Katoliki."

Kardinali Pell, akitoa ushahidi katika vikao vitatu, mnamo March 2014 akiwa jijini Sydney na kupitia mazungumzo ya video akiwa jijini Vatican, Agosit 2014; pia kati ya Machi na Februari, mwaka 2016 nchini humo mwaka.

Katika ufafanuzi wake wa kikao cha mwaka 2014. Alieleza kwamba Kanisa Katoliki ni sawa na kampuni ya usafirishaji, akitumia mfano: "Kama dereva wa gari akampakia mwanamke na akamdhalilisha, sidhani kama ni sahihi kuuwajibisha uongozi wa kampuni."

Ni hoja iliyouamsha Umoja na Wazazi wa Watoto Waathirika wa Udhalilishaji, kupitia Rais wao Cathy Kezelman, aliyekuja juu 'kuponda' utetezi huo kwamba unazidi kuwavuruga, huku wenzake wakiunga kupitia mitandao ya jamii, wakitumia mawazo yanayofanana nayo.

Katika utetezi wake alipokuwa jijini Roma kati ya Februari na Machi 2016 akiwa katika hoteli moja, mbele ya watoto 15 waathirika na kuonyeshwa moja kwa moja kwenye televisheni, Pell aliapa

# mtupia ...a sita

## ...ma za waumini ...iku ya upadrisho





George Pell (aliyezungushiwa, aliyekaa mbele wa pili kutoka kulia), alipokuwa mcheza soka.



Kardinali George Pell, katika sura ya kusononeka.

kwa Biblia, akikiri kuwapo kosa.

Hata hivyo, alisisitiza tukio halikuwa na uhusiano wote na makusudi ya kanisa lake, akifafanua:"Kanisa limefanya kosa zito na inafanyia kazi marekebisho."

Baada ya kuhojiwa katika makao makuu ya kanisa hilo jijini Roma, Juni 2016 kupitia taarifa ya Kurugenzi ya Habari, ilitangaza Kardinal Pell kuendelea na nafasi yake ya Mkuu wa Sekretarieti ya Uchumi ya Kanisa.

Makao makuu ya kanisa, ilikataa kutoa kwa matamshi, ikiahidi kufanya hivyo baada ya kesi kwisha

### AFYA YAKE

Huku akiwa katika msukouko wa shitaka dhidi yake kutoka upelelezi wa Polisi, Kadinali Pell ndani ya kipindi hicho alifanyiwa ziara katika makao makuu ya kanisa,Vatican Roma, alikoripotiwa kuugua ghafla.

Shida hiyo ya kiafya aliripotiwa kuipata mnamo Januari 2010, hata akalazimika kwenda makao makuu ya kanisa kuhudumiwa kiafya. Ni suala lililozua mjadala kisheria, ukiwapo msukumo wa kisheria uliomhitaji nyumbani. Madaktari waliomtibu, walituma ripoti maalum iliyoeleza afya yake na kwamba hakufaa kusafiri angani, wakiahidi angetarajiwa kuwa

> Katika vita ya kutetea usalama wa mazingira naye amekuwa mstari wa mbele, katika moja ya hotuba zake akiwashambulia Wapagani wa Bara la Ulaya kuwa wanachangia uharibifu wa mazingira.

nafuu ifikapo Februari 2016. Mamlaka za kisheria ziliridhia.

Aliporejea Australia, mashtaka dhidi yake yaliendelea, akifanyiwa ukaguzi maalum kiafya ya mwili na akili akatiwa rumande wakati kesi inaendelea.

Hata hivyo, Desemba mwaka jana alipatiwa dhamana maalum kutoka gereza la Melbourne alipokuwapo, kwenda kwenye tiba ya figo.

### AFYA NA FAMILIA

Msimamo wa jamii ya vijana ambao wamemuangushia katika mikono ya sheria, kwanza ana historia nao hadi kufikia hatua kufanikisha kufanyika tamasha lao nchini Australia mwaka 2008, ikiwakusanya watu milioni 500 jijini Sydney.

Kutoka mkusanyiko huo alitoa kauli ya kuomba msamaha kwa niaba ya kuwapo vitendo vya aina ya udhalilishaji kufanyika na aliowaita 'baadhi ya waumini.'

Huko nyuma katika misimamo yake ya kikanisa, alikemea kitendo cha wanandoa kitengana na athari zake. Mwaka 2001 alipozungumza na radio moja, Pell wakati huo akiwa askofu, alihimiza ubaya wake, hasa kwa wanandoa wenye watoto.

Alielekeza maoni kwamba ndoa, ivunjike katika mazingira ya lazima kama vile ukiukwaji wa faragha ya wanandoa na akawa na orodha ya adhabu inayosaidia kulinda uhusiano wa kifamilia.

Kuhusu suala la kuwapo ushoga, mwaka 1990 alitamka kwanza anatambua kuwapo kwake, huku akiweka msimamo wa kutokubaliana nao huku, akiipa heshima mabaya kwamba "ni sumu mbaya kuliko sigara."

Ni eneo aliloenda nalo mbali, wakati, mwaka 1998 alikataa kuwalisha mkate kanisani 'mashoga' kanisani na miaka miwili kabla ya hapo, aliipinga azma ya serikali ya nchi yake kutaka kutunga muswada wa sheria inayowaruhusu mashoga kuasili watoto

Mnamo mwezi Februari mwaka 2007, Kardinali Pell, katika eneo lake la utawala alikemea tabia ya watu kutungaza mabaya ya marehemu wanapokuwa katika taratibu za mazishi na maziko, badala yake alihimiza utaratibu wa kikanisa kwamba ni wakati wa kutoa wasifu bora unaomhusu marehemu.

### UKIMWI NA NGONO

Kadinali Pell mwaka 2009 alijitokeza tena katika namna nyingine kuhusu vita dhidi ya Ukimwi, pale alipoungana na kiongozi wao mkuu, Papa Benedict wa 16, anayesimamia hoja ya mafunzo kanisa hilo kwamba, kupungua maradhi hayo daima hakutapatikana kupitia kinga ya kondomu.

Anaangukia msisitizo wa ndoa au kuacha vitendo hivyo, akiponda kinga kwamba inamhimiza mtu kutokuwa na tabia ya kuendekeza ngono na kushindwa kuchagua mwenza.

Hata hivyo, katika mtazamo wa namna ya pili ambayo alionekana kuongeza makali ya hoja yake kwamba, wakati wao wana kanisa huanza kwa kugawa kondomu ikiwa hatua ya awali kuibadili tabia.

Katika vita ya kutetea usalama wa mazingira naye amekuwa mstari wa mbele, katika moja ya hotuba zake akiwashambulia Wapagani wa Bara la Ulaya wanachangia uharibifu wa mazingira.

Katika suala la mapenzi ya jinsia moja amekuwa mkali, akikemea, tangu mara alipoingia katika nafasi yake alikumbukwa mwamzoni mwa mwaka 2000, kwamba ni ukiukwaji wa amri 10 za Mungu.

"Mafunzo ya Kikristo kuhusu mapenzi ya ngono, ni sehemu ya amri 10 za Mungu na muhimu kwa ajili ya afya ya mwanadamu," anasema Kardinali Pell, akitaja maeneo muhimu kama ndoa na familia.

### HISTORIA YAKE

Kardinali Pell, alizaliwa Juni 8, mwaka 1941 nchini Uingereza, akiwa mtoto wa muumini wa dini ya Kianglikana na mama yake ndiye alikuwa Mkatoliki.

Maisha yake ya ujana, katika ya mwaka 1956 na 1959, baada ya shule alikuwa msakata kabumbu maarufu, hata kuwahi kusajiliwa na vilabu vya Richmond na baadaye VFL, nchini Australia.

Kwanini aligeukia upande wa dini? Ana ufafanuzi: "...Nilihofu, nikashuku na hatimaye nikashawishika Mungu ananihitaji kufanya kazi yake."

Huku akiwa hajaupa kisogo kikamilfu, mwaka 1960, alianza mafunzo rasmi ya dira na mwaka 1963 alipatiwa nafasi zaidi ya kwenda kusoma ngazi ya shahada huko Roma, Italia ambako ni makao makuu ya kanisa hilo.

Huko hakuweka kando usakataji soka, hadi pale alipohitimu masomo na kupatiwa upadrisho, mnamo Agosti mwaka 1966.

Baada ya hapo alitumikia kanisani kwa mwaka mmoja, 1967, aliporudi darasani katika Chuo Kikuu cha Oxford, Uingereza na mwaka 1971, alitunukiwa Shahada ya Uzamivu ya Historia ya Kanisa.

Kardinali Pell ni mpenda vitabu na darasa, kwani baada ya kuwa kazini, hadi kufikia mwaka 1982 alisharudi na kutunukiwa shahada ya juu ya elimu, katika Chuo Kikuu, cha Melbourne

Nchini Australia, ni kipindi hicho alitumikia uongozi wa vitengo vya elimu kanisani, kati ya mwaka 1973 to 1983, ikiwamo kuongoza chuo cha kanisa kati ya mwaka 1973 na 1984, pia wakati huo huo mhariri wa jarida, kati ya mwaka 1979 na 1984.

Mwaka 1987, ndipo alipoteuliwa kuwa msaidizi wa askofu na miaka tisa baadaye, aliteuliwa kuwa Askofu wa Melbourne nchini Australia mnamo mwaka 1996, baadaye mwaka 1997 alihamishiwa jijini Sydney, Juni 2001.

AFYA

# Wajua sababu mtu kuendekeza tabia ya kuahirisha aliyopanga?

## • Watafiti waja njia nane muhimu

TABIA ya mwanadamu inaelezwa kuwa na mazoea ya kuchelewa na kuahirisha mambo. Tatizo linatajwa kuwa pale, anapokubali hali hiyo kuwa sehemu ya maisha yakea ya kila siku.

Watu wanaamua kuahirisha mambo, licha ya kujua madhara yake. Mwenendo wa kuchelewesha mambo kupindukia, unatajwa kuwa hatari kwa afya, kwa sababu unamletea mhusika msongo wa mawazo.

Moja ya athari hizo inatajwa ni kumfanya mhusika aachae mazoezi ya viungo au kula vyakula murua kwa afya.

Wakati mwingine muathiriwa, huenda akachelewa kumuona daktari, ili akafanyiwa uchunguzi wa kimatibabu, anapojikuta kuwa na dalili za maradhi.

Je utafiti wa kisaikolojia umekuja kutusaidia kuepukana na suala la kuchelewesha mambo tunayotaka kufanya kwa kuahirisha mara kwa mara bila kuwa na sababu za kimsingi?

Yapo baadhi ya mambo muhimu yanayoweza kusaidia kuondokana na tabia ya kuchelewesha au kuahirisha baadhi ya mambo;

Mosi, inatajwa mtu asitegemee azma pekee kupata motisha mwanasaikolojia, Ian Taylor, aliyebobea katika eneo hilo la kitaaluma, kupitia utafiti katika Chuo Kikuu cha Loughborough, Uingereza aligundua watu mara nyingi wanafikiria azma kufanya jambo, dhana anayoieleza kuwa haifai.

"Azma ni njia moja ya motisha, lakini sio mfano mzuri wa kufikia malenzo yako," anasema, badala yake ni kigezo cha azma kinachomfanya mtu kupuuza sehemu muhimu ya kazi itakayomfanikishia malengo yake.

Pili, anamkubusha mtu kuangazia manufaa ya kazi anayoiahirisha kila wakati, kama sababu halisi inayomfanya kuahirisha anachotaka kufanya ni hofu ya kufeli?

Fuschia Sirois, kutoka Chuo Kikuu cha Sheffield, Uingereza amekuwa akifanya utafiti kuhusu tabia ya kuchelewesha jambo au kuwa na mwenendo wa kuahirisha mambo kwa miaka 15.

Alichobaini ni kwamba, tatizo ni muda wote sio uvivu au ukosefu wa kuzingatia muda, bali tatizo ni kushindwa la kudhibiti hisia.

Ikiwa mtu ana hofu huenda asifaulu, atakiwa anatafuta 'vijisababu' vya kuahirisha mpango mzima, ili asijikute katika dhiki ya kushindwa kutekeleza jambo, hali inayomfanya kurejea tabia hiyo miaka nenda rudi.

Anasema, kuchelewesha huko kunakosesha muda wa kutosha kufanya jambo, hali inayomuweka katika hatari ya kufeli na ajihisi vibaya na huenda asifanye kabisa.

Ili kukabilia na hisia hizo, moja ya kinga au suluhisho ni kujaribu kuangazia umuhimu wa kazi anayotaka kufanya: huenda ukajifunza kitu au na kufurahia kazi yenyewe kuliko ulivyotarajia.

Tatu, ni kujiandaa mapema, mtu atakuwa anajiandaa. Ikiwa unajua kitu fulani kinakufanya uwe na tabia ya kuchelewa kufanya jambo, jiandae mapema kwa kutumia mfumo unaojulikana kama "kama halita" kuashiria umuhimu wa kile unachotaka kufanya.. Kwa vyovyote utalifanya kwa sababu huna budi..."

Huenda rafiki, kwa mfano akapendekeza mkutano mwisho wa juma wakati uliokuwa umepangwa kudurusu, badala ya kukataa pendekezo hilo, unaweza kupendekeza muda mwingine kama jioni hivi badala ya kuvuruga mipango yako.

Mwanasaikolojia wa Marekani Peter Gollwitzer alipofanyia uchunguzi wa watu 94 kwa kutumia mbinu hiyo, alibaini walikuwa na uwezo mara mbili au tatu zaidi ya kufikia malengo yao, ikilinganishwa na wasio na mpango huo.

> **Alichobaini ni kwamba, tatizo ni muda wote sio uvivu au ukosefu wa kuzingatia muda, bali tatizo ni kushindwa la kudhibiti hisia.**

Nne, Lifanye jambo lako kuwa rahisi zaidi kulianza. Je, imewahi kusikia juu ya usanifu wa kuchagua?

Katika maeneo ya kula inasadikiwa kuwa ukiweka matunda mahali zinapoonekana badala ya chokoleti, huwafanya wateja kula vyakula vilivyo na afya kwao.

Mfano, mtu anaweza kujiamulia mambo kama hayo maishani, kama vile kuvaa nguo ya mazoezi akiwa na mpango wa kufanya mazoezi mapema asubuhi, au weka nguo zako za mazoezi juu ya meza mahali unapoweza kuziona kwa urahisi kabla hujalala, ukiamka kitu cha kwanza utakachoona ni nguo zitakazo kukumbusha kile kinachokusubiri kabla ya kuanza siku.

Pia kumbuka kuweka kando vitu vitakavyokushawishi usifanye jambo ulilopanga kufanya.

Tano, jizawadie; Hali ya kuahirisha mambo kunamfanya mhusika ajihisi amejizawadia papo kwa hapo. Kutokana na hilo, wataalamu wanapendekeza haja ya kukabiliana na hali hiyo kwa kutumia njia mbadala.

Utafiti uliofanywa na Catherine Milkman, kutoka Chuo Kikuu cha Pennsylvania, umegundua watu wakipewa nafasi ya kusikiliza hadithi ya kusisimua ukumbini, kuna uwezekano wakarudi wakiambulia kusikiliza hadithi.

Anashauri, mhusika kufuta kitu kitakachompatia msukumo wa kufanya kazi.

Sita, kuza mtazamo wa kweli juu ya hali yako ya baadaye; Baadhi ya watu wanaamini watapata muda zaidi katika siku zijazo.

Kwa kawaida, hilo huenda lisifanyike na ndio maana watu wengi wanapuuza muda kukamilisha kazi wanayotarajia kufanya.

Mfano mzuri hai, watafiti wanarejea mpangilio wa mambo unaopatikana katika toleo la kwanza la kamusi ya Kiingereza ya Oxford. Mwaka 1860, ilitangazwa itachukua miaka miwili kuikamilisha, lakini haikukamilishwa hadi mwaka 1928. Hadi kufikia wakati huo ilishapitwa na wakati, ikaanza upya.

Saba, jihurumie; hoja ni kwamba mtu hawezi kufikia lengo lolote, ikiwa muda wake mwingi utaumalizia katika mitandao ya kijamii, badala ya kufanya kazi.

Ukweli ni kwamba, watu wanajihisi vibaya kuhusu kazi walio nayo hasa ikiwa utekelezaji wake unawapa changamoto. Bila shaka inaongeza hisia inayowapa usumbufu wa mawazo, ni jambo wasilotaka kuliwazia.

Katika utafiti uliofanywa dhidi ya wanafunzi wanaosomea mtihani, wale walijihurumia kwa kuahirisha wakati wa kudurusu walikuwa katika nafasi nzuri ya kujirekebisha siku zijazo, ikilinganishwa na waliojilaumu kwa kuendekeza tabia hiyo.

Wataalamu wanakumbusha mtazamo wa kujihurumia ni katika dhana ya "kosa ni kurudia kosa."

Nane, Jiangazie kwa njia nzuri unapozungumza yanayokuhusu; Mtu anapaswa kujiweka katika dhana ya kujitakia mazuri muda wote kufikia ndoto yake.

Katika kutimiza mtazamo huo wa kisaikolojia, muda mfupi kabla ya uchaguzi wa Urais Marekani mwaka 2008, kuna utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha California: watu waliojisajili kupiga kura waliombwa kushiriki kwa kujibu swali kuhusu wanavyojihisi "wapiga kura" na walivyohisi "wapiga kura". **BBC**



Kijana anayetafakari maisha yake. **PICHA; MTANDAO**



# Wataka mgogoro umalizwe haraka

Na Nebart msokwa, MBARALI

WAKULIMA wa Kijiji cha Igumbilo, Chimala wilayani Mbarali, wameiomba serikali kuingilia kati na kuainisha vizuri mipaka kati ya kijiji chao na Ranchi ya Matebete ili kumaliza mgogoro uliodumu kwa muda mrefu.

Wananchi hao walidai kuwa kwa sasa mpaka halisi kati ya vijiji hivyo haujulikani hali ambayo imekuwa ikisababisha mgogoro na mapigano ya mara kwa mara baina ya pande hizo mbili.

Wakizungumza kwenye mkutano wa hadhara, wananchi hao walidai kuwa kwa sasa hawana maeneo ya kuwatosheleza kulima baada ya maeneo yao ya asili kumilikishwa kwa wafugaji wa ranchi ya Matebete ambao ni jamii ya Wamaasai.

Mmoja wa wakulima hao, Paulo John, alisema kwa sasa wanakodishiwa mashamba yao kwa bei kubwa na kwamba wakati mwingine wanalazimishwa kulipa mara mbili ili kuepuka mazao yao kulishwa mifugo.

Alisema kwa muda mrefu mgogoro huo umekuwa ukiibuka miongoni mwa jamii hizo na bado haijapatikana suluhu ya kudumu ya unahatarisha amani baina yao.

"Tunaomba serikali itusaidie kuainisha mipaka halisi ya maeneo haya maana sasa tunaona kama tunaonewa na wenzetu, maeneo ambayo sisi tunaamini ni ya kwetu ya asili yanamilikiwa na wenzetu na haturuhusiwi kwenda kuyalima," alisema John.

Alimtuhumu Mwenyekiti wa Ranchi hiyo, Paulo Ole Kurupashi, kuwa amekuwa akiwakodishia baadhi ya maeneo hayo kwa bei kubwa mpaka Sh. 100,000 kwa ekari moja.

Katibu wa Ushirika wa Wafugaji wa Ranchi ya Matebete, Leteyo Kisota, alisema wafugaji hao wanamiliki eneo hilo kisheria na wana hati miliki tofauti na madai ya wakulima.

Alisema kwa muda mrefu wakulima hao wamekuwa wakiwachokoza kwa kuingilia maeneo yao ambayo ni ya kuchungia na kuanza kufanya shughuli za kilimo hali ambayo inakuwa chanzo cha vurugu baina ya makundi hayo.

"Sisi tunamiliki eneo hili kisheria na ni eneo pekee nchi nzima ambalo linamilikiwa na wafugaji kwa ajili ya kuchungia, sisi tuliamua kulimiliki ili kuondokana na migogoro ya mara kwa mara na wenzetu wakulima ndio maana tukajitenga huku," alisema Kisota.

Alisema awali kabla hawajamiliki eneo hilo walikuwa wanatangatanga na mifugo yao katika maeneo mbalimbali kutafuta malisho na maji hali ambayo ilikuwa inawafanya waingie kwenye migogoro na wakulima pamoja na baadhi ya hifadhi za taifa.

# Kiongozi mbio za Mwenge atema cheche

Na Nebart Msokwa, CHUNYA

SERIKALI wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, imeagizwa kuhakikisha inakamilisha marekebisho ya miradi miwili ambayo Mwenge wa Uhuru umezindua na kukabidhi taarifa kabla haujatoka katika mkoa huo.

Agizo hilo lilitolewa jana asubuhi na Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Mzee Ali, wakati wa makabidhiano ya Mwenge huo kati ya Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika.

Kiongozi huyo aliitaja miradi hiyo kuwa ni pamoja na kukamilisha vyoo kwenye nyumba ya walimu katika Shule ya Msingi Kambikatoto ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua familia mbili na kupaka rangi ya pili ili iendelee kutumika.

Mradi mwingine alioutaja Ali ni zahanati ya Isangawana ambayo aliagiza shimo la kuchomea taka liongezwe kuchimbwa kwa madai kuwa lililochimbwa ni fupi na likibaki kama lilivyo, baadhi ya taka zitakuwa zinashindwa kuungua.

Pia katika zahanati hiyo, alisema baadhi ya maeneo swichi za umeme hazijawekwa, hivyo zinatakiwa kuwekwa haraka kabla umeme haujaingizwa.

"Nawashukuru sana viongozi wa Wilaya ya Chunya kwa kusimamia vizuri miradi ambayo tumeizindua na tuliyoiwekea mawe ya msingi. Sasa hakikishani ile miradi iliyoonekana kuwa na upungufu mnaikamilisha na kutukabidhi taarifa kabla hatujahama Mbeya," alisema Ali.

Aidha, aliwashukuru viongozi wa wilaya hiyo kwa kusimamia vizuri miradi kwa madai kuwa mingi imetekelezwa kwa viwango vinavyostahili tofauti na maeneo mengine ambayo alidai wamekuwa wakiikataa baadhi ya miradi kutokana na kutekelezwa chini ya kiwango.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Chunya ambaye ni Mkuu wa Wilaya hiyo, Mahundi, alishukuru kwa Mwenge huo kumaliza salama mbio katika wilaya yake kabla ya kukabidhiwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Mbeya.

Alisema atahakikisha anashirikiana na viongozi wengine wa wilaya hiyo kusimamia na kuhakikisha miradi iliyotajwa kuwa na mapungufu inarekebishwa mapema kama walivyoelekezwa na kukabidhi taarifa ya utekelezaji mapema.

Mahundi aliwashukuru viongozi wa mbio za Mwenge kwa ushauri walioutoa kwa wilaya yake na kwamba watahakikisha wanazingatia ushauri huo na kuufanyia kazi ili miradi yote inayotekelezwa inakuwa na viwango vinavyoainishwa.

"Tunashukuru kwa maelekezo na tutahakikisha tunayatekeleza kabla ya muda tuliyopewa, lakini tunawashukuru viongozi hawa kwa kutupatia changamoto maana tunaamini zitatusaidia katika kutekeleza miradi yote," alisema Mahundi.

Mwenge wa Uhuru uliingia katika wilayani Chunya ukitokea katika Mkoa wa Tabora, ambapo Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alikabidhiwa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Agrey Mwanri, katika Kata ya Kambikatoto.

Chalamila alisema miradi itakayowekwa mawe ya msingi na itakayozinduliwa ndani ya mkoa wake ni 59.



Mbunge wa Liwale mkoani Lindi, Zuberi Kuchauka (mwenye baraghashia na kitabu mkononi), akikagua matofali yatokanayo na mifuko 50 ya saruji aliyotoa kuchangia ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Ngorongopa, juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Wapania kuongeza uzalishaji maharage

Na Nebart Msokwa, MBEYA

KIKUNDI cha wanawake wanaolima maharage kwenye Kata ya Mshewe wilayani Mbeya kijulikanacho kwa jina la 'Zinduka' kimesema kinakusudia kuongeza uzalishaji wa zao hilo baada ya kupewa mtambo wa kisasa wa kukaushia maharage.

Kikundi hicho kilikabidhiwa mtambo wa kisasa wa kukaushia zao hilo unaotumia nishati ya jua (bean solar drier) na taasisi ya kimataifa inayoshughulikia kilimo cha mazao ya kitropiki (CIAT) ili kukisaidia kikundi hicho kuokoa mazao yaliyokuwa yanaoza kutokana na kushindwa kukauka hasa kipindi cha mvua.

Wakizungumza na Nipashe jana, wanachama wa kikundi hicho walisema kabla ya kupewa mtambo huo walikuwa wanapata shida kukausha maharage kipindi cha mvua na kusababisha sehemu kubwa ya mavuno kupotea kwa kuoza.

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Witness Sikayange, alisema kikundi hicho kina wanachama 21 na kinalima ekari 300 za maharage na kwamba kwa mwaka wanalima misimu mitatu ukiwamo mmoja wa kiangazi ambao wanatumia mbinu ya umwagiliaji.

Alisema mavuno mengi wanapata msimu wa mvua, hivyo kusababisha mazao kuoza yakiwa shambani au yakiwa yamevunwa na kuhifadhiwa ndani ya nyumba na hatimaye kukosa soko hali ambayo imekuwa ikiwasababishia hasara.

"Tunawashukuru CIAT kwa mtambo huu na tunaamini kuwa utatuongezea nguvu ya kuzalisha, tofauti na ilivyokuwa awali ambapo tulikuwa tumeanza kupunguza uzalishaji. Hawa wataalamu wametueleza kuwa mtambo huu una uwezo mkubwa wa kukausha mazao," alisema Sikayange.

Alisema kikundi hicho kimekuwa kikishirikiana na wataalamu wa kilimo kutoka katika taasisi mbalimbali za serikali na binafsi ikiwamo Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) Kituo cha Uyole, wataalamu kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na Ofisa Kilimo wa Kata hiyo. Alisema kabla hawajaanza kushirikiana na wataalamu hao walikuwa wanatumia mbegu za kienyeji pamoja na mbinu duni za kilimo hali iliyokuwa inawafanya wazalishe chini ya kiwango, lakini kwa sasa wanazalisha kuanzia kilo 600 mpaka 800 kwa ekari.

Mratibu wa Mtandao wa Utafiti wa Maharage Kusini mwa Bara la Afrika, Rolland Chirwa, alisema mtambo huo una uwezo wa kukausha tani moja ya maharage kwa siku na kwamba ni salama kwa mazao kutokana na kuzuia mifugo kula na mvua kunyeshea.

Alisema waliamua kukisaidia kikundi hicho cha Zinduka baada ya kubaini kuwa kina uwezo mzuri wa kuzalisha na kina watu wanaojituma ikilinganishwa na vikundi vingine.

Chirwa alisema kwa kawaida mazao ambayo yameoza hayawezi kuuzika sehemu yoyote na badala yake inakuwa hasara kwa wakulima na akawataka wanakikundi hao kuutunza vizuri ili wafaidike zaidi.

Mtafiti wa Maharage kutoka Tari Uyole, Agness Ndunguru, alisema moja ya vitu walivyokisaidia kikundi hicho ni pamoja na kuwapatia elimu ya kilimo bora na kuwasaidia mbegu za kisasa.





# Katibu Mkuu ampa kibarua kizito DMO

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Dk. Dorothy Gwajima, amemwagiza Mganga Mkuu wa Wilaya Chamwino, kuifanyia kazi haraka changamoto ya ukosefu wa kitanda cha kujifungulia wajawazito katika zahanati ya kijiji cha Chiboli wilayani humo.

Dk. Gwajima alitoa agizo hilo jana alipoitembelea zahanati hiyo na kukagua miundombinu mbalimbali.

"Suala la ukosefu wa kitanda kwa ajili ya wajawazito namtaka mganga mkuu wa wilaya kuifanyia kazi ndani ya siku tatu kiwe tayari kimeshafika hapa ili kinamama hawa waendelee kupata huduma kama kawaida," alisema Dk. Gwajima.

"Kitanda hicho anatakiwa kukileta haraka ndani ya siku tatu, kitatoka wapi yeye atajua kwani MSD wapo hapa Dodoma. Anatakiwa kukileta haraka na nitampigia simu," aliongeza Dk. Gwajima.

Awali, muuguzi wa zahanati hiyo, Shija Makeja, alimweleza naibu katibu mkuu huyo kuwa wanakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa watumishi.

"Mmoja wa watumishi wetu alifariki (dunia) hivi karibu, hivyo tumebaki watumishi wawili tu. Tunaomba serikali kama inaweza kutuongezea wengine ili kuongeza nguvu," alisema Makeja.

Mwenyekiti wa kijiji hicho, Ernest Mgora, alimwomba Naibu Katibu Mkuu kuwawezesha kujenga kituo cha afya kwa kuwa hivi sasa zahanati hiyo inazidiwa na idadi ya wagonjwa.

"Tunaiomba serikali kama inawezekana tujenge kituo cha afya kwani hii zahanati yetu inatumika na watu kutoka katika vijiji vingine vitatu hata vile vya mkoa jirani wa Iringa kuja hapa kupata tiba," alisema Mgora.



Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Chenene, wakishiriki kufanya doria ya ulinzi wa msitu wa Chenene, uliopo katika Wilaya ya Chamwino na Bahi mkoani Dodoma juzi, kutokana na baadhi ya watu kuuvamia na kuvuna mkaa na wengine kufanya ujangili wa kuua wanyama. Wananchi hao wanakabiliwa na changamoto ya vifaa duni vya ulinzi pamoja na usafiri jambo ambalo limekuwa likisababisha kushindwa kuwakabili wahalifu hao. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Magari mabovu barabarani kukamatwa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SERIKALI imeagiza kuanzia Oktoba Mosi, mwaka huu, kukamatwa magari yote mabovu yanayotembea yakiwamo yale ambayo hayajakaguliwa na kupewa stika ya usalama barabarani na Jeshi la Polisi.

Uamuzi huo umefanywa baada ya kikao cha siku mbili cha Baraza la Usalama Barabarani kilichofanyika jijini hapa na kubaini chanzo cha ajali kubwa ambazo huleta hisia kali kwa jamii ni magari mabovu ambayo hutembea barabarani ovyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kikao hicho kilichojumuisha Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na mamlaka husika, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alisema katika baraza hilo kuna kamati ndogo ambazo zimepewa jukumu la kufanya uchunguzi wa ajali ambazo zimetokea hivi karibuni na kuwasilisha ripoti za uchunguzi.

Alisema moja ya kamati zilizoteuliwa ni ile ya ajali na usafirishaji ambayo itaendelea kufanya uchunguzi wa kina na baadaye kutoa mapendekezo ya namna bora ya kuzuia ajali ikiwa ni moja ya malengo waliojiwekea ya kupunguza ajali zinazotokea barabarani.

"Tumegundua ajali kubwa husababishwa na na magari mabovu, hivyo tumejipanga kuyaondoa magari hayo kuanzia Oktoba Mosi," alisema Masauni.

Kutokana na hali hiyo, alisema inaonyesha jinsi gani mwaka huu ukaguzi wa magari mabovu haujafanyika ipasavyo, hivyo jitihada zaidi zinaendelea katika udhibiti wa magari mabovu kuendelea kuwapo barabarani.

Alisema hiyo ni moja ya mikakati ya muda mrefu ambayo serikali imejiwekea kwa kushirikiana na mamlaka zingine lengo likiwa kuona ajali za barabarani zinazosababishwa na uzembe zinatoweka kabisa.

Katika kutekeleza hilo, alisema jamii inapaswa kuzingatia agizo hilo ili ifikapo Oktoba Mosi, magari yote mabovu ambayo hayajafanyiwa ukaguzi na kupewa stika ya usalama barabarani, yaondolewe barabarani.

"Naomba jamii izingatie agizo hili hakuna msamaha wowote utakaotolewa ukibainika na makosa hayo," alisema Masauni.

Masauni pia alisema moja ya mikakati waliyojiwekea ni kuhakikisha usimamizi na udhibiti wa magari mabovu unafanyika kiufasaha.

Sambamba na hilo, alisema serikali kupitia mpango mikakati iliyojiwekea imepanga kuweka askari katika vituo maalumu ili kupunguza kusimamishwa kwa magari ovyo barabarani hususani yale yanayokwenda masafa ya mbali.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni pamoja kutaka kuleta ufanisi katika utendaji kazi kwenye magari hayo hususani mabasi, maroli pamoja na mengine yanayokwenda masafa marefu.

## Mahiga ampa tano Makonda

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Balozi Augustine Mahiga, ameahidi kuifanyia kazi sheria ya mirathi ikiwamo kuangalia jinsi ya kuwapo adhabu ndani yake kwa wasimamizi watakaokiuka pale itakapofanyiwa marekebisho na kupitishwa.

Kauli ya Balozi Mahiga imekuja baada ya Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam, Paul Makonda, kuwasilisha ombi la marekebisho ya sheria ya mirathi na ndoa ambazo zinaonekana kuwakandamiza wajane.

Akizungumza baada ya kupokea waraka huo, Waziri Mahiga alisema anamshukuru Makonda kutokana na kuwakumbusha kitu muhimu ambacho hakijawahi kujadiliwa kwa kina kama alivyokitilia mkazo.

Balozi Mahiga alisema amepokea mapendekezo hayo na kuahidi kuwa wizara yake ndiyo mhusika mkuu wa sheria, hivyo watalisimamia kiufasaha na kulitekeleza.

"Kama ulivyosema umekuja kukata rufani kwangu, basi uko sahihi kwa sababu wizara hii ndiyo mhusika mkuu na tutalisimamia kikamilifu," alisema.

"Ninasema hivi sababu suala la wanawake kunyanyaswa lipo kwa muda mrefu na limekuwa likijadiliwa lakini kwa upande wa mirathi lilikuwa halitiliwi mkazo kama unavyofanya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam," alisisitiza.

Waziri alisema uthubutu huo unaonyesha jinsi gani jitihada za Makonda zilivyo mstari wa mbele katika kuhakikisha wanawake hasa wajane wanapata haki zao za msingi hususani mirathi.

Alisema kuna mambo mengi ya unyanyasaji wa kijinsia unaofanyika vijijini na mijini, lakini mengine hayafiki sehemu husika kutokana na kukosa watu wa kuyafikisha.

"Mapendekezo haya yamenipa mwongozo na wiki hii nitawasilisha bungeni kwa sababu nimekuwa nikiulizwa maswali katika Bunge lililopita," alisema Mahiga.



# Wizara yalalamika ukataji barabara kupitisha mabomba

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KATIBU Mkuu Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Mustafa Aboud Jumbe, amesema changamoto kubwa inayoikabili wizara hiyo ni baadhi ya taasisi kukata barabara kwa ajili ya kupitisha huduma za kijamii hali inayoleta uharibifu mkubwa wa barabara.

Aliyasema hayo Ikulu mjini Zanzibar wakati wizara hiyo ikiwasilisha taarifa za Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Wizara hiyo kwa mwaka 2018/2019.

Alisema kumekuwapo na ukataji ovyo wa barabara na kupitisha huduma za maji na umeme unaofanywa na taasisi bila kuzingatia gharama za utengenezaji wa barabara hizo.

"Kuna baadhi ya taasisi mbili kwa nyakati tofauti hukata barabara kila mmoja na kupitisha miundombinu, jambo ambalo kama kungekuwapo na ushirikiano kwa taasisi kukaa pamoja kabla ya ujenzi na kupitisha miundombinu yao katika eneo moja, kusingekuwa na uharibifu huu wa barabara," alisema.

Naye Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Sira Ubwa Mamboya, alisema katika kipindi hicho wizara imepata mafanikio makubwa, ikiwamo kukamilisha ujenzi wa kilomita 28 za barabara mbalimbali Unguja na Pemba kwa kiwango cha lami.

Alisema wizara inaendelea na ujenzi wa Barabara ya Bububu-Mahonda-Mkokotoni, yenye urefu wa kilomita 31, wakati kilomita 28.8 za barabara hiyo zikiwa tayari zimewekwa kifusi tabaka la mwisho, pamoja na kuweka lami ya maji kilomita 14 katika upande mmoja wa barabara.

Akigusia azma ya serikali katika kuimarisha ujenzi wa miundombinu, Dk. Sira alisema wizara imefanikiwa kununua vifaa vya ujenzi ambavyo tayari vimewasili nchini.

Alisema wizara imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa meli mpya ya mafuta (MT Ukombozi 11), ambayo imeshawasili nchini tangu Agosti 7, mwaka huu.

Dk. Sira alisema wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imefanikiwa kuimarisha huduma katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume (AAKIA) kwa kuimarisha ulinzi na usalama, ufungaji wa mkanda wa mizigo, ununuzi wa mashine tano mpya za ukaguzi, kuimarisha ukumbi wa marais pamoja na kuendelea na ufungaji wa vipoza hewa.

Kwa upande wake Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, alisema kuna umuhimu kwa wizara na taasisi za serikali kushirikiana ili kufanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa wakati.

Alisema kuna baadhi ya miradi ya maendeleo ambayo imeshindwa kutekelezwa kwa wakati, kutokana na ukosefu wa ushirikiano, baada ya taasisi kuwa na mitizamo inayokinzana katika suala la uwekaji wa miundombinu.

Alieleza kuwa, kabla ya mradi wowote wa maendeleo kuanza kutekelezwa, ni muhimu kwa taasisi zenye miundombinu inayoingiliana kukaa pamoja na kuangalia itakavyowekwa ili kuepuka gharama na uharibifu usio wa lazima.

Alisema kuna baadhi ya barabara zilizokatwa kwa ajili ya kupitisha miundombinu bila ya wenye mamlaka kuarifiwa hivyo alisisitiza umuhimu wa kuendeleza ustaarabu wa kufanyakazi kwa pamoja ili kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazojitokeza.

Dk. Shein alitoa ufafanuzi huo baada ya uongozi wa wizara hiyo kuelezea changamoto kubwa ya uharibifu wa barabara unaotokana na baadhi ya taasisi kupitisha miundombinu, ikiwamo ya maji na taa.



Makamu wa Rais wa Kwanza Chama cha Mabunge Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika Tawi la Zambia, Dk. Evans Chibanda, akizungumza na wanachama wa jumuiya hiyo, wakati wa semina ya matumizi ya teknolojia katika kuendeleza demokrasia iliyofanyika mjini Zanzibar juzi. Kulia ni Spika wa Bunge la Rwanda, Rebecca Kadaga na Mwenyekiti wa Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola Tawi la Zanzibar, Simai Mohamed Said. **PICHA: BUNGE**

# Mafuta ya mlangilangi, mkaratusi kuanza kuzalishwa

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KIWANDA cha makonyo kilichopo Pemba kinatarajiwa kuanza uzalishaji wa mafuta yanayotokana na malighafi ya mkaratusi na mlangilangi baada ya kukamilika kwa ukarabati mkubwa.

Meneja mkuu wa kiwanda hicho, Ramadhan Kombo Ferouz, alisema ukarabati huo umeanza kwa kuweka baadhi ya vifaa na njia mpya ya uzalishaji wa mafuta ya mkaratusi na mlangilangi.

Alisema uongozi wa kiwanda umechukua uamuzi wa kuzalisha mafuta hayo kufuatia kuwapo kwa soko la uhakika katika baadhi ya nchi za Asia ikiwamo China.

"Tumeanza ukarabati mkubwa wa matengenezo ya kuweka baadhi ya vifaa na mitambo ambayo itatumika kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta ya makonyo na mlangilangi," alisema.

Alisema ukarabati huo unafanywa kwa ushirikiano na kampuni ya Asia Roma kutoka China, ambayo itakuwa na jukumu la kununua mafuta hayo na kuyatafutia soko nje ya nchi.

Naye Mkurugenzi mwendeshaji wa Shirika la Taifa la Biashara ZSTC, Dk. Said Seif Mzee, alisema kazi kubwa inayofanywa kwa sasa ni kuwahamasisha wakulima kuongeza kasi ya kilimo cha miti hiyo.

Alisema kwa kuanzia shirika linakusudia kuyaendeleza mashamba yake yaliopo Matangatwani, Pemba kwa kuotesha miti hiyo kwa wingi.

Pia baadhi ya kamati za vijana za wilaya zimeanza kuhamasishwa kuimarisha kilimo cha mikaratusi na mlangilangi kwa ajili ya kujipatia kipato zaidi.

## Wanawake washauriwa kutooneana wivu nafasi za uongozi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

NAIBU Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, amewataka wanawake kuwa na uthubutu wa kugombea nafasi mbalimbali za uamuzi hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu mwaka 2020.

Aliyasema hayo katika mkutano wa kuhamasisha jamii kuhusu nafasi za uongozi kwa wanawake ulioandaliwa na Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (Tamwa), uliofanyika Shehia ya Magomeni, Mjini Unguja.

Alisema bado uthubutu wa wanawake ni mdogo na ndio maana katika vyombo vya kutunga sheria kumekuwa na ushiriki mdogo wa wanawake ikilinganishwa na wanaume.

Aliwataka wanawake hao kubadili tabia ya kuoneana wivu na roho mbaya wanapogombea nafasi za uongozi majimboni na badala yake kuwapa ushirikiano.

Pia aliwataka kupaza sauti zao katika vyama vyao vya siasa ili kuondoa changamoto zinazowakabili wanapogombea nafasi za uongozi ikiwamo rushwa.

Wakizungumza katika mkutano huo wanawake wa Shehia ya Magomeni, walisema elimu duni waliyonayo wanawake wanashindwa kupata nafasi za uongozi. "Tokea nyuma wanawake tumenyimwa elimu na wazazi wetu walikuwa wakiwapa elimu zaidi watoto wa kiume na ndio maana wanawake tupo nyuma," alisema Tatu Othman Kipingu, mkazi wa Shehia hiyo.

Alisema changamoto nyingine inayowakwaza wanawake ni kipato kidogo walichonacho na kushindwa kumudu gharama za uchaguzi.

Naye Khuzaima Hamdani, aliiomba serikali kupitia Tume ya Uchaguzi kupunguza gharama za uchukuaji wa fomu hasa kwa wanawake kwa kuwa kiwango kilichowekwa ni kikubwa.

"Tunaiomba serikali ipunguze gharama za uchukuaji wa fomu ili na sisi wanawake tupate fursa ya kugombea nafasi za uongozi," alisema.

Alisema ushindani mkali wa vyama vya siasa umesababisha wanawake kutopata nafasi za uongozi kwa sababu baadhi ya vyama vinaona vikimsimamisha mwanamke vitakosa nafasi.

# RC azuia watumishi kuanzisha NGO

**Na Mwandishi Wetu, KIGOMA**

MKUU wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali mstaafu Emmanuel Maganga, amepiga marufuku tabia ya baadhi ya watumishi wa serikali mkoani humo kuanzisha mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, na kwamba serikali inaandaa utaratibu wa kuyafuta mashirika yote yaliyoanzishwa na kushindwa kufuata sheria kwa kutafuta fedha za wahisani na kuzitumia kwa manufaa binafsi.

Akizungumza wakati akipokea msaada wa mabati 1,050 yenye thamani ya Sh. milioni 35 yalitolewa na benki ya NMB kwa shule za msingi saba katika halmashauri za wilaya ya Kasulu Mji, Uvinza na Buhigwe, alisema mtumishi wa serikali kuanzisha mashirika hayo ni kinyume cha taratibu za kiutumishi na kwamba mtumishi huyo atakuwa akiwaza kufanya kazi ya shirika lake badala ya kuwatumia wananchi kwa kazi aliyopewa.

"Nawaonyeni watumishi wa serikali msianzishe mashirika ama ya NGO, majukumu ni kukagua na kuisaida serikali... msiingie huko huwezi kuwa mchezaji halafu wakati huo ukawa mwamuzi ni makosa siku tukiyafuta tukakukuta huko tutakushughulikia," alisema Maganga.

Alishukuru benki ya NMB kwa kuwa sehemu ya jamii ya wananchi wa mkoa wa Kigoma kwa kutoa misaada mbalimbali ambayo alisema imekuwa ikiusaidia mkoa kupunguza baadhi ya changamoto zilizomo ndani ya jamii, huku akitoa wito kwa walimu wa shule za msingi na sekondari mkoani humo kutumia benki hiyo kujiendeleza kiuchumi kwa kukopa mikopo itakayowasaidia kuanzisha biashara zitakazowasaidia katika masuala mbalimbali ya kimaisha.

"Dunia hii watu wote maarufu na matajiri wakubwa wameendelea kwa kukopa, nendeni mkakope hasa katika NMB mimi siamini katika umaskini, kuzaliwa maskini sio kufa maskini," alisema na kuongeza:

"Serikali imewawekea utaratibu wa kufanya kazi ya serikali na kufanya biashara na mikopo mnayoikopa muitumie ipasavyo na sio kwenda kuongeza mke."

Meneja wa benki hiyo Kanda ya Magharibi, Sospeter Magesse, alisema hadi sasa benki hiyo imetenga zaidi ya Sh. bilioni moja kama sehemu ya faida yake kuirudisha kwenye jamii ambapo hadi sasa imetoa msaada wa vitu mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 81 kuusaidia mkoa wa Kigoma katika sekta za elimu na afya.

Pia Magesse aliongeza kuwa jitihada kubwa zinahitajika kwa wazazi kuwasaidia wanafunzi kusoma vizuri kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali katika kuhakikisha malengo ya serikali yanafikiwa kwa kiwango kikubwa. Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kasulu, Martha Moremi, alisema shule hiyo ina changamoto kadhaa ikiwamo ya upungufu mkubwa wa madawati 600 kati ya 900 yaliyopo, huku wanafunzi zaidi ya 2,000 wakilazimika kukaa chini kutokana na upungufu wa madawati hayo.



Mafundi wakiendelea na kazi kuweka lami katika barabara za pembeni katika eneo la Temeke, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Utafiti wabaini changamoto za wafanyabiashara ndogo

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

UTAFITI uliofanywa na Shirika la Kidini la Kuwahudumia Wakimbizi la Tanzania (TCRS) umebaini wafanyabiashara ndogo katika Manispaa ya Morogoro wanashindwa kukuza mitaji yao kutokana na changamoto mbalimbali.

Changamoto hizo ni ukosefu wa nafasi za kufanyia biashara, ukosefu ama upungufu wa mazingira mazuri ya kufanyia biashara pamoja na migogoro kati ya wafanyabiashara na mamlaka za serikali.

Nyingine ni ukosefu wa nafasi ya kufanyia biashara, kukosekana kwa mitaji ya uhakika, ukosefu wa elimu na stadi za biashara wanazofanya pamoja na kutokuwa na bima ya afya, jambo ambalo linawasababishia kutumia gharama kubwa za fedha na kuwamalizia mitaji.

Akiwasilisha utafiti huo katika kikao cha wadau kilichohusisha wafanyabiashara ndogo, maofisa watendaji wa kata na madiwani katika Manispaa ya Morogoro, Kiongozi mradi wa TCRS, Rehema Samuel, alisema ulilenga kubaini changamoto za kibiashara zinazowakabili ili ziweze kufanyiwa kazi au kupatiwa majibu.

Alisema sababu nyingine ya kufanya utafiti huo kutambua jitihada zinazofanywa na serikali pamoja na sekta binafsi kuwaendeleza wafanyabiashara ndogo na biashara zao pamoja na kuainisha na kupendekeza njia bora wanazoweza kuzitumia ili kuboresha biashara.

Kiongozi huyo mradi alisema kilichofanyika hadi sasa kwa wafanyabiashara ndogo kuwapa elimu ya masuala mtambuka kupitia kwa wataalamu kutoka Shirika la Viwanda Vidogo (Sido), kuwawezesha mafunzo ya ujasiriamali pamoja na kuwawezesha mafunzo ya kibiashara sahihi kwa njia ya teknolojia ya simu.

Mmoja wa watafiti hao kutoka Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT), ambaye alifanya utafiti kupitia TCRS, Dk. Wambuka Rangi, alisema changamoto ya wafanyabiashara ndogo kutojiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii imekuwa chanzo cha kushindwa kujiendeleza kibiashara kwa kuwa wengi wao wanakosa mikopo ya kuendeleza biashara zao na kuishia kulalamika.

## Ajali ya Hiace, pikipiki yaua

**Na Restuta Damian, BUKOBA**

MKAZI mmoja wa Manispaa ya Bukoba, amefariki dunia, baada ya pikipiki aliyokuwa amepanda kugongwa na basi la abiria.

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Revocatus Malimi, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kumtaja abiria wa pikipiki aliyefariki kuwa ni Jackline Mwombeki.

Kamanda Malimi alisema ajali hiyo ilitokea maeneo ya Kata ya Rwamishenye Manispaa ya Bukoba juzi saa 5:53 usiku, ambapo dereva wa pikipiki, Revocatus Mjwahuki, yenye nambari za usajili T.117 CBP iligongana na gari aina ya Toyota Hiace yenye namba T.865CDK.

Alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa pikipiki iliyokuwa ikitokea barabara ndogo kuingia barabara kuu na kugonga ubavuni mwa gari ya abiria lililokuwa likitokea eneo la Mutukula wilayani Missenyi.

## Wadau wataka mabadiliko VVU

**Na Rose Jacob, MWANZA**

WAKATI Tanzania na dunia kwa ujumla ikijitahidi kuja na mbinu mbalimbali ili kupunguza kasi ya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (VVU) na Ukimwi ikiwamo malengo ya dunia ya 90-90-90, wadau jijini Mwanza wamekuja na mapendekezo ya kurekebisha kifungu cha sheria kama sehemu ya kuunga mkono jitihada hizo.

Kupitia mradi wa 'Data Driven Advocacy (DDA)' ambao umejikita zaidi katika kifungu cha 15 (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Ukimwi ya Mwaka 2008, wadau hao wanaomba kifungu hicho kirekebishwe.

Kifungu hicho kinaelekeza kuwa mtoto au mtu yeyote ambaye hana uwezo wa kupokea matokeo, anaweza kupimwa VVU iwapo tu ana ruhusa ya maandishi kutoka kwa mzazi au mlezi anayetambulika.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Vijana na Watoto mkoani Mwanza (MYCN), Shaban Maganga, alisema kifungu hicho cha sheria kwa sasa kinambana mtoto na kumnyima haki ya kufahamu hali yake ya kiafya.

HABARI KIMATAIFA

# AU yalaani wageni kushambuliwa

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

MWENYEKITI wa Umoja wa Afrika (AU), Moussa Faki, amelaani ghasia hizo lakini ametiwa moyo na hatua zilizochukuliwa na Afrika Kusini za kuwakamata watuhumiwa.

Mbali na AU kulaani tukio hilo, Nigeria nayo imemwita balozi wao aliyeko Afrika Kusini na kutuma ujumbe mjini Pretoria ili kuelezea masikitiko makubwa dhidi ya raia wake kushambuliwa.

Rais wa Nigera, Muhammadu Buhari amechukua hatua hiyo kufuatia magenge ya raia wa Afrika Kusini kuvamia biashara katika sehemu tofauti za nchi hiyo, wakipora mali na kuchoma magari katika wimbi jipya la chuki dhidi ya wageni.

**Rais Buhari alimuagiza waziri wake wa mambo ya nje kumuita balozi wa Afrika Kusini ili kuelezea masikitiko yake juu ya vitendo wanavyofanyiwa raia wa Nigeria.**

Rais Buhari alimuagiza waziri wake wa mambo ya nje kumuita balozi wa Afrika Kusini ili kuelezea masikitiko yake juu ya vitendo wanavyofanyiwa raia wa Nigeria na kutaka hakikisho la usalama wao pamoja na mali zao.

Serikali ya Nigeria kupitia ukurasa wake wa mtandao wa Twitter iliandika kwamba ujumbe wake utawasili mjini Pretoria siku ya Alhamis na kukutana na Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa.

Rais Ramaphosa amelaani mashambulizi hayo akisema hayakubaliki.

"Mashambulizi dhidi ya wafanyabiashara wa kigeni ni suala lisilokubalika na hatuwezi kuruhusu litokee Afrika Kusini ambako watu wanaoendesha biashara zao wanashambuliwa, mali zao kuporwa na kuchomwa moto kitu ambacho ni kinyume na sisi waafrika kusini tunavyoamini" alisema Ramaphosa.

Nalo Shirikisho la Mpira wa Miguu la Zambia (FAZ), limefuta mechi ya kirafiki iliyokuwa ifanyike mjini Lusaka siku ya Jumamosi kutokana na vurugu hizo.

Kwenye taarifa yake iliyoitoa jana, FAZ inasema sababu za kusitisha mechi hiyo ni hali ya kiusalama nchini Afrika Kusini, hata kama Zambia ilikuwa mwenyeji.

Hadi kufikia sasa watu watano wamepoteza maisha kutokana na ghasia hizo, na polisi wamewakamata zaidi ya watu 80 kuhusiana na matukio hayo ya chuki dhidi ya wageni.

Raia kadhaa wa Nigeria walitumia mitandao ya kijamii kuhamasisha watu kuyasusia makampuni ya Afrika Kusini ikiwamo kampuni ya kutoa huduma ya simu ya MTN, DSTV na duka la Shoprite.

Ghasia za chuki dhidi ya wageni Afrika Kusini zina historia ndefu ambapo wazawa wamekuwa wakiwalaumu raia wa kigeni kwa kiwango kikubwa cha ukosefu wa ajira. Afrika Kusini ni kitovu cha wahamiaji wa kiuchumi kutoka nchi jirani za Lesotho, Msumbiji na Zimbabwe. Raia wengine hutoka mbali kama vile Kusini mwa Asia na Nigeria.

Mashambulizi dhidi ya maduka ya wageni yalianza siku moja baada ya madereva wa malori kuanza mgomo wa nchi nzima siku ya Jumapili kupinga hatua ya kuwaajiri madereva wa kigeni.

Vurugu hizo zimetokea kuelekea kongamano la kiuchumi la dunia litakalofanyika mjini Cape Town kuanzia Jumatano. **DW**



Raia wa Afrika Kusini wakipora mali katika maduka ya kigeni. **PICHA: AFP**

## Papa aanza ziara Afrika

**VATCAN,** Italia

PAPA Francis jana alianza ziara rasmi ya kihistoria barani Afrika, anatarajia kuzitembelea nchi za Msumbiji, Madagascar na Mauritius.

Mojawapo ya mambo yanayotarajiwa kuigubika ziara hiyo ni suala la umaskini, uhifadhi wa mazingira na ufisadi.

Wahudumu katika Kanisa Katoliki wamenukuliwa na baadhi ya vyombo vya habari wakisema kwamba ziara hiyo ni ya pili kwa Papa Francis kuwahi kuifanya kusini mwa jangwa la Sahara Afrika.


Wamesema ni fursa muhimu kutoa wito mpya uliogubikwa katika barua yake ya mnamo mwaka 2015 inayohusu mazingira.

Kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia (WB), Msumbiji imepoteza hekari milioni nane za misitu tangu miaka ya 70.

Masuala mengine yanayotarajiwa kuigubika ziara ya Papa katika mataifa hayo ya Afrika ni umasikini, vita na ufisadi au rushwa.

Katika mahojiano na kituo cha Vatican, Kadinali Pietro Parolin, ambaye ni Waziri wa Mambo ya Nje wa Vatican alisema Papa anatazamiwa kutuma ujumbe mzito kuhusu amani na majadiliano.

Licha ya kwamba baadhi hulihusisha Afrika na matatizo kama mizozo na majanga, kadinali huyo anaamini kuwa Afrika ni zaidi ya yote eneo lililo na utajiri wa utu au ubinaadamu, lenye utajiri wa maadili na Imani. **BBC**



Raia wa Afrika Kusini wakiwa wameshika silaha wakishambulia maduka ya wahamiaji na kuchukua mali zao. **PICHA: REUTERS**

## HABARI KITAIFA

# Wanaonunua 'changudoa' waonywa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WANAUME wanaojihusisha na tabia ya kununua wanawake wanaofanya biashara ya ukahaba, wameonywa kujiepusha kuwa wateja wa watu hao kwa kuwa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Onyo hilo lilitolewa bungeni jana na Naibu Waziri wa Mambo ya ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Maryam Msabaha, ambaye alisema kuna makundi matatu ambayo ni waathirika wakuu wa utupaji vichanga.

Alitaja makundi hayo kuwa ni kinamama wanaojiuza, watoto wanaofanya kazi nyumbani na wanaume wenye akili timamu wanawalaghai na kuwapa ujauzito lakini pindi wanapotaka huduma za kijamii, wanatishiwa.

"Nini kauli ya serikali kuhusu wahusika wa matukio hayo? Kwenye majiji makubwa kama Mwanza, Arusha, Dar es Salaam na Dodoma kuna ongezeko kubwa la biashara ya ukahaba. Je, serikali ina mkakati gani kupunguza matukio hayo ambayo kwa kiasi kikubwa kinababa ndio wahusika wakuu wa kununua makahaba hao?" alihoji.

Akijibu maswali hiyo, Masauni alisema endapo mtu atabainika kujihusisha na biashara ya kujiuza au kununua kahaba, hatua zitachukua pande mbili za shilingi.

Naibu Waziri huyo alisema hakuna kitu kinachohalalisha utupaji wa mtoto na hatua zitachukuliwa kwa mama anayetupa mtoto.

Pia alisema wanaojihusisha na kurubuni wanafunzi kuna Sheria ya Mtoto na adhabu yake ni kifungo cha miaka mitano.

Hata hivyo, aliagiza kinababa kujiepusha kuwa wateja wa biashara hiyo kwa kuwa shilingi ina pande zote mbili na ikibainika wote wanachukuliwa hatua za kisheria.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge huyo alisema kumekuwa na matukio ya mara kwa mara ya watoto wachanga kutupwa jalalani, mitaroni na katika mifuko ya Rambo.

Msabaha alihoji kauli ya serikali kuhusu matukio hayo na ni watuhumiwa wangapi walishakamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Akijibu maswali hayo, Masauni alisema katika kipindi cha Januari hadi Juni mwaka huu kumekuwa na jumla ya matukio 66 ya watoto wachanga waliopatikana wametupwa huku watuhumiwa 18 walikamatwa na kufikishwa mahakamani na kesi zao zipo katika hatua mbalimbali.

Alisema vitendo vya kutupa watoto majalalani, mitaroni na maeneo mengine ni kinyume cha sheria za nchi na haki za binadamu.

"Kwa mujibu wa kanuni ya adhabu sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002 chini ya kifungu cha 218 na 219, adhabu ya makosa hayo ni kifungo cha maisha, na serikali inalaani vikali vitendo hivyo na itaendelea kuchukua hatua kali dhidi ya wale watakaopatikana na hatia,"alisema.

Alieleza kuwa takwimu za matukio ya kutupa watoto wachanga zinaonyesha kuwa katika kipindi cha mwezi Januari hadi Juni mwaka huu kumekuwa na jumla ya matukio 66 ya watoto waliopatikana wakiwa wametupwa, 43 kati yao walikutwa hai na 23 walikutwa wamefariki dunia.

## Gharama leseni chuma chakavu sasa zashushwa

**Beatrice Moses na Jovin Lamwel,** TUDARCO

SERIKALI imeshusha gharama za leseni za vyuma chakavu kutoka Sh. milioni 10 hadi Sh. milioni tano, kuliagiza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuunda kikosi kazi maalum kuchunguza upya makontena zaidi ya 200 yanayotajwa kuwa na vyuma hivyo yaliyozuiliwa kusafirishwa nje ya nchi kwa sababu mbalimbali.

Hayo yamebainishwa na Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, jana baada ya kusikiliza maoni kutoka kwa wadau wa vyuma chakavu ambavyo pia utajwa kama taka hatarishi.

Alisema serikali imeamua hivyo ili kuwapa nafasi wafanyabiashara hao kulipa kodi, pia kushiriki kikamilifu katika kutunza mazingira. Gharama hizo zimeshushwa pia kwa wafanyabiashara wadogo wa vyuma kwa kufanyiwa Sh. 500,000 kwa leseni.

Alisema wamefikia hatua hiyo baada ya kufuatilia kwa karibu mambo yanayoendelea kwenye biashara hiyo, ambapo wamebaini mengi ikiwamo kiwango kikubwa cha rushwa na udanganyifu.

"Hii biashara miongoni mwenu wamekuwa wakitumia vibaya wapo wanaotumia kuficha madini na kuyasafirisha kwa vyuma chakavu, lakini pia kama ofisi yangu kama waziri wenye dhamana ambaye anatajwa kwenye sheria haijawahi kutoa kibali cha kusafirisha vyuma," alisema.

Alisema: "Pamoja na kuwa kwa kiasi kikubwa tumejadili changamoto na matatizo lakini tujaribu kutengeneza fursa za ajira zinapatikana lakini malighafi zinapatikana kwa viwanda vyetu, lakini tunaingiza fedha za kigeni kutokana na biashara hii."

Alibainisha kuwa ni kubwa na inavutia mtaji wa dola za Marekani zaidi ya Sh. bilioni 434.55 duniani. Pia alisema kuwa wamefuta vibali vyote vya zamani hivyo wafanyabiashara hao watatakiwa kuomba upya kwa wale waliolipia hawatadaiwa tena.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alibainisha kuwa walizuia makontena 280 ya vyuma hivyo kwenda nje ya nchi mbalimbali kutokana na kukiukwa kwa taratibu za usafirishajiwa mali hizo.



Mwonekano wa jengo jipya la 'Mwalimu Nyerere Foundation Square' lililopo jijini Dar es Salaam baada ya kukamilika kwa ujenzi. Jengo hilo lenye ghorofa 29 limejengwa na kampuni ya Kichina ya CRJE (East Africa), na linatarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Upelelezi kesi ya Mkurugenzi UDART

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imeambiwa kwamba upelelezi wa kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Mkurugenzi wa Mradi wa Mabasi yaendayo Haraka Dar es Salaam (UDART), Robert Kisena (46) na wenzake wanne bado haujakamilika.

Kesi hiyo imetajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi, Vick Mwaikambo.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (Takukuru), Fatuma Waziri, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, aliomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Mwaikambo alisema kesi hiyo itatajwa Septemba 17, mwaka huu na washtakiwa wamerudishwa rumande. Mbali na Kisena washtakiwa wengine ni mkewe Florencia Membe, Kulwa Kisena (33), Charles Newe(47) na raia wa China, Cheni Shi (32), ambao kwa pamoja wanawakilishwa na Wakili Nehemia Nkoko.

Washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka 19 ikiwamo kusababisha hasara kwa UDART ya Sh. bilioni 2.41.

Katika mashtaka hayo yapo ya kuongoza genge la uhalifu, kujenga kituo cha mafuta bila kibali, kuuza mafuta sehemu zisizoruhusiwa, wizi wa mafuta na utakatishaji fedha wa Sh. bilioni 1.2, kughushi na kusababisha hasara ya Sh. bilioni 1.4.

Inadaiwa Kisena, Kulwa, Simon na Florencia walijenga kituo cha mafuta ya petroli bila kibali kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura) na kipindi hicho wakiwa wakurugenzi walifanya biashara eneo ambalo halijaruhusiwa kujengwa.

Katika mashtaka ya utakatishaji fedha yanaomkabili Robert Kisena na Chen Shi, inadaiwa kuwa Aprili 8, 2016 katika benki ya NMB, Kisena akiwa Mkurugenzi wa UDART alihamisha Sh. milioni 594.92 kwenda kwenye akaunti nyingine ya Kampuni ya Longway Engineering Company, wakati akijua fedha hizo ni za haramu zilizotokana na makosa ya kughushi.

Ilidaiwa kuwa washtakiwa wote walisababishia UDART hasara kati ya Mei 25, 2015 na Desemba 2016 ya Sh. bilioni 2.41.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA KAZI

Anahitajika - Mhasibu na sales Lady
Sifa – Awe Mwanamke
Elimu – Diploma

Ofisi yetu ipo Posta – Dar es Salaam
Kwa Mawasiliano :- 0715 – 885 533


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA Tutumie
E-mail: advertise@guardian.co.tz,
au piga simu: 0767 223311


### KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**JALIATH HAMZA MSILIKALE** anatangaza kupotelewa na Result Slip yenye index namba S.5413-0031 iliyotolewa na SARANGA SEKONDARI mwaka 2018.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DAR/GOG/RB/253505/2019.**

115404402

### KADI YA GARI IMEPOTEA

JAMES COLMAN SALAKANA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI CHASSIS NO SXA160039152 ENGINE NO 352629367

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI

ARU/ARU/168658/2019.

215405002

### KUPOTEA KWA OFA YA KIWANJA

**ROBERT SIMON MAHEWA** anatangaza kupotelewa na ofa ya kiwanja Na. 6 kitalu M KINYAMBWA DODOMA yeyote atakayeiyona atoe taarifa kituo cha polisi, taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/257258/2019.**

215404702

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**PRINCE ARON NYATO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 321 DNJ** TOYOTA RACTIS. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DAR/KIJ/RB/174080/2019.**

115405502

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AMARKUMAR VIJAY KOTEDIA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **LEXUSRX300** yenye namba za usajili T 555 CRV, Chassis Na **JTJHF3LU200023541,** Engine Na.**1692801.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/269894/2019.**

215404802

### KUPOTEA KWA CHETI



**Caroline Shayo** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba S220/526 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 1992 kilichotolewa na Tabora Girls Sekondari,

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi .

Polisi Taarifa:
**KJN/RB/1896/19**

115403702

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Andrea Partson Mwandimbile** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Fuso Mitsubish yenye namba za usajili T686 cheses namba FK417JZ520032 injini namba 6M61 081793 Kilichotolewa kwa mtahiniwa namba S.0250 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa mwaka 2011 katika shule ya sekondari wasichana Murigha

yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Taarifa ya polisi RB. Namba IR/IR/RB/2097/2019**

215403502

### JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
### MAHAKAMA
### USIMAMIZI WA MIRATHI
### (S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)

Katika Mahakama ya Mwanzo **DODOMA MJINI**
Usimamizi wa mirathi **57/2019**

Ombi la **SHARIFA IDDY** kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu **HAMAD NASORO MAKALA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe **23/9/2019** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa

215404302

### JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
### MAHAKAMA
### USIMAMIZI WA MIRATHI
### (S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)

Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI
Usimamizi wa mirathi 54/2019

Ombi la **GLORIA JAPHET RAZALO** kuteuliwa Msimamizi wa mirathi Marehemu **EMMANUEL HAMIS NDOLOSI**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 13/9/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 2/9/2019

215404502

### KADI YA PIKIPIKI IMEPOTEA

QUALITY MOTOR LIMITED ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA HONDA YENYE NO T152 CUN

YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI

ARU/ARU/RB/267601/2019

215404902


Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako la
Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE
BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# CHIELLINI KUWA NJE YA DIMBA MIEZI SITA

**TURIN,** Italia

GIORGIO Chiellini atakuwa nje ya dimba kwa kipindi cha miezi sita baada ya kufanyiwa upasuaji wa goti, klabu ya Juventus imethibitisha.

Beki huyo wa kati, Chiellini mwenye umri wa miaka 35, aliumia wakati wa mazoezi Ijumaa iliyopita, huku Matthijs de Ligt aliyesajiliwa hivi karibuni kutoka Ajax akichukua nafasi yake kwenye kikosi cha Juventus wakati kikiibuka na ushindi wa mabao 4-3 dhidi ya Napoli wikiendi iliyopita.

"Giorgio Chiellini amefanyiwa upasuaji wa goti lake la kulia," ilisema taarifa ya Juventus jana.

"Operesheni hiyo ilifanyika katika kliniki ya Hochrum mjini Innsbruck na profesa Christian Fink pamoja na daktari wa klabu ya Juventus, Dkt. Tzouroudis, na ilifanyika kwa mafanikio makubwa.

"Anatarajia kupona baada ya kipindi cha miezi sita."

Juve imeshinda mechi zake mbili za ufunguzi wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, msimu huu wakiwa kwenye mbio za kuwania taji lao la tisa mfululizo na sasa kwa muda mrefu watakuwa bila Chiellini.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Italia anatarajiwa kuwa nje ya uwanja hadi Machi mwakani, maana yake kwamba atakuwa fiti wakati wa michuano ya Ligi ya mabingwa Ulaya itakapokuwa hatua ya robo fainali kama Juventus itafuzu.



# United yajipa matumaini kumsajili Eriksen

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inapanga kujitosa kwenye usajili wa kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen baada ya Real Madrid kushindwa kumsajili raia huyo wa Denmark wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Na hiyo imewapa matumaini miamba hao wa dimba la Old Trafford kwamba wanaweza kumsajili Eriksen, ambaye amebainisha mwenyewe kwamba anataka kutafuta changamoto mpya.

Mkataba wa sasa wa Eriksen unamalizika mwishoni mwa msimu huu na watalazimika kumuuza wakati wa dirisha dogo la usajili Januari ili kupata fedha, kwani atakuwa na uwezekano wa kuondoka akiwa huru.

Eriksen alifunga bao la uongozi wakati Spurs wakiongoza 2-0 dhidi ya Arsenal kwenye mchezo wa 'dabi' ya timu za Kaskazini mwa jiji la London kabla ya mchezo huo kumalizika kwa sare ya 2-2.

Kuhusu uwezekano wa kuondoka kipindi kijacho cha usajili, Eriksen alinukulia akisema: "Ningefurahi kama ningeweza kuwa na maamuzi ya wapi pa kwenda, lakini bahati mbaya siwezi.

"Kwangu mimi sio ngumu kuamua kupata changamoto mpya. Sisomi nyingi vinavyoandikwa kuhusu mimi.

"Na sasa nimekuwa nikihusishwa kwa miaka mingi, ambako kumekuwa na uvumi mwingi kuhusu mimi kila mwaka.

"Lakini ni wazi kwamba, kumekuwa na mambo mengi mwaka huu kuhusu majaliwa yangu kwa sababu mkataba wangu unakaribia kumalizika. Yamezungumzwa mengi kuhusu mimi."

# Moreno: Nitampisha Enrique ukocha Hispania

**MADRDI,** Hispania

KOCHA wa Hispania, Robert Moreno, amesema yupo tayari kuachia ngazi kama Luis Enrique akiamua kurudi kwenye ukocha.

Enrique alitangaza kujiuzulu kama kocha wa timu ya taifa ya Hispania Juni 19 mwaka huu na msaidizi wake, Moreno akachukua nafasi yake.

Moreno amechukua majukumu ya kukiongoza kikosi cha kwanza tangu Machi 26 baada ya Enrique alipokwenda likizo kwa ajili ya kumuuguza binti yake wa kike mwenye umri wa miaka tisa, Xana, ambaye alifariki wiki iliyopita baada ya kuugua saratani ya mifupa kwa miezi mitano.

Alipoulizwa kama kuna uwezekano wowote wa Enrique akarudi kuinoa timu ya taifa, Moreno aliwaambia waandishi wa habari Jumanne: "Hilo halina ubishi na hakutakuwa na muda wa kulijadili.

"Namchukulia Luis kama rafiki yangu na urafiki ni zaidi ya kila kitu. Kama siku moja anataka kurudi, sitakuwa na kikwazo chochote kwake na mimi nitakuwa wa kwanza kuachia ngazi kumpisha yeye. Nilifurahia wakati nikiwa nae kabla."

Moreno, ambaye tangu mwaka 2011 amefanya kazi kama msaidizi wa Enrique katika klabu za Celta Vigo, AS Roma, Barcelona na timu ya taifa ya Hispania, alifuta mkutano wake na waandishi wa habari Ijumaa iliyopita kwa ajili ya kutangaza kikosi cha timu ya taifa, baada ya taarifa ya kifo cha Xana.

"Imekuwa wiki mbaya,"Moreno alisema. "Tutajaribu kumpa furaha kidogo wakati huu wa kipindi kigumu.

"Kitu pekee ambacho tunaweza kukifanya."

Moreno pia aliulizwa uwezekano wa 'dogo' wa Barcelona, Ansu Fati kuvaa jezi ya timu ya taifa ya Hispania.

Fati mwenye umri wa miaka 16, alikuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kuichezea Barcelona na kufunga bao kwenye La Liga wakati wakitoka sare ya kufunga bao 2-2 na Osasuna.

"Tunaweza kumuamini," Moreno alisema. "Anatakiwa kuendelea kujiimarisha zaidi katika umri wake."



# ABRAHAM AOMBWA AICHEZEE NIGERIA




**LONDON,** England

NAGERIA imeanzisha mpango wa kujaribu kumshawishi mshambuliaji wa Chelsea, Tammy Abraham kuitosa England na kuiwakilisha Super Eagles kwenye mechi za kimataifa.

Kustaafu kwa Odion Ighalo baada ya Nigeria kumaliza ikiwa nafasi ya tatu kwenye michuano ya mataifa ya Afrika, Nigeria inatafuta mshambuliaji mpya wa mbele.

Abraham mzaliwa wa Camberwell aliichezea kwa mara ya kwanza England kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Ujerumani Novemba mwaka 2017 kabla ya kucheza dhidi ya Brazil wiki moja baadae na bado hajacheza mchezo wowote wa mashindano katika kikosi hicho cha kocha, Gareth Southgate, hali ambayo inamfanya kuweza kuichezea timu nyingine ya taifa.

Rais wa Shirikisho la soka la Nigeria, NFF, Melvin Amaju Pinnick amesema: "Hatutakata tamaa kuwaomba wachezaji wazuri kuichezea nchi yetu. Tunaendelea kuzungumza na wachezaji wazuri wenye asili ya Nigeria kuichezea nchi ya baba yao.

"Lakini kama ninavyojua, vijana hawa wana mawazo yanayojitegemea. Kiukweli tumeambiwa kusubiri hadi Aprili 2020, wakati matumaini ya kufanya maamuzi ya mwisho yatakapofikia.

# Hazard na mdogo wake wajiondoa

**BRUSSLES,** Ubelgiji

EDEN na Thorgan Hazard wote wamelazimika kujiondoa kwenye kikosi cha timu ya taifa ya Ubelgiji kwa ajili ya mechi za kimataifa zinazokuja baada ya kuumia.

Eden bado hajaichezea Real Madrid kwenye Ligi Kuu tangu atue hapo kutoka Chelsea kipindi cha majira ya joto msimu huu, kwani anaendelea kujiuguza majeruhi ya nyama za paja.

Pia mdogo wake, Thorgan ambaye amejiunga na klabu ya Borussia Dortmund - ameichezea mechi tatu msimu hu, lakini hivi karibuni alilazimika kukaa benchi dhidi ya Union Berlin kutokana na majeruhi.

Chama cha soka cha Ubelgiji kimethibitisha kwamba wawili hao hawatacheza mechi zijazo za kimataifa za kufuzu kwenye mashindano ya Ulaya dhidi ya San Marino na Scotland.

Hakuna ishara kama kocha, Roberto Martinez ataongeza mchezaji yoyote kwa ajili ya kuziba nafasi zao kabla ya mchezo wa kwanza dhidi ya San Marino Ijumaa.

Kocha wa Real Madrid, Zinedine alishasema kuhusu Eden kuitwa kwenye kikosi cha taifa akibainisha kwamba, winga huyo hatakuwa fiti kuichezea nchi yake mechi za hivi karibuni.

"Ndio anaweza kusafiri na Ubelgiji, lakini kwa wakati huu hawezi kucheza," alisema Zidane katika mkutano wake na waandishi wa habari Jumamosi.

"Anajua hilo, tuna matumaini kwamba hatacheza, kwa ajili ya kila mmoja kuhakikisha anakuwa fiti zaidi ikiwamo Ubelgiji yenyewe."



# Klabu EPL zataka kuongeza muda usajili

**LONDON,** England

KLABU kubwa za Ligi Kuu ya England zinataka kuongezewa muda wa kufungwa kwa dirisha la usajili ili kuwa sawa la lile la Ulaya, kwa mujibu wa ESPN FC.

Nyota wa Manchester United, Paul Pogba na kiungo wa Tottenham, Christian Eriksen walikuwa wakihusishwa na uhamisho wa kwenda Real Madrid, licha ya dirisha la England kufungwa Agosti 8 mwaka huu.

Jambo hilo litajadiliwa kwenye mkutano na mwenyekiti wa Ligi Kuu, Septemba 12, ambapo klabu 11 kati ya 20 zitakiwa kusapoti hoja hiyo ili ishinde na maamuzi ya mwisho yatatolewa Novemba mwaka huu.

Dirisha la usajili la England linafungwa mapema zaidi ya ligi nyingine za Ulaya na hivyo timu kushindwa kusajili wachezaji wapya kama wachezaji wao watasajiliwa wakati dirisha lao likiwa limefungwa.

Kwani ligi nyingine za Ulaya dirisha lake la usajili linafungwa Septemba 2 wakati lile la England linakuwa limeshafungwa.

United imeshuhudia Alexis Sanchez na Chris Smalling wakiondoka kwenda kujiunga na klabu za Inter Milan na Roma pamoja na Matteo Darmian akijiunga moja kwa moja na Parma wakati dirisha la usajili la England likiwa limefungwa.

Henrikh Mkhitaryan yeye aliondoka Arsenal kwenda kujiunga na AS Roma kwa mkopo.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RAMOS AONYWA KIKOSI CHA KWANZA HISPANIA

Atakuwa na ushindani, ninaweza kusema mambo mazuri tu kuanzia muda nilipokuwa...

**MADRID,** Hispania

SERGIO Ramos hapaswi kuendelea kujihakikisha kuanza kikosi cha kwanza katika timu ya Taifa ya Hispania, Kocha Mkuu, Robert Moreno amemuonya.

**Beki huyo wa kati mwenye umri wa miaka 33, amekuwa na wakati mgumu katika ngazi ya klabu kwa mwaka huu, wakati huu Real Madrid ikiwa imeshinda mechi nne tu kati ya 12 za La Liga kuanzia za msimu uliopita.**

Sare mbili mfululizo dhidi ya Real Valladolid na Villarreal kumeongeza maswali zaidi kuhusu safu ya ulinzi ya Madrid na kiwango cha Ramos kwa ujumla.

Moreno amemtetea Ramos, ambaye ameichezea timu ya taifa ya wakubwa mara 165, akimwelezea kama mchezaji mwenye "tabia nzuri" ambaye anaweza kusaidia kizazi kijacho katika nafasi ya beki wa kati kikosini hapo.

Hata hivyo, amesema Ramos atakuwa amewekwa katika uhitaji mkubwa kuliko mchezaji mwingine yeyote kwenye kikosi cha Hispania wakati huu wakijiandaa na mechi ya kuwania kufuzu fainali za Euro 2020 dhidi ya Romania na Visiwa vya Faroe.

"Kwa namna ilivyo ndiyo, Sergio atacheza. Lakini ninamtaka kufikiri kama hayupo sawa, hatacheza," alisema Moreno.

"Nimefurahi kuwa vijana wana Sergio kando yao kwa sababu atawasaidia sana. Tunacho kizazi kizuri cha mabeki wa kati na sidhani kama tutakuwa na 'pacha' mzuri kwa Sergio, lakini tutakuwa na mbadala [pia].

"Atakuwa na ushindani. Ninaweza kusema mambo mazuri tu kuanzia muda nilipokuwa naye. Ana tabia nzuri. Yeye ni mfano kwa wote, katika mazoezi, nje... Sergio ni mmoja ambaye nitahitaji mengi kutoka kwake."

Moreno pia aliulizwa kuhusu maendeleo ya Ansu Fati, ambaye alikuwa mfungaji bora kinda wa Barcelona kwenye La Liga wakati wakicheza dhidi ya Osasuna Jumamosi wakati akiwa na umri wa miaka 16 na siku 304.

"Hatuwezi kumharakisha," Moreno alisema. "Lazima aruhusiwe kuendelea kupitia kila hatua.

"Alikuwa mchezaji kinda tu hadi hivi karibuni na sasa anacheza huko Camp Nou. Lazima tuwe na subira sana kwa kila maana. Ninajua [Kocha wa Barcelona] Ernesto [Valverde] atamwongoza vema, lakini ikiwa atacheza na kikosi cha wachezaji wa akiba au vijana, hakuna kitu kibaya na kwa hilo. "

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMTEGA ERIKSEN

MANCHESTER United itajaribu kuinasa saini ya kiungo wa Tottenham, Mdenmark Christian Eriksen, 27, kwa punguzo ya dau Januari wakati huu akiwa mwaka wake wa mwisho kwenye mkataba wake. ***(Sun)***

### MANDZUKIC, CAN WAKATWA

JUVENTUS imewakata kiungo Mjerumani Emre Can, 25, mshambuliaji wa zamani wa Croatia, Mario Mandzukic, 33, na beki Muitaliano Giorgio Chiellini, 35, kutoka katika kikosi chake kitakachoshiriki Ligi ya Mabingwa msimu huu wa 2019-20. ***(Football Italia)***

### MADRID YAMWACHA HURU SILVA

REAL Madrid walikuwa na makubaliano ya pande zote na kiungo Lucas Silva, 26, kuhusu kuvunja mkataba, hiyo ikiwa na maana Mbrazil huyo sasa ni mchezaji huru. ***(Marca)***

### SESSEGNON AWINDWA SPURS

TOTTENHAM inataka kumsajili beki wa Fulham na England U-20, Steven Sessegnon, 19, ambaye anaweza kucheza kama beki wa pembeni, kati na kiungo- ikiwa ni mwezi mmoja baada ya kumnasa kama pacha wake, Ryan kwa pauni milioni 25. ***(Sun)***

### SARRI AMTAKA WILLIAN

WINGA wa Chelsea, Mbrazil Willian, 31, anatakiwa na kocha wake wa zamani anayeinoa Juventus kwa sasa, Maurizio Sarri wakati akiwa mwaka wake wa mwisho kwenye mkataba wake hapo Stamford Bridge. ***(Express)***

### CAKIR APIGIWA HESABU LIVER

LIVERPOOL inamfuatilia kipa wa Trabzonspor, Ugurcan Cakir anayeelezwa kuwa na thamani ya pauni milioni 14. 'Wekundu' hao walimtazama kipa huyo mwenye umri wa miaka 23 wakati wakitoka sare ya bao 1-1 na Fenerbahce wiki iliyopita. ***(Mail)***

### WENGER KURUDI MZIGONI

KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger, anafikisha umri wa miaka 70 Oktoba mwaka huu, anataka kurudi kazini - ikiwa ni miezi 16 baada ya Mfaransa huyo kuhitimisha miaka 22 ya kuinoa 'Gunners'. ***(Sun)***

### LIVER, CHELSEA KWA GELHARDT

LIVERPOOL na Chelsea zinamfukuzia mshambuliaji wa Wigan Athletic, Joe Gelhardt, 17, ambaye amecheza mechi mara tatu katika kikosi cha kwanza. ***(Mirror)***

### SABABU BAYERN KUMKOSA SANE

BAYERN Munich ambayo ilijaribu kumsajili winga wa Manchester City, Leroy Sane, 23, kipindi cha majira ya joto walishindwa kufanikisha kutokana na mshahara mkubwa aliohitaji. ***(Manchester Evening News)***

### TRIPPIER AFUNGUKA ATLETICO

BEKI wa kulia wa England, Kieran Trippier, 28, amesema kujiunga na Atletico Madrid akitokea Tottenham ni "hatua moja mbele". ***(Diario AS - in Spanish)***

### SMALLING KUBAKI ROMA

BEKI wa Manchester United na England, Chris Smalling, ambaye amejiunga na Roma kwa mkopo kwa kipindi kilichobaki cha msimu, anaweza kubaki Italia baada ya msimu huu. ***(Manchester Evening News)***

**HABARI MICHEZO**

# WIMBO WA MSECHU ROHO JAMAFEST 2019

**Na Mwandishi Wetu**

WIMBO mpya wa Jamafest 2019 ulioimbwa na msanii Peter Msechu, umeteuliwa kuwa wimbo maalum katika Tamasha la Utamaduni la Afrika Mashariki linalotarajiwa kufanyika nchini kuanzia Septemba 21-28, mwaka huu katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Taarifa za wimbo wa Jamafest 2019 kuteuliwa kuwa wimbo rasmi wa tamasha hilo maarufu Afrika Mashariki zilifahamika baada ya Msechu kuandika katika ukurasa wake wa Instagram akimshukuru Mungu kwa wimbo wake huo kupitishwa.**

Akizungumza kwa njia ya simu kutoa ufafanuzi juu ya kuchaguliwa kwa wimbo huo kuwa maalum katika tamasha la Jamafest, Msechu alisema alituunga baada ya uongozi wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuwaomba wasanii mbalimbali kutunga wimbo ambao ungetumika kama wimbo maalum wa tamasha.

"Wasanii tupo wengi sana kwa mimi kupata fursa hii ya kuimba katika ufunguzi wa tamasha hili kubwa la Jamafest kwangu ni heshima kubwa sana. Tulikuwa wasanii wengi tuliotunga nyimbo kwa ajili ya tamasha, lakini wimbo wangu umechaguliwa ni furaha kubwa," alieleza Msechu.

Alisema kwa sasa anaandaa video ya wimbo huo ili uweze kutumika kuhamasisha Watanzania na watu wa Afrika Mashariki kushiriki katika tamasha ambalo lina lengo la kudumisha urithi wa utamaduni, sanaa za mikono na ubunifu.

Akizungumzia wimbo huo, Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Maandalizi ya Tamasha la JAMAFEST, Joyce Fissoo, alisema mchakato wa uteuzi wa wimbo rasmi kwa ajili ya tamasha hilo haukuwa na rahisi kwani kulikuwa na ushindani mkubwa kutokana na wasanii wengi kujitokeza na kufanya utunzi wa wimbo.

"Mchakato wa kupata wimbo wa tamasha ulikuwa mgumu kutokana na wasanii kujitokeza na baada ya kusikiliza nyimbo zote ndipo sekretarieti ya maandalizi ya tamasha inayoundwa na wajumbe kutoka nchi sita wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikauchagua wimbo wa Jamafest 2019 ulioimbwa na Msechu kuwa ndio wimbo wa tamasha," alieleza Fissoo.

Tamasha la Jamafest ni tamasha lililopitishwa na Baraza la Mawaziri la Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuenzi na kulinda utamaduni wa makabila ya Afrika Mashariki. Tamasha hili hufanyika kila baada ya miaka miwili katika nchi wanachama ambapo mwaka huu litafanyika nchini kuanzia Septemba 21-28 katika Uwanja wa Taifa.

## Kiungo Mtanzania atamani kutua EPL

**Na Mwandishi Wetu**

KIUNGO mshambuliaji wa Minnesota United ya Marekani, Mtanzania Ally Ng'anzi, amesema anamshukuru Mungu kupata nafasi katika klabu hiyo, lakini ndoto yake kubwa ni kuona anasajiliwa na klabu mojawapo inayoshiriki Ligi Kuu England.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ng'anzi, alisema kila siku amekuwa akipambana kufanya vema katika timu yake kuanzia mazoezini, hadi kwenye michezo ya ligi, kwa sababu anataka kuona anafanikiwa kuwashawishi mawakala wanaofuatilia ligi hiyo.

Ng'anzi alisema anaamini mchezaji yeyote ambaye anajituma, kufikia mafanikio ni jambo la kawaida na si miujiza.

"Naendelea vizuri katika timu yangu, ninafanya mambo makubwa kila ninapopata nafasi ya kucheza, kwa sababu ninataka kutimiza ndoto yangu ya kwenda kucheza Ligi Kuu ya England, bado sijafika mwisho," alisema mshambuliaji huyo wa zamani wa Singida United ya mkoani Singida.

## Kagera watamba kuimaliza Alliance

**Na Philip Nyiti,** Tudarco

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa imesimama kupisha timu ya Taifa (Taifa Stars), inayokabiliwa na mechi za kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Dunia nchini Qatar 2022, benchi la ufundi la Kagera Sugar limetamba kutumia vema mapumziko hayo ili kujiandaa kuwakabili Alliance FC.

Kagera Sugar itasafiri kuwafuata Alliance FC katika mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara, ambayo itachezwa Septemba 14, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba jijini Mwanza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, alisema kikosi chake kinaendelea vema na mazoezi na wamefurahia kupata mapumziko hayo kwa sababu wachezaji wake wanaendelea kujiimarisha pamoja.

Maxime alisema anafahamu mchezo huo utakuwa mgumu na wenye ushindani kutokana na wenyeji wao kuimarika zaidi tofauti na walivyokuwa katika msimu uliopita.

"Tunaendelea vema na mazoezi, tumejiandaa kupambana na kwa sababu tutakuwa ugenini, tunatarajia pia kuondoka na matokeo mazuri kama tulivyopata katika mechi ya kwanza dhidi ya Biashara ya Mara," alisema Maxime.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya KCB Tanzania, Cosmas Kimario, akikabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 495.6 kwa Rais wa TFF, Wallace Karia (kushoto), kwa ajili ya udhamini wa Ligi kuu Tanzania Bara. Wanaoshuhudia hafla hiyo ya makabidhiano iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana, watatu kutoka kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya KCB Tanzania, John Ulanga, Mkuu wa Idara ya Masoko wa Benki hiyo, Christine Manyeye na Mwanasheria Mkuu wa Benki ya KCB, Anthonia Kilama (kulia). **NA MPIGAPICHA WETU**

# *KCB yaimwagia Ligi Kuu Bara milioni 495/-*

**Na Mwandishi Wetu**

LIGI Kuu Tanzania itazidi kunoga na kuongezeka ushindani kufuatia Benki ya KCB Tanzania kuingia mkataba na Shirikisho la Soka nchini (TFF) wa kuwa mdhamini mwenza katika msimu huu wa 2019/20.

KCB Tanzania sasa inaungana na Kampuni ya Vodacom ambayo ni mdhamini mkuu baada ya mwezi uliopita kampuni hiyo ya mawasiliano kuingia mkataba na TFF wa kuidhamini ligi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu kwa thamani ya Sh. bilioni tisa.

Kwa upande wa KCB, mkataba wao una thamani ya Sh. milioni 495.6 kabla ya kodi, na ulitiwa saini na Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Cosmas Kimario na Rais wa TFF, Wallace Karia katika Hoteli ya Hyatt Regency jijini Dar es Salaam jana na kushuhudiwa na Mwenyekiti wa Bodi ya KCB Tanzania, John Ulanga, Katibu Mkuu TFF, Kidao Wilfred, Mwenyekiti wa Bodi

ya Ligi Kuu, Steven Mnguto na Mkurugenzi wa Bodi ya Ligi, Boniface Wambura pamoja na Wakurugenzi wa Bodi wa wafanyakazi wa Benki ya KCB Tanzania.

Hii ni mara ya tatu kwa KCB Tanzania kudhamini ligi hiyo, mara ya kwanza ilikuwa msimu wa 2017/18 ambapo ilidhamini Ligi Kuu kwa Sh. milioni 325 na kuongeza udhamini kwa msimu uliofuata wa 2018/19 hadi kufikia Sh. milioni 420.

Akizungumza katika halfa ya utiaji saini mkataba huo jana, Mtendaji wa Benki ya KCB Tanzania, Cosmas Kimario alisema mafanikio makubwa yaliyopatikana kwa udhamini wa misimu iliyopita ndiyo yameivutia KCB Tanzania kuendeleza udhamini

huo na kuwa Sh. milioni 495.6

ambapo kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia msimu wa 2017/18 hadi 2019/20 udhamini wao utakuwa jumla ya Sh. bilioni 1.16.

Kimario alisema pamoja na

dhamira ya benki hiyo kurudisha kwa jamii, udhamini huo pia ni fursa kubwa kwa KCB kuwekeza kwenye sekta yenye kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa kukuza ajira na

vipaji vya vijana wa Kitanzania.

"Matarajio ya benki yetu ni kuona Watanzania wengi zaidi

wanapata ajira kupitia sekta mbalimbali tunazozigusa, " alisema.

Rais wa TFF, Karia mbali na kuishukuru KCB Tanzania kwa kuidhamini Ligi kuu Bara, alisema udhamini wao utasaidia kufanikisha msimu huu wa 2019/20 huku akizitaka taasisi zingine na watu binafsi kuiga mfano huo.

Michezo
Alhamisi Septemba 5, 2019
Nipashe



Abraham aombwa aichezee Nigeria UKURASA 29



Washambuliaji wa Taifa Stars, mfungaji wa bao, Simon Msuva na Mbwana Samatta ambaye alifanya kazi kubwa kuhakikisha anamzuia beki wa Burundi kuokoa mpira wa Msuva uliokuwa ukijaa wavuni kwenye mechi ya jana. **PICHA: MAKTABA**

# Stars yachungulia hatua ya makundi

## ●●● Mbinu za Ndayiragiji zakubalika, wagoma kuingia chumba cha kubadilishia, Msuva asawazisha usiku...

**Na Mwandishi Wetu,** BUJUMBURA

TIMU ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), imetanguliza mguu mmoja ndani kufuzu hatua ya makundi ya kuwania kushiriki Kombe la Dunia nchini Qatar 2022 baada ya jana kulazimisha sare ya bao 1-1 dhidi ya wenyeji wao, Burundi.

**Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Mashujaa mjini Bujumbura, Burundi, Taifa Stars ilikataa kuingia katika vyumba vya kubadilishia wakati wa mapumziko baada ya kubaini kuchezewa mchezo mchafu, hivyo kupewa maoni na kocha katika benchi kwa muda wote wa dakika 15.**

Wenyeji ndio walikuwa wa kwanza kupata bao kupitia kwa mshambuliaji wake, Amissi Cedric ambaye aliwahi krosi iliyopigwa na Amissi Mohammed na kuwapita wachezaji watatu wa Taifa Stars, Farid Mussa, Jonas Mkude na Gadiel Michael waliokuwa jirani na golikipa, Juma Kaseja.

Hata hivyo, bao hilo lilidumu kwa dakika tano tu baada ya Simon Msuva kuisawazishia Taifa Stars baada ya kuwahi mpira mrefu uliopigwa na Gadiel na kumzidi mbinu beki wa Burundi na kupiga mpira uliotinga wavuni moja kwa moja huku nahodha wake, Mbwana Samatta, akifanya kazi kubwa ya kumzuia beki wa Burundi asiucheze.

Kwa matokeo hayo, sasa Stars inayofundishwa na Mrundi Etienne Ndayiragije ambaye mbinu zake zilionekana kufaulu, inahitaji ushindi wa aina yoyote ama sare tasa ili iweze kutinga hatua ya makundi ya kuwania tiketi ya kushiriki fainali hizo za Kombe la Dunia nchini Qatar 2022.

Dakika 10 za kwanza za mchezo huo ambao makipa wote wawili, Juma Kaseja wa Taifa Stars na Jonathan Nahimana wote wanaichezea klabu ya KMC FC ya jijini Dar es Salaam, zilimalizika bila kuwapo kwa shambulizi kutokana na washambuliaji kukosa utulivu wanapokaribia kwenye lango la wapinzani wao.

Kipa wa Burundi, Nahimana aliinyima bao Taifa Stars baada ya kupangua shuti la Msuva na baadaye kiungo Hassan Dilunga alichelewa kuunganisha krosi iliyopigwa na Samatta dakika ya 16.

Burundi ilijibu shambulizi hilo, lakini mshambuliaji wake, Bimenyimana Be-Fils Caleb ambaye alikuwa amefanikiwa kumpita beki wa Stars, Haruna Shamte alipiga pembeni na kuikosesha timu yake nafasi ya kufunga.

Dakika ya 50 Stars ilikosa nafasi nyingine ya kupata bao baada ya mpira wa 'frikiki' uliopigwa na Samatta kugonga ukuta wa Burundi huku wenyeji hao pia wakipoteza nafasi ya kufunga kwa straika wake, Abdoul Fiston, kupiga pembeni wakati ameshafanikiwa kumtoka Mkude na kubakia peke yake na kipa Kaseja.

# Zahera: Hesabu Yanga zitatimia

**Na Somoe Ng'itu**

HESABU zitatimia! Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, amesema kikosi chake kinafanya mazoezi kwa kufuata "hesabu" ili waweze kupata ushindi katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Zesco kutoka Zambia, ambayo inatarajiwa kuchezwa Septemba 14, mwaka huu kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zahera, alisema programu ya mazoezi pamoja na mechi ya kirafiki watakayocheza jijini Mwanza, ni moja ya mipango ya kuwaimarisha wachezaji wake kabla ya kuwavaa Wazambia katika mchezo wa kwanza ambao wanahitaji kupata matokeo mazuri.

Zahera alisema kila mchezaji anafahamu umuhimu na changamoto ambazo watakutana nazo kwenye mchezo huo, hivyo kuwa imara na tayari kuwadhibiti wapinzani wao, ndilo jambo muhimu kwa sasa.

"Nimekubali timu yetu iende Mwanza kwa sababu maalumu, najua huko kila kitu kitakwenda vizuri, hesabu zangu zitatimia, wachezaji watapata nafasi ya kufanya mazoezi na kujipima kwenye uwanja mzuri, naamini malengo yetu ya kuwafunga Zesco yatatimia, tunaendelea kujipanga ili tuweze kufikia malengo yetu ya msimu huu," alisema Zahera.

Yanga ilisonga mbele katika michuano hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya kuwaondoa Township Rollers ya Botswana kwa jumla ya mabao 2-1 na kuwa klabu pekee ya Tanzania inayoshiriki Ligi ya Mabingwa na kimataifa ikiungana na Azam FC inayopeperusha bendera ya Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Baada ya mchezo huo, Yanga iliyoanza msimu mpya kwa kufungwa bao 1-0 na Ruvu Shooting ya Mlandizi, mkoani Pwani, itarejesha nguvu zake katika Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kujiandaa kuwakabili Mbeya City ya jijini Mbeya katika mechi itakayochezwa Septemba 18, mwaka huu kwenye Uwanja Sokoine.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >